# Nipashe

Ijumaa Februari 22, 2019 • Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

ISSN 0856 • Na. 0579848

MWANGA WA JAMII

www.ippmedia.com

twitter.com/nipashetz

www.facebook.com/nipashetz

www.instagram.com/theguardian_newspaper

LIKE & FOLLOW US




## Hatima uenyekiti wa Lipumba bayana leo

UKURASA 3




UKURASA 13

# Acacia, Barrick 'lugha gongana'

• **Ni** kuhusu malipo ya bil. 682/- kwa Tanzania, moja yasema uamuzi wa mwisho ni wa bodi ya wakurugenzi... *Endelea ukurasa 2*

## YALIYOMO

UKURASA WA 2

**MBOWE, MATIKO WATIMIZA SIKU 90 WAKIWA MAHABUSU**

MBUNGE wa Hai ambaye pia ni Mwenyekiti wa Chama cha Demokrasia na Maendeleo (Chadema), Freeman...

UKURASA WA 26

**WEMA AKANA KUSAMBAZA PICHA NGONO MTANDAONI**

MSANII wa Filamu nchini, Wema Sepetu (30), amekana mahakamani tuhuma za kuchapisha video ya...

## Mwanafunzi sekondari ajiua kwa kujipiga risasi

UKURASA 3



Dereva wa bodaboda Masoud Ramadhan (kushoto), wa Kimara Temboni, akiwa na majeraha yaliyosababishwa na kipigo katika jaribio la kuporwa pikipiki yake na majambazi katika eneo la Suka jijini Dar es Salaam mapema wiki hii. Kulia ni Ally Kayombo, ambaye ni dereva wa bodaboda aliyeporwa pikipiki yake na majambazi baada ya kutishiwa kwa bastola katika eneo la Makuburi Mabibo. **PICHA: BEATRICE MOSES**



UKURASA 2

## Uporaji bodaboda kwa mtutu washamiri Dar

**MICHEZO** **SIMBA, AZAM FC KUMALIZA UBISHI** UK.32

**MAONI, KATUNI** UK.6

# Mbowe, Matiko watimiza siku 90 mahabusu

**Na Enock Charles**

MBUNGE wa Hai ambaye pia ni Mwenyekiti wa Chama cha Demokrasia na Maendeleo (Chadema), Freeman Mbowe na Mbunge wa Tarime Mjini, Ester Matiko, wametimiza siku 90 mahabusu ambazo ni sawa na miezi mitatu. Mbowe na Matiko walifutiwa dhamana zao Novemba 23, mwaka jana, baada ya kutohudhuria mahakamani katika siku ambazo kesi yao ilikuwa ikitajwa.

Baada ya kufutiwa dhamana, Mbowe na Matiko kupitia mawakili wao walikata rufani mara kadhaa Mahakama Kuu bila mafanikio kuhusu uamuzi huo na kwa mara ya mwisho ilikuwa Jumatatu ya wiki hii kesi yao ilipofika mahakama ya rufani.

Jumatatu, Mkurugenzi wa Mashtaka (DPP) alikata rufani Mahakama ya Rufani kupinga uamuzi wa Mahakama Kuu kukubali kuendelea na usikilizaji wa rufani ya wabunge hao ya kupinga uamuzi wa Mahakama ya Hakimu Mkazi Kisutu kuwafutia dhamana.

Katika kesi iliyosikilizwa katika mahakama hiyo ambayo ndiyo ya mwisho katika uamuzi, Mbowe na Matiko walirejeshwa mahabusu baada ya mahakama hiyo kusema itatoa uamuzi wa rufani iliyokatwa na DPP dhidi yao tarehe na siku itakayopangwa, hivyo kufanya wabunge hao kuendelea kusota rumande.

Katika kesi ya msingi, Mbowe, Matiko na viongozi wengine saba wa Chadema wanakabiliwa na mashtaka 13 ikidaiwa kuwa kati ya Februari 1 na 16, mwaka jana jijini Dar es Salaam, walikula njama, kufanya mkusanyiko wenye ghasia na uchochezi na kuhamasisha hisia za chuki na kuwa kwa kufanya hivyo ni kosa la jinai.

Mbali na Mbowe na Matiko, washtakiwa wengine ni Naibu Katibu Mkuu Zanzibar, Salum Mwalimu; Naibu Katibu Mkuu Bara na Mbunge wa Kibamba, John Mnyika; Mbunge wa Tarime Vijijini, John Heche; Mbunge wa Iringa Mjini, Peter Msigwa; Mbunge wa Kawe, Halima Mdee; Mbunge wa Bunda Mjini, Esther Bulaya na Katibu Mkuu wa chama hicho, Dk. Vincent Mashinji.

Awali, Mahakama ya Hakimu Mkazi Kisutu ilitoa ruhusa kwa Mdee ahudhurie michezo ya mabunge ya Afrika Mashariki nchini Burundi na pia kwa Mbunge wa Tarime Vijijini kumuuguza mkewe.

Katika kesi hiyo, mara zote pamekuwa na ulinzi mkali kila inapotajwa hali inayoonyesha ni ya kukabiliana na wafuasi wa chama hicho kikuu cha upinzani nchini, iwapo wataanzisha vurugu.

# Acacia, Barrick zagongana bil. 682/-

**Na Mwandishi Wetu**

SIKU moja baada ya Ofisa Mwendeshaji Mkuu wa Kampuni ya Barrick Gold, Dk. Willem Jacobs, kumhakikishia Rais John Magufuli kuwa watalipa Sh. bilioni 682 walizoahidi mwezi ujao, kampuni mwenza ya uchimbaji madini ya Acacia imeibuka na kusema bado haijapokea mapendekezo yoyote kuhusu malipo hayo.

Acacia, ambayo ni moja ya kampuni zinazoendeshwa na kampuni mama ya Barrick Gold ya Canada inayoendesha shughuli zake za uchimbaji Tanzania, katika taarifa yake jana, ilieleza kuwa bado haijapokea mapendekezo yoyote kutoka Barrick kuhusu maazimio ya mazungumzo yaliyofanyika baina ya kampuni hiyo na serikali.

"Acacia bado haijapokea mapendekezo yoyote kutoka Barrick. Mapendekezo yoyote yatakayotoka yatafanyika kazi na Bodi ya Wakurugenzi ya Acacia," alisema.

Juzi, Rais Magufuli na mwendeshaji mkuu huyo wa Barrick Gold anayeshughulikia Afrika na Mashariki ya Kati, walifanya mazungumzo Ikulu na kumhakikishia Rais kuwa watalipa fedha walizoahidi mwezi ujao.

Baada ya mazungumzo hayo, kwa mujibu wa taarifa hiyo iliyotolewa siku hiyo, Dk. Jacobs aliyeongozana na washauri wa Barrick Gold Corporation, Rich Haddock, Duncan Vullivant na Wicus du Preez, alisema wamekutana na Rais Magufuli na kumhakikishia kuwa makubaliano yaliyofikiwa Oktoba 19, 2017 watayatekeleza kikamilifu baada ya kampuni kubwa ya uchimbaji dhahabu ya Rand Gold ya Afrika Kusini kuungana na Barrick Gold Corporation katika umiliki, uwekezaji na menejimenti.

Dk. Jacobs alisema hakuna kitakachokuwa tofauti na makubaliano yaliyofikiwa awali ambayo yaliongozwa na Mwenyekiti Mtendaji wa Barrick Gold Corporation, Prof. John Thornton, ikiwamo Barrick Gold Corporation kuilipa serikali ya Tanzania kifuta machozi cha dola za Marekani milioni 300 (sawa na Sh. bilioni 682.5).

Makubaliano mengine ni kuendelea na uwekezaji kwa ubia katika ya serikali ya Tanzania na Barrick Gold na mgawanyiko wa mapato ya kiuchumi kwa uwiano wa asilimia 50 kwa 50 kati ya Tanzania na kampuni hiyo.

Taarifa hiyo iliyotolewa na Ikulu juzi, ilisema Dk. Jacobs alimpongeza Rais Magufuli kwa jitihada zake za kusimamia maslahi ya Watanzania katika rasilimali za nchi na kwamba pamoja na ukweli kwamba Rais yuko katika njia sahihi, akiwa Mwafrika anaunga mkono juhudi hizo kwa kuwa ndio mwelekeo sahihi ambao nchi za Afrika zinapaswa kuufuata.

"Mimi ni Mwafrika na sisi sote ni Waafrika. Anachofanya Rais Magufuli ni sahihi kabisa, anahakikisha utajiri wa rasilimali uliopo unabainishwa na unawanufaisha Watanzania ndiyo maana tupo hapa kwa sababu tunakubaliana na Rais," alisema.

INAENDELEA UK. 26



Mkurugenzi Mtendaji wa Taasisi ya Sekta Binafsi (TPSF), Godfrey Simbeye (katikati), akizungumza na waandishi wa habari, jijini Dar es Salaam jana, kuhusu kuongezeka kwa kasi ya majadiliano ya kisekta, kimkoa na kitaifa baina ya sekta ya umma na sekta binafsi na mkutano wa majadiliano ya kitaifa ya kutathmini maendeleo ya sekta binafsi unaotarajiwa kufanyika mwezi Mei mwaka huu. **PICHA: JOHN BADI**


**Majembe Auction Mart Ltd.**
**(VIJANA WA KAZI)**

215074502

**NOTISI /MNADA WA HADHARA**

**MAJEMBE AUCTION MART LTD.** KWA IDHINI TULIYOPEWA NA **BRAC TANZANIA FINANCE LTD.** S.L.P 105213 DAR ES SALAAM TUNATOA NOTISI YA SIKU KUMI NA NNE (14) KUANZIA SIKU YA TANGAZO HILI KWA WADAIWA WOTE NA WADHAMINI MLIPE MADENI YENU YOTE VINGINEVYO TUTAUZA KWA MNADA WA HADHARA DHAMANA YA MDAIWA MAHALI DHAMANA ILIPO.

| Na. | Jina la Mkopaji/ Mdhamini | Aina ya Dhamana | Eneo lilipo | Tarehe | Saa |
|---|---|---|---|---|---|
| 1. | Hawa Iddy Mweta/ Abas Mohamedi | Kiwanja chenye nyumba urefu futi 46 na upana ft 30 | Mwanama mtaa wa mbeshere kata ya Oleirien | 07.3.2019 | 5.00 asubuhi |

**Masharti ya mnada**
1. Ukaguzi utaruhusiwa siku mbili kabla ya mnada.
2. Mnunuzi atatakiwa kulipa 25% ya bei iliyofikiwa kwenye mnada (au zaidi) na salio la 75% litalipwa ndani ya siku kumi na nne (14)
3. Endapo mshindi atashindwa kulipa salio la 75% kwa muda uliotolewa atakuwa amepoteza haki yake na mali itauzwa upya.

**Kwa masiliano zaidi wasiliana nasi kwa simu:**
**0767 608090, 0754 475932, 0754 374351, 0625 666247**


# Uporaji bodaboda kwa mtutu tishio Dar

**Na Beatrice Moses**

MAUAJI na uporaji wa pikipiki kwa kutumia mtutu wa silaha za jadi yanadaiwa kuendelea kushamiri katika maeneo ya vijiwe vya Kimara hadi Mbezi wilayani Ubungo, jijini Dar es Salaam.

Vijana wawili waliokuwa wanafanya shughuli zao kwenye vijiwe vilivyoko maeneo ya Mpakani kwa Msuguri, wanadaiwa kuuawa kwa risasi wiki iliyopita, wengine kujeruhiwa kisha kuporwa pikipiki.

Hali hiyo imezusha hofu kwa waendesha bodaboda kadhaa, ambao wameliomba Jeshi la Polisi kuwasaidia kuwanasa majambazi husika ili wafanye kazi hiyo katika hali ya usalama.

Akizungumza na gazeti hili, Ally Kayombo, anayefanya shughuli zake katika kijiwe cha Temboni, alisema wiki iliyopita alishiriki kwenye mazishi ya vijana waliouawa na kuporwa pikipiki kwa Msuguri hakujua kama naye alikuwa mawindoni.

Kayombo alisema kuwa Ijumaa ya Februari 15, mwaka huu akiwa kijiweni kwake aliitwa na dereva taksi wa kijiweni hapo akamjulisha kuna mteja anataka kufuatiwa mzigo wake Makuburi Mabibo, akazungumza naye wakakubaliana bei.

Alisema kuwa yule mteja alibaki pale Temboni wakati yeye anaondoka akampa namba ya mtu aliyepaswa kumpa mzigo, lakini alipofika kule alipiga simu haikupokelewa, akamjulisha mteja wake akamwambia amsubiri.

"Baada ya muda yule alifika akanielekeza tukasogea kwenye gari nikiamini wanatoa mzigo, lakini

INAENDELEA UK. 26

## HABARI KITAIFA




Balozi wa Ufaransa nchini, Frederic Clavier, akizungumza wakati wa mkutano katika Siku ya Nishati ya Kifaransa, uliofanyika jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: HALIMA KAMBI**

# Korti kuamua uenyekiti wa Lipumba CUF leo

**Na Enock Charles**

SIKU chache baada ya Mahakama Kuu Kanda ya Dar es Salaam, kutengua Bodi ya Wadhamini ya Chama cha Wananchi (CUF) upande wa Prof. Ibrahim Lipumba, leo mahakama hiyo inatarajiwa kutoa uamuzi mwingine kuhusu hatima ya uenyekiti wake.

Prof. Lipumba ni Mwenyekiti wa CUF anayetambuliwa na Ofisi ya Msajili wa Vyama vya Siasa nchini.

Shauri hilo namba 23 la mwaka 2016, lililofunguliwa na chama hicho upande wa Katibu Mkuu, Maalim Seif Sharif Hamad, linatarajiwa kutolewa uamuzi leo mbele ya Jaji Benhajj Masoud wa Mahakama Kuu, baada ya awali kushindwa kusikilizwa na Jaji Wilfred Dyansobera aliyehamishiwa Mahakama Kuu Kanda ya Mtwara.

Profesa Lipumba alitangaza kujiuzulu uenyekiti wa chama hicho Agosti 2015, wakati wa kampeni za Uchaguzi Mkuu kwa madai kuwa haungi mkono makubaliano yaliyofikiwa na vyama vingine vinavyounda Umoja wa Katiba ya Wananchi (Ukawa).

Prof. Lipumba alichukua uamuzi huo baada ya vyama hivyo kumkaribisha Waziri Mkuu wa zamani, Edward Lowassa, kuwa mgombea wao wa urais.

Hata hivyo, mwaka mmoja baadaye Prof. Lipumba alimwandikia barua Katibu Mkuu, Maalim Seif, akiomba kurudi katika nafasi yake.

"Nimemwandikia Katibu Mkuu (Maalim Seif Sharif Hamad) kutengua barua yangu niliyoandika tarehe 5 Agosti, mwaka 2015. Sasa nasubiri majibu kutoka kwa

INAENDELEA UK. 7

# Waziri ashtushwa kasi ukuaji kilimo

**Na Mwandishi Wetu**

WAZIRI wa Kilimo, Japhet Hasunga, amesema ukuaji wa sekta ya kilimo nchini si wa kuridhisha japo inachangia karibu asilimia 30 ya pato la taifa.

Amesema hali hiyo inatokana changamoto zinazoikumba sekta hiyo hali ambayo imesababisha kukua kwa asilimia 7.7, kwa mujibu wa taarifa za hivi karibuni.

Kutokana na changamoto hizo, Hasunga alisema serikali ya awamu ya tano, chini ya Rais John Magufuli, imekuwa ikifanya jitihada mbalimbali katika kuweka mazingira bora ya kuleta mapinduzi katika kilimo.

Waziri Hasunga aliyasema hayo jana wakati akifungua mkutano wa siku mbili wa wadau wa asasi zinazotoa huduma ndogo za fedha vijijini kwa wajasiriamali wadogo (TAMFI), katika ukumbi wa mikutano wa Benki Kuu ya Tanzania (BoT), jijini Dar es Salaam.

Alisema kwa kutambua hilo, Wizara ya Kilimo kwa kushirikiana na wizara zinazojihusisha na sekta ya kilimo (ASLM) pamoja na wadau wengine, imetekeleza Programu ya Kuendeleza Sekta ya Kilimo Awamu ya Pili (ASDP II).

Lengo kuu la ASDP II ni kuleta mageuzi katika sekta ya kilimo (mazao, mifugo na uvuvi) ili kuongeza uzalishaji na tija, kufanya kilimo kiwe cha kibiashara na kuongeza pato la wakulima wadogo kwa ajili ya kuboresha maisha na usalama wa chakula na lishe.

Alisema utekelezaji wa lengo hilo ni kuhakikisha taifa linaendelea kujitosheleza kwa chakula; kuimarisha uchumi; kuwa kichocheo cha kukua kwa viwanda na kuongeza ajira.

Ili kufikia malengo hayo, alisema utekelezaji wa ASDP II utazingatia mnyororo wa thamani wa mazao ya kipaumbele ya kilimo, mifugo na uvuvi.

Alizitaja jitihada zingine katika kuleta mapinduzi ya kilimo kuwa ni kuanzishwa kwa eneo maalum la kuboresha mnyororo wa thamani kwa mazao mbalimbali (Sagcot), kuanzishwa kwa Programu ya Miundombinu ya Masoko, Uongezaji Thamani na Huduma za Kifedha Vijijini (MIVARF) ambayo lengo lake kuu ni kusaidia nyanja mbalimbali muhimu katika kuendeleza kilimo cha kisasa nchini na kuanzishwa kwa Benki ya Maendeleo ya Kilimo (TADB), ili kurahisisha upatikanaji wa mikopo nafuu kwa wakulima na shughuli za kilimo nchini.

Hasunga alisema jitihada za dhati zinahitajika kuwashawishi vijana kwa njia mbalimbali ili nao waingie katika biashara ya kilimo hasa katika uboreshaji wa mnyororo wa thamani kutokea shambani hadi kwa mlaji.

# Mwanafunzi kidato 4 ajiua kwa risasi

**Na Mwandishi Wetu**

MWANAFUNZI wa kidato cha nne katika Shule ya Sekondari Lupanga, amejiua kwa risasi mjini Morogoro huku akiacha ujumbe kuwa alikuwa anatamani kufa wakati wowote.

Kamanda wa Polisi Mkoa wa Morogoro, Wilbroad Mutafungwa, alisema jana kuwa Jasmin Ngoye (18) alikutwa amekufa Februari 19, mwaka huu, saa 12 asubuhi akiwa na jeraha kichwani.

Mutafungwa alisema mwili wa mwanafunzi huyo ulikutwa Kola B, Kata ya Bigwa katika Manispaa ya Morogoro.

Alisema hadi sasa uchunguzi wa tukio hilo umeonyesha kuwa chanzo ni msongo wa mawazo wa muda mrefu aliokuwa nao.

Kamanda Mutafungwa alisema kuwa polisi wamepata kitabu cha kumbukumbu (diary) cha Jasmin, aliyoiacha kwa rafiki yake, Imelda Milanzi.

"Ni mtoto asiyejua wazazi wake na asiyejua kazaliwa wapi? Mtoto

INAENDELEA UK. 7

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
WIZARA YA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO

Simu: +255 26 2324455
Fax: +255 26 2323233
Barua pepe: ps@mow.go.tz
Tovuti: www.mwtc.go.tz

Mtaa wa Moshi,
S.L.P 2888,
40470 DODOMA

TANGAZO

1. Ndugu wananchi mnatangaziwa kuwa siku ya **Ijumaa tarehe 22/02/2019** kampuni ya **Mainline Carriers Ltd** itasafirisha Mizigo yake yenye vipimo vikubwa kutoka Bandari ya **Mtwara** kuelekea **Mbeya,** magari hayo yana namba za usajili:

**T221BYM/T887DJB**
**T636DFA/T837DJB**
**T133CCP/T574BZB**
**T296CZS/T900BAZ**

2. Magari hayo yana vipimo vifuatavyo:
Urefu - mita 27.0
Upana - mita 5.50
Kimo - mita 6.40

3. Njia itakayotumika: **Mtwara hadi Mbeya** Kupitia **Makambako,**
Magari yatasafiri muda wa mchana tu **(Kuanzia saa 06:30 Asubuhi mpaka saa 12:00 Jioni)**

Tunaomba radhi kwa usumbufu utakaojitokeza.

215065902

Visit Visit Visit Visit

14TH EDITION
TANZANIA TRADE SHOW
INTERNATIONAL TRADE EXHIBITION

22 - 24 FEBRUARY 2019
DIAMOND JUBILEE HALLS
MALIK RD, UPANGA, DAR-ES-SALAAM
TANZANIA, 10.30 AM to 6.00 PM (DAILY)

Exhibitors Displaying Over 300
Products from various countries

MAJOR SECTORS

Agriculture - Automotive - Beauty & Cosmetics - Building & Construction - Consumer & Household - Food & Hotel Supplies Industrial & Machinery - IT & Electronics - Medical & Pharmaceutical Plastics & Rubber - Printing & Packaging - Safety & Security

SUPPORTED BY:

FIEO
Organized by Federation of Indian Export Organisations www.fieo.org

Incorporating
BUILDINT TANZANIA 2019

Tel : 0714 739 080 / 0787 473 520
Email: info@tanzaniatradeshow.com

115070302

# NEMC yakaribisha utafiti kabla ya kuchimba urani

**Na Mwandishi Wetu**

BARAZA la Taifa la Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira (NEMC), limekaribisha mradi wa utafiti wa kisomi kabla ya uchimbaji wa urani utakaohusisha Tanzania, Malawi, Namibia na Zambia.

Akifungua mkutano wa siku moja wa wasomi na wadau wengine wa mazingira jijini Dar es Salaam jana, Mkurugenzi Mtendaji wa NEMC, Dk. Samuel Gwamaka, alisifu mradi huu kwa maelezo kwamba utafanya utafiti mbalimbali wa kisomi ambao utatoa mwelekeo thabiti wa kutunza mazingira ya

Tanzania katika uchimbaji wa madini ya urani.

"Huu ni mradi mzuri kwa sababu utafiti wa kisomi utasaidia kutupa upeo wa kulinda mazingira ya nchi yetu na nchi tatu zilizomo katika mradi huu," Dk. Gwamaka alisema na kuielezea warsha hiyo kuwa ni muhimu na itaongeza uelewa miongoni mwa washiriki.

Dk. Gwamaka alisema kama wadau watakubaliana basi uchimbaji wa urani utakuwa na manufaa kwa nchi zote husika na hasa kwa kuwa madini hayo

INAENDELEA UK. 7



Waziri wa Nishati, Dk. Medard Kalemani (kushoto), akikagua mitambo ya kisasa ya kuchenjulia madini tani 10 kwa saa ambayo iko katika Kijiji cha Shenda, wilayani Mbogwe Mkoa wa Geita jana, na kuahidi kupeleka umeme hivi karibuni. **PICHA: WN**

# Waziri azuia maandamano wafugaji kumpongeza JPM

**Na Mwandishi Maalum,** SIMIYU

WAZIRI wa Mifugo na Uvuvi, Luhaga Mpina, amepiga marufuku makongamano ya wafugaji ya kumpongeza Rais John Magufuli kwa uamuzi aliochukua wa kuwasaidia, badala yake amewataka watumie kipindi hiki kifupi walichopewa na serikali kuainisha maeneo ambayo yamepoteza sifa za uhifadhi, ili yachukuliwe na serikali kwa ajili ya malisho ya mifugo.

Amewaagiza wafugaji kote nchini kujipanga na kupendekeza maeneo yaliyopoteza sifa za uhifadhi, mashamba yasiyoendelezwa ili wafugaji wapatiwe kwa ajili ya malisho ya mifugo yao kama sehemu ya kuunga mkono uamuzi uliotolewa wa kusaidia sekta hiyo.

Akizungumza katika mkutano wa kuwasikiliza wananchi waishio kando ya Hifadhi ya Pori la Akiba la Maswa wilayani Meatu, mkoani Simiyu, kwenye ziara ya Kamati ya mawaziri nane uliofanyika Mjini Mwandoya wilayani Meatu, Mpina alisema tangu mwaka 2000 tume zaidi ya 27 ziliundwa na Bunge na Serikali kushughulikia migogoro zaidi ya 1,095, lakini asilimia 99 ya mapendekezo ya tume hizo hayajatekelezwa hadi leo.

Mpina alisema tume nyingi zilizoundwa miaka ya nyuma kushughulikia migogoro hiyo zilichakachuliwa hata kabla ya kukabidhi matokeo ya mambo waliyobaini kwa kuwa kwenye migogoro hiyo, na kwamba wako baadhi ya viongozi wa serikali wako nyuma kwa kuwa na manufaa binafsi wanayopata ndio maana mapendekezo yaliyotolewa ya kutatua migogoro hiyo hayajawahi kutekelezwa hadi leo.

Alisema baadhi ya watendaji wa serikali walilazimika hata kutoa rushwa ili kubadilisha maamuzi ya tume zilizokuwa zinaundwa kushughulikia migogoro hiyo kwa sababu wananufaika na migogoro hiyo.

"Mheshimiwa Rais John Magufuli akasema

INAENDELEA UK. 7

# Utouh aeleza miaka minane ya u-CAG

**Na Augusta Njoji**, DODOMA

MDHIBITI na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG) mstaafu, Ludovick Utouh, amesema kwa miaka minane ambayo alitumikia nafasi hiyo amebaini kuna udhaifu wa kibinadamu ukiwamo mgongano wa maslahi unaosababisha mambo yasifanyike inavyotakiwa.

Utouh ambaye pia ni Mkurugenzi Mtendaji wa Taasisi ya Wajibu alitoa kauli hiyo jana, katika mafunzo ya siku mbili kwa Kamati ya Fedha na Utawala pamoja na Kamati ya Ukaguzi ya Jiji la Dodoma yaliyoandaliwa na taasisi hiyo kwa kushirikiana na Shirika la Maendeleo la Ujerumani (GIZ) kupitia mradi wa usimamizi bora wa fedha za umma.

Alisema nchi ina sheria na kanuni nzuri za uendeshaji wa shughuli zake, lakini wakati mwingine mambo hayafanyiki kama inavyotakiwa.

"Ukiangalia nchi ina sheria na kanuni nzuri, lakini unajiuliza kwanini mambo hayafanyiki kama inavyotakiwa, kwa nafasi yangu mimi kama Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kwa miaka minane nimekuja kugundua mara nyingi ni udhaifu wa kibinadamu unasababisha mambo yasifanyike kama inavyotakiwa.

"Wakati mwingine tunaweka ubinafsi mkubwa mno, hatuangalii mgongano wa maslahi na tunafanya vitu wakati mwingine tunajua si sahihi, lakini kwa sababu ya ubinafsi unakuta tunafungwa macho hayaoni madhara yatakayotokea kwa matendo yetu," alisema.

INAENDELEA UK. 7



TOLEO MAALUM

# USHIRIKIANO WA JICA KATIKA SEKTA YA USAFIRISHAJI DAR ES SALAAM

## SEHEMU YA KWANZA: UBORESHAJI WA USAFIRISHAJI ENEO LA TAZARA KWA KUJENGA DARAJA LA JUU LA KWANZA TANZANIA

DARAJA la Juu la kwanza nchini Tanzania lilizinduliwa mwezi Septemba 2018 na Rais wa Jamhuri ya Mwungano wa Tanzania Mheshimiwa Dk. John Pombe Magufuli mbele ya Balozi wa Japani nchini Tanzania Mheshimiwa Masaharu Yoshida. Daraja hilo la juu lilipewa jina la MFUGALE kwa heshima ya Bwana Patrick Mfugale, mhandisi mashuhuri Tanzania ambaye kwa sasa ni Mtendaji Mkuu wa Wakala wa Barabara Tanzania (TANROADS).

Daraja la Juu la Mfugale liko katika eneo la TAZARA, katika kona ya barabara za Nelson Mandela na Julius Nyerere jijini Dar es salaam, sehemu ambayo ina shughuli nyingi sana. Baada ya ufunguzi wa daraja hilo msongamano wa magari umepungua kwa kiasi kikubwa. Kwa mfano kabla ya ujenzi wa daraja hilo ilichukua muda wa saa moja kutoka katikati ya jiji hadi kufika Uwanja wa Ndege wa Kimataifa wa Julius Nyerere lakini kwa sasa inachukua muda wa nusu saa tu. Isitoshe mabasi ya usafiri wa umma sasa yanaweza kutumia daraja hilo hivyo wananchi wa Jiji la Dar es salaam sasa wanaweza kufurahia usafiri ulioboreshwa.

Ni kweli kwamba Daraja la Mfugale limechangia katika kupunguza msongamano wa magari. Hata hivyo limeleta manufaa mengine kama vile kuonyesha umuhimu wa ujenzi wa miundombinu bora na kwa kiwango cha hali ya juu, kumalizwa miradi kwa muda uliopangwa, kutokuwapo kwa ajali zozote wakati wa ujenzi na pia umuhimu wa kusambaza utaalam kwa wahusika.

Mkandarasi wa mradi huu yaani Sumitomo-Mitsui Construction Company (SMCC) ni mkandarasi mashuhuri kutoka Japani alifanikiwa katika mambo matatu kwa kushirikiana na wafanyakazi wa Kitanzania waliokuwa katika eneo la kazi. Eneo la kwanza la mafanikio ni kumaliza kazi bila ajali yeyote. Tangu mwanzo hadi mwisho wa ujenzi wa Daraja hilo jumla ya saa za kazi milioni 250 zilitumika bila ajali yeyote ile. Hii ni rekodi ya kupigiwa mfano kwani si tu kwa ukanda huu wa Afrika kutokea kwa jambo hilo bali hata nchini Japani si rahisi kufikia rekodi hiyo. Usalama katika eneo la kazi huchangia katika usalama wa wafanyakazi husika na pia katika kumaliza ujenzi husika kwa muda uliopangwa.



Daraja la Juu la Mfugale kama linavyoonekana wakati wa usiku

Eneo la pili la mafanikio ni eneo la kupeana ujuzi. Wafanyakazi Watanzania waliokuwa wanafanya kazi na Mkandarasi (SMCC) walipata ujuzi mbalimbali kutoka katika kampuni hiyo ya Kijapani. Walipata ujuzi na utaalam katika maeneo mbalimbali kama vile usimamizi bora wa miradi, usalama kazini n.k. ambao nao waliutumia katika sehemu zao mbalimbali za kazi.

Mradi wa Daraja la Juu la Mfugale si tu kwamba umechangia katika eneo lililopo mradi huo bali pia umechangia katika uendelezaji wa uwezo wa ujenzi katika Tanzania nzima. Kwa upande wetu JICA tunaweza kuthibitisha kwamba uendelezaji wa rasilmali watu ni sehemu ya ushirikiano wetu katika miradi yote ya JICA. Aidha miradi yetu ya miundombinu huchangia pakubwa katika kuendeleza rasilmali watu.

Ukipita katika Daraja la Juu la Mfugale wakati wa usiku utaona taa maalum ambazo zinakuongoza kuelekea katika daraja hilo. Taa hizi hutumia mwanga wa jua na hazihitaji matengenezo yeyote kwa muda wa miaka kumi. Taa hizi maalum hutengenezwa na kampuni ya Kijapani inayoitwa TSUJI PLASTICS Co. Ltd.

Taa hizi maalum zinatarajiwa kupunguza ajali za barabarani kwa kua zinatoa mwanga mkali katika eneo husika. Aidha taa hizi hung'arisha Tanzania ijayo. JICA hufanya kazi kama mwenza mwaminifu wa maendeleo ya Tanzania. Tunafanya kazi kwa pamoja na Serikali ya Tanzania na pia na Watanzania wote bega kwa bega.



Muonekano wa Makutano ya Tazara kabla ya Ujenzi wa Daraja la Juu la Mfugale

### Japan International Cooperation Agency (JICA)

**Ni Shirika la Umma la Serikali ya Japani linalosimamia misaada yote inayofadhiliwa na Serikali ya Japan (Official Development Assistance). JICA ni miongoni mwa mashirika makubwa sana duniani linalosaidia katika maendeleo ya kiuchumi na kijamii katika nchi mbalimbali zinazoendelea. Nchini Tanzania, JICA imekua mshiriki mwaminifu kwa Tanzania katika nyanja mbalimbali kwa zaidi ya miaka 50 kuanzia mwaka 1962. Katika uendelezaji wa miundombinu mijini ushirika wa JICA ulianza mwaka 1980 kwa kufadhili ujenzi wa Daraja la Selandar jijini Dar es salaam.**



Wakati wa ujenzi wa Daraja la Juu la Mfugale: Watanzania na Mkandarasi wa Kijapani wanafanya kazi kwa pamoja



Muonekano wa Daraja la Juu la Mfugale: Barabara 4 sasa zinatumika kwa umma

215073802

# MAONI & UCHAMBUZI

Nipashe
MWANGA WA JAMII

## Polisi waongeze nguvu utekaji, mauaji bodaboda

**KATIKA** toleo la leo tumechapisha habari kuhusu kuibuka kwa vitendo vya utekaji wa waendesha pikipiki za biashara kisha kuwaua katika baadhi ya maeneo ya Jiji la Dar es Salaam. Uporaji wa bodaboda katika jiji hilo umekuwapo kwa miaka mingi, kwa kufanywa na watu wasiojulikana, ambapo pia haijabainika pikipiki hizo wanakwenda kuziuza wapi.

Katika matukio haya mapya ambayo yameripotiwa kutendeka katika maeneo kadhaa ya Wilaya ya Ubungo yakiwamo Mbezi na Kimara, yanaogopesha kutokana na wahalifu hao kutumia silaha za moto kuwateka madereva, kuwapora bodaboda na kuwashambulia kwa risasi za moto.

Vijana kadhaa waliokumbwa na mkasa huo, lakini wakanusurika wamesimulia jinsi wahalifu hao wanavyotekeleza unyama huo, hivyo kuzua hofu kwao katika kujitafutia kipato. Kuna taarifa kutoka kwa vijana hao wanaojitafutia riziki katika vijiwe vyao maeneo ya Mpakani kwa Msuguri zinadai kuwa vijana wawili wanadaiwa kuuawa kwa risasi wiki iliyopita, wengine kujeruhiwa kisha kuporwa pikipiki.

Kwamba hali hiyo imezusha hofu kwa waendesha bodaboda kadhaa, ambao wameliomba Jeshi la Polisi kuwasaidia kuwanasa majambazi husika ili wafanye kazi hiyo katika hali ya usalama. Kuna mbinu nyingi ambazo wahalifu hao wanazitumia katika uporaji wa bodaboda kutoka kwa waendeshaji, ikiwamo kuwarubuni kwa kuwaelekeza wawafuate wateja, kumbe wanawaelekeza kwa majambazi wenye silaha za miti, ambao huwatishia kwa bastola kisha kuwapora. Waendesha bodaboda wameeleza mengi kuhusiana na jinsi walivyoathiriwa na vitendo hivyo na kueleza kuwa hali hiyo imezua hofu kubwa kwao.

Kimsingi, matukio ya wizi na uporaji wa bodaboda jijini Dar es Salaam siyo jambo jipya, isipokuwa linakuwa jambo jipya na tishio kutokana na matumizi ya silaha za moto katika uporaji huo. Kutokana na hali hiyo, tunaona kuwa Jeshi la Polisi linawajibika kujiongeza nguvu katika kukabiliana na vitendo hivyo, ambavyo havitawaathiri wenye bodaboda, bali jamii nzima kwa kutilia maanani kuwa bodaboda sasa ni ajira ya uhakika kwa vijana wengi nchini.

Vijana wengi vijijini na mijini wanaishi kwa kutegemea ajira ya bodaboda katika kujipatia mahitaji yao ya msingi ya maisha, na kusema ukweli wengi wanaojitambua kazi hiyo imewatoa.

Bado tunaona kuwa ulinzi wa raia na mali zao si jukumu la Jeshi la Polisi tu, bali hata raia wenyewe kwa kupitia njia mbalimbali, yakiwamo matumizi ya vikundi vya ulinzi shirikishi. Hata hivyo inapofika mahali wahalifu wakatumia teknolojia ya kisasa yakiwamo matumizi ya silaha za moto kupora vitu kama bodaboda, jeshi hilo linapaswa kuchukua hatua maalum na za makusudi kukabiliana nao.

Kwa kuwa jeshi hilo limethibitisha kupata taarifa za matukio ya Mpakani kwa Msuguri na mengine yote yaliyoripotiwa, bila shaka litayafanyia kazi kama alivyoeleza Kamanda wa Mkoa wa Polisi Kinondoni, Mussa Taibu, ili kuwabaini wahusika. Kuwasaka na kuwakamata kisha kuwafikisha katika vyombo vya sheria, tunaamini kuwa kutasaidia kuusambaratisha mtandao wote wa wahalifu, hivyo kuwawezesha vijana wetu kuendelea kujitafutia kipato kwa njia halali ya bodaboda.

Aidha, tunawahimiza vijana hao kufanyia kazi ushauri wa kamanda huyo wa kuwataka kuwa makini na abiria wanaowabeba hasa usiku, ikiwezekana wawapige picha ndipo wawapeleke, anayekataa atakuwa na lake baya. Pia wasikubali kwenda kwenye maeneo ambayo yana mazingira yasiyoeleweka.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
**THE GUARDIAN LIMITED**

**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Meneja Matangazo:** Kauthar D'souza, 0767 223311.
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
epaper.ippmedia.com




# Muungwana Lazima Nilonge



## Umakini barabarani ni wajibu wa abiria, chombo cha moto

Na Mary Geofrey

**LICHA** ya serikali kujitahidi kuboresha miundombinu barabarani, zipo changamoto zinazochangiwa na watumiaji wa miundombinu, ambao kwa kiasi kikubwa inachangiwa na uzembe wa watumiaji kutotii sheria, alama na michoro ya barabarani.

Kutokana na changamoto hizo, ajali za barabarani mzizi wake mkuu ni uzembe wa abiria na watumia barabara, wanachangia ajali zinazoishia katika kuzaa ulemavu na vifo kwa watumiaji.

Mbali na watu kupoteza maisha, pia mali kama magari huharibiwa vibaya na kusababisha hasara kwa mmiliki.

Pia, taifa linapoteza nguvu kazi na wengine wamebakia walemavu wa kudumu, kiasi cha kushindwa kujitafutia kipato cha kila siku na kuwa mzigo kwa familia zao au wategemezi wanaoiacha familia anayoipenda, iishi katika maisha yasiyo na dira.

Hiyo ni upande mmoja. Kuna madereva wa magari wa kupongezwa, wanaojitahidi kuzingatia sheria, alama na michoro ya barabarani.

Orodha inaenda mbali. Pia yapo matatizo yanayosababishwa na kuchangiwa na baadhi ya wananchi wanaoishi pembezoni mwa barabara kung'oa alama za barabarani, zinazomwelekeza dereva wa chombo cha moto na mpitanjia, tahadhari na maamuzi ya kufanya aliko na anakoenda barabarani.

Kutokana na dereva kutofuata alama za barabarani, matokeo yake ni ajali inayogharimu maisha na mali. Hizo ni changamoto ambazo polisi kupitia Kikosi cha Usalama Barabarani, imekuwa ikitoa elimu ya hatua za kifuata.

Polisi imekuwa ikiandaa programu mbalimbali za elimu na kufanya uelimishaji mbalimbali, ikiwamo kwa njia ya televisheni, redio, mitandao ya kijamii na usambazaji vipeperushi, huku ikiwakusanya makundi ya watu katika sehemu tofauti, waweze kujua na kujifunza matumizi sahihi ya barabara.

> **Hiyo ni upande mmoja. Kuna madereva wa magari wa kupongezwa, wanaojitahidi kuzingatia sheria, alama na michoro ya barabarani.**

Ni hatua ambayo nchini imekuwa na changamoto za watu kutozingatia sheria za usalama barabarani na wamekuwa wakitembea mwendo unaozidi kiwango na matokeo yake, hata kusababisha ajali na uharibifu wa mali za watu.

Pia, watumiaji wa vyombo vidogo kama pikipiki, baiskeli na mikokoteni, wanakatiza katikati ya barabara, bila hata ya kuangalia usalama wa watembeaji kwa miguu.

Ukatishaji katikati ya barabara bila ya tahadhari, matokeo yake ni ajali zisizotarajiwa.

Unakuta mwendesha baiskeli au mkokoteni anakatiza katikati ya barabara kwa kujiamini na mwendo taratibu, ilhali anaona magari yakiwa yanakuja.

Kwa ustaarabu, watumiaji wa barabara tunapaswa kutambua kila mtu ana haki ya kutumia barabara, lakini kwa tahadhari na wapo wapita njia hasa wakazi wa mijini wanaojiamini wanapokatisha njiani, wanajiamini dereva anaweza kuona.

Kitu ambacho watu hawakifahamu au wanakichukulia 'poa' ni kuamini kila dereva ana uwezo wa kumuona mtembea kwa miguu, jambo linalowafanya kugongwa, kwa sababu wanaona magari yakiwakaribia, bado dereva wanawaona.

Ni muhimu sheria za usalama barabarani kwa watembea kwa miguu, wahakikishe wanasimama kwenye alama za pundamilia kwa ajili ya kusimamisha magari wavuke.

Pia, siku za karibuni kumekuwapo na tabia ya watembea kwa miguu kuvuka maeneo ambako askari wa usalama barabarani wanaruhusu magari.

Ni muhimu watembea kwa miguu wakaheshimu kazi wanazofanya askari wa usalama barabarani, kama anaita magari ya upande mmoja watu wanapaswa kusubiri hadi atakaposimamisha na kuruhusu watu wavuke.

Tuache tabia ya kujifanya wajanja wakati wa kuvuka barabara, jambo linaloweza kuhatarisha maisha ya watu kwa sababu za uzembe ambao unaweza kuzuilika.

## Utouh aeleza miaka minane ya u-CAG

INATOKA UK. 4

Hata hivyo, hakufafanua kwa kina kwenye maelezo yake kuhusu mgongano huo wa maslahi.

Aidha, Utouh alisema Rais John Magufuli, alipokuwa akizungumzia kikokotoo cha mafao, alisema mifuko iangalie matumizi yake ni jambo muhimu sana.

"Wakati mwingine tunapofikiria kuongeza mapato ukiangalia matumizi yako vizuri ukaenda kwenye matumizi ya muhimu unaongeza matumizi na wakati mwingine hatulioni hilo," alisema.

Akizungumzia Jiji la Dodoma, Utouh alisema wanajitahidi kutafakari nini kifanyike kulifanya jiji hilo ambalo limeng'ara kwa kuwa la kwanza kimapato liendelee kushika namba moja.

"Pamoja na hongera mnazopewa, lakini mna kihatarishi kitu kimoja kigumu sana cha kuhimili hiyo namba moja, kwa sababu wenzenu huko waliko wanawaza wafanye nini kulipiku Jiji la Dodoma, msibweteke wala kulala msifanye kazi kwa mazoea," alisema.

Alisema katika mafunzo hayo mada nane zitatolewa ikiwamo changamoto za upatikanaji wa mapato katika halmashauri, ubunifu wa kamati hizo katika usimamizi wa rasilimali za jiji, mifano ya usimamizi na ukusanyaji endelevu wa mapato na matumizi ya rasilimali katika majiji.

Pia alisema itatolewa mada ya umuhimu wa ukaguzi wa ndani katika kuimarisha matumizi bora ya rasilimali za jiji, hoja za ukaguzi zinazohusu usimamizi na ukusanyaji wa mapato kwa mwaka 2016/17, uwekezaji katika hatifungani na matumizi ya miradi ya ubia kama fursa ya kuongezea mapato.

"Mada zingine ni uzingatiaji wa sheria ya manunuzi ya umma katika kuongeza thamani ya fedha za jiji na vihatarishi vya jiji katika usimamizi wa rasilimali zake," alisema.

Akifungua mafunzo hayo, Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais -Tamisemi, Selemani Jafo, alisema kutolewa kwa mafunzo hayo ni majibu ya maombi yake aliyoyatoa kwa taasisi hiyo kutokana na kubaini kuwa halmashauri zinachangamoto kwenye usimamizi wa rasilimali za umma.

Naye, Mwakilishi wa GIZ, Dk. Annette Mummert, alisema shirika hilo litaendelea kushirikiana na Taasisi ya Wajibu ili kufanikisha masuala ya usimamizi wa rasilimali za umma nchini.

Alisema wanatarajia kuona mamlaka za serikali za mitaa zinafanya vizuri kwenye masuala ya fedha kupitia mafunzo hayo.

## NEMC yakaribisha utafiti kabla ya kuchimba urani

INATOKA UK. 4

yanatoa mchango mkubwa katika kuzalisha umeme.

Warsha ya aina hiyo inafanyika pia Malawi, Namibia na Zambia kwa ufadhili wa Jumuiya ya Umoja wa Ulaya (EU) kwa lengo la kuwa na uchimbaji, uchakataji, usafirishaji na matumizi salama ya urani.

Wajumbe walitoka Chuo Kikuu cha Dodoma, Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, Wizara ya Madini na NEMC, taasisi mbalimbali za umma na binafsi zinazojishughulisha na madini pamoja na mazingira nchini. Chuo Kikuu cha Dodoma ndicho kinachotaratibu na kukusanya taarifa zitakazotoa majibu iwapo ni busara na ni namna gani urani ichimbwe Tanzania au vinginevyo.

Washiriki katika warsha hiyo walijadili changamoto zinazojitokeza katika uchimbaji wa madini, hasa urani kwa sababu ni madini yenye madhara makubwa kwa viumbe na mazingira na hasa kama uchimbaji unafanywa kabla ya utafiti wa kutosha.

Mkuu wa Kitivo cha Sayansi Mazingira na Teknolojia wa Chuo Kikuu cha Dodoma, Dk. Meserecordias Lema, alisema washirika walipata nafasi ya kujadili namna bora ya kuboresha sheria ili ziendane na sheria za nchi husika.

"Warsha hii ililenga kutafuta njia bora ya kufanyia maboresho ya sheria katika uchimbaji wa urani kusudi mataifa yote manne yawe na mfumo wa sheria moja, ili kuondokana na madhara ya urani katika nyanja mbalimbali," alisisitiza Dk. Lema.

Alisema wajumbe walijikita katika ulinzi na usalama kwenye uchimbaji, uchakataji na usafirishaji na matumizi salama ya urani.

## Korti kuamua uenyekiti wa Lipumba

INATOKA UK. 3

Katibu Mkuu baada ya barua yangu kujadiliwa na ngazi husika za chama," alisema Lipumba kwenye barua yake ya wakati huo.

Ombi hilo la Prof. Lipumba lilikataliwa na baadhi ya wanachama wa chama hicho hasa wanaomuunga mkono Maalim Seif, hivyo kusababisha mgawanyiko kati ya wanachama wanaomuunga mkono profesa huyo wa uchumi na wale wanaomuunga mkono Maalim Seif.

Hata hivyo, Msajili wa Vyama vya Siasa, Jaji Francis Mutungi, alitangaza kumtambua Prof. Lipumba kama mwenyekiti halali wa (CUF), jambo lililopingwa vikali na baadhi ya wanachama wa chama hicho wakiongozwa na Katibu Mkuu.

Mtafaruku huo ndio uliosababisha kufunguliwa kwa kesi ya kikatiba na kambi ya Maalim Seif kupinga uenyekiti wa Prof. Lipumba.

Tangu kurejea kwake kama mwenyekiti wa chama hicho, kumekuwa na mgawanyiko na mivutano baina ya viongozi na wanachama wa chama hicho.

Hali hiyo ilisababisha hata baadhi ya wabunge wa chama hicho kujiuzulu na wengine kutenguliwa ubunge wao baada ya mwenyekiti huyo kuteua wabunge wapya wa kambi yake.

## Mwanafunzi kidato cha 4 ajiua kwa risasi

INATOKA UK. 3

huyu anatamani kukiona kifo chake wakati wowote na muda wowote. Mtu yeyote atakayeisoma hii 'diary' ndiye atakayeiandika tarehe ya kifo changu," ulisomeka ujumbe wa Jasmin kwenye 'diary' hiyo.

Kamanda Mutafungwa alisema, mwili wa Jasmini ulikuwa na jeraha la risasi iliyoingia kooni na kutokea utosini na pia pembeni kulikuwa na bastola aina ya Berreta yenye namba H.11135Y, magazine moja, risasi moja na ganda la risasi lililotumika.

Alisema mmoja wa waliohojiwa kuhusiana na kifo hicho, Profesa Hamis Mahigi (69) aliwaeleza Polisi kuwa bastola hiyo ni yake, anamiliki kihalali na anamtambua Jasmin kuwa ni shemeji yake na alikuwa akiishi naye Kihonda, Morogoro.

Mutafungwa alisema, Profesa Mahigi amewaeleza polisi kuwa Jasmin alikuwa mwanafunzi wa kidato cha nne katika Shule ya Sekondari Lupanga na alitoweka nyumbani Februari 18, saa 10 jioni.

## Waziri azuia maandamano wafugaji kumpongeza JPM

INATOKA UK. 4

hapana nitaunda tume ambayo haitapokea rushwa, timu ya Lukuvi mnaiona ina sura ya kupokea rushwa. Vichwa vya kina Mpina unaweza ukawapa nini wakakubali?" Alihoji na kuendelea:

"Akasema wananchi wangu watahangaika mpaka lini, watauana mpaka lini, mifugo mingi imedhulumiwa kwa kivuli cha uhifadhi, akasema nitaunda tume ndio hii sasa ya mawaziri 8."

Mpina aliwahakikishia wananchi kuwa mapendekezo yaliyotolewa na wananchi yatafika kwa Rais tofauti na tume zingine zilizotangulia zilikuwa hazina uwazi wa namna ya kuchukua maoni na namna ya kufikisha mapendekezo serikalini.

Aliwaagiza wafugaji wote nchini kupoteza muda kwa kufanya makongamano na maandamano ya kumpongeza Rais kwa sasa kwa kuwa Rais amewapa kazi wakulima, wafugaji, wavuvi kuangalia maeneo ambayo yamepoteza sifa yaweze kupendekezwa ili wafugaji wayapate.

"Najua furaha yenu kwa uamuzi huu, lakini kwa sasa sisi kama wafugaji tusipoteze muda wa makongamano na kumshangilia Meshimiwa Rais wakati ametupa kazi kubwa ya kupendekeza maeneo hayo ili mwisho tuyapate, yafutwe tuweze kufanya shughuli kilimo, ufugaji," alisema.

Aidha, alikataa kuhudhuria makongamano ya vyama vya wafugaji ambao walimwalika kuhudhuria sherehe hizo na kuwataka kujipanga vizuri kupendekeza ili kuitumia vizuri nafasi ya pekee waliyopewa na Rais Magufuli.


## KUMBUKUMBU

**BALOZI FULGENCE MICHAEL KAZAURA**

**Kuzaliwa: 11/09/1940 - Kufariki: 22/02/2014**



Ilikuwa tarehe **22 Februari, 2014** ulipotutoka, ikawa dakika, masaa, siku na hatimaye leo umetimiza miaka mitano (5) toka Baba yetu wa mbinguni akutwae kwenda kwenye makao yako ya milele. Ni vigumu kwetu kukubali kwamba haupo nasi kimwili, lakini tunafarijika kwa imani kwamba uko nasi kiroho na unaendelea kutuombea.

Ingawa ulitutoka ghafla bila neno lolote kwetu, matendo yako yatabakia daima ndani mwetu na amani na upendo uliotuachia vitaendelea kuwa mwongozo kwetu. Japo haupo nasi kimwili lakini kiroho bado tupo nawe. Baba, tulikupenda sana na tutaendelea kukupenda daima.

Unakumbukwa sana na mke wako mpendwa Bibi Coelestina Kazaura watoto wako Kokuhumbya, Kamugisha, Rweyunga, Kemilembe, Sima, Kokutulage, Mwijage na Mwesigwa. Wakwe zako, wajukuu, ndugu, jamaa na marafiki.

Familia ya Marehemu Balozi Fulgence Michael Kazaura inawaalika kwenye misa ya kumbukumbu ya miaka mitano (5) tangu kifo chake itakayofanyika siku ya Jumamosi tarehe 23rd Februari, 2019 saa 4.00 asubuhi nyumbani Oysterbay mkabala na shule ya Genesis.

**Mnakaribishwa sana,**

**BWANA ALITOA NA BWANA AMETWAA**
**JINA LA BWANA LIHIMIDIWE, AMINA.**

xxxxxxxx

# STANBIC BANK TANZANIA

## Tariff Guide Uhuru Banking

**Effective as of 1st March 2019**

| TRANSACTION/SERVICE | | | FOREIGN CURRENCY CURRENT ACCOUNT | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|
| **MONTHLY MANAGEMENT FEES** | **DESCRIPTION** | **TZS** | **USD** | **EURO** | **GBP** | **ZAR** |
| Personal Current Account | Monthly Management Fee | FREE | FREE | FREE | FREE | FREE |
| Hatua Account | Monthly Management Fee | FREE | FREE | FREE | FREE | FREE |
| **TRANSACTION SERVICES** | | | | | | |
| Cash Withdrawal @ Branch Counter (Either With Cheque, Deposit Slip Etc.) | Fee could be a % charge on withdrawal (with min charge per withdrawal) or lat charge per transaction. | 3,894 for amounts below 20M, 0.15 % of value max 118,000 for amount above 20M | For FCY withdrawals 1.18 % min 7.08, Maximum 300 | For FCY withdrawals 1.18% min 14.16, Maximum 300 | For FCY withdrawals 1.18% min 14.16, Maximum 300 | For FCY withdrawals 1.18% min 14.16, Maximum 300 |
| Cash Deposit Charge | 1.77% of FCY currency below 50 note. Otherwise FREE. | FREE | 1.77% of FCY currency below 50 note. Otherwise FREE. For all FCY currency. | 1.77% of FCY currency below 50 note. Otherwise FREE. For all FCY currency. | 1.77% of FCY currency below 50 note. Otherwise FREE. For all FCY currency. | 1.77% of FCY currency below 50 note. Otherwise FREE. For all FCY currency. |
| Cheque Deposit | | FREE | FREE | FREE | FREE | FREE |
| Account Closure | Charge for closing account | FREE | FREE | FREE | FREE | FREE |
| Cheque Book | Per leaf | 413 | 0.36 | 0.24 | 0.24 | 3.54 |
| **CARDS AND ATM FEES** | | **TZS** | **USD** | **EURO** | **GBP** | **ZAR** |
| Card expired | | FREE | FREE | FREE | FREE | FREE |
| Card New | | FREE | FREE | FREE | FREE | FREE |
| Card Not working | | FREE | FREE | FREE | FREE | FREE |
| Card compromised | | FREE | FREE | FREE | FREE | FREE |
| POS Purchase ( Domestic) | | FREE | FREE | FREE | FREE | FREE |
| Annual card fees | | 10,000 | 10.00 | 10.00 | 10.00 | 112.00 |
| Secondary Card fee | | 25,000 | 15.00 | 12.00 | 9.00 | 139.00 |
| Card Damaged | | 25,000 | 15.00 | 12.00 | 9.00 | 139.00 |
| Card lost/Stolen | | 25,000 | 15.00 | 12.00 | 9.00 | 139.00 |
| Card Name Change | | 25,000 | 15.00 | 12.00 | 9.00 | 139.00 |
| Cash withdrawal @ other bank ATM (in another country) | | 8,000 | 5.00 | 4.00 | 3.00 | 44.00 |
| International card access fee | | 8,000 | Tzs equivalent | Tzs equivalent | Tzs equivalent | Tzs equivalent |
| Uncollected cheque/CARDS fees ( Two month) | | 10,000 | 4.00 | 4.00 | 1.90 | 28.00 |
| POS Purchase ( International) | | FREE | FREE | FREE | FREE | FREE |
| Declined ATM cash withdrawal no funds - Stanbic/Standard Bank ATM (internationally) | | 2,500 | 1.50 | 1.20 | 0.90 | 14.00 |
| Cash withdrawal @ other bank ATM (in country) | | 1,000 - 400,000 = 2800<br>400,001-above=4000 | 1,000 - 400,000 = 2.8<br>400,001-above=4 | 1,000 - 400,000 = 2.8<br>400,001-above=4 | 1,000 - 400,000 = 2.8<br>400,001-above=4 | 1,000 - 400,000 = 28<br>400,001-above=40 |
| Declined ATM cash withdrawal no funds - other bank's ATM (in country) | | 1,000 | 0.60 | 0.50 | 0.40 | 6.00 |
| Balance enquiry on other Banks ATM/ CCC and at Branch | | 1,000 | 0.60 | 0.50 | 0.40 | 6.00 |
| Cash withdrawal @ own ATM (in country) | | 950 | 0.60 | 0.40 | 0.40 | 5.00 |
| Mini stat at own ATM | | 900 | 0.60 | 0.40 | 0.40 | 5.00 |
| Declined ATM cash withdrawal no funds (own ATM) | | 700 | 0.40 | 0.34 | 0.30 | 4.00 |
| Pin management | | 700 | 0.40 | 0.34 | 0.30 | 4.00 |
| Balance enquiry own ATM | | 300 | 0.20 | 0.14 | 0.11 | 1.70 |
| **USSD/WAP AND INTERNET BANKING** | | | | | | |
| Fee- Top-up Other | | FREE | FREE | FREE | FREE | FREE |
| Fee- Top-up Self | | FREE | FREE | FREE | FREE | FREE |
| Fee- Self Funds | | FREE | FREE | FREE | FREE | FREE |
| Biller Payment | | FREE | FREE | FREE | FREE | FREE |
| Fee-Monthly Subscription | | FREE | FREE | FREE | FREE | FREE |
| Bank To Wallet | | 1,000 - 25,000 =1500<br>25,001 - 100,000 = 2000<br>100,001 - 250,000 = 2500<br>250,001-500,000=3000<br>500,000-1,000,000=3,500 | Tzs equavalent | Tzs equavalent | Tzs equavalent | Tzs equavalent |
| Transfers Of Money Outside Stanbic(Express) | | 8,000 | Tzs equavalent | Tzs equavalent | Tzs equavalent | Tzs equavalent |
| Transfers Of Money Outside Stanbic(Normal) | | 2,000 | 1.20 | 0.90 | 0.80 | 12.00 |
| Transfers Of Money 3rd party Within Stanbic | | 1,000 | 0.60 | 0.50 | 0.40 | 6.00 |
| Mini statement | | 500 | 0.30 | 0.30 | 0.30 | 3.00 |
| Balance Inquiry( wap and ussd charged) | | 350 | 0.20 | 0.14 | 0.11 | 1.70 |
| **OTHER FEES** | | | | | | |
| Statement (Monthly) OTC | | 1,000 | 1.00 | 1.00 | 1.00 | 12.00 |
| E statement | | FREE | FREE | FREE | FREE | FREE |
| Interim Statement (Over The Counter)( More Than One Month But Not Exceed 3 Month) | | 4,720 | 2.90 | 2.00 | 1.80 | 26.00 |
| Certiicate Of Balance | | 41,300 | 24.78 | 20.06 | 15.34 | 228.92 |
| Letter Of Introduction | | 47,200 | 28.32 | 22.42 | 17.70 | 261.96 |
| Certiicate Covering Interest Paid | | 47,200 | 28.32 | 22.42 | 17.70 | 261.96 |
| Certiicate Of Account Balance Only | | 41,300 | 24.78 | 20.06 | 15.34 | 228.92 |
| Confirmation Auditor List | | 129,800 | 79.06 | 61.36 | 48.38 | 720.98 |
| Search Fees For Copies | | 60,000 | 32.00 | 25.00 | 21.00 | 300.00 |
| Fee- OTC History Statements | | 60,000 | 32.00 | 25.00 | 21.00 | 300.00 |
| **PAYMENTS** | | | | | | |
| Unpaid Cheque(Insuficient Fund) | Flat fee per unpaid item | 100,000 | 100.00 | 100.00 | 100.00 | 560.00 |
| Overdraft Establishment Fee | Cost of establishing an overdraft. - once off charge | 1.5% of the facility min 100 000. | 1.5% of the facility min 100 | 1.5% of the facility min 100 | 1.5% of the facility min 100 | 1.5% of the facility min 1500 |
| Unarranged Overdraft | Unauthorised overdraft fee - lat fee charged for overdraft excesses | 100,000 | 60.00 | 50.00 | 40.00 | 560.00 |
| Overdraft Renewal Fee | Fees for renewal of overdraft facility | 1.5% of the facility min 100 000. | 1.5% of the facility min 100 | 1.5% of the facility min 100 | 1.5% of the facility min 100 | 1.5% of the facility min 1500 |
| Salary for SFI | per person | 4,000 | 2.00 | 2.00 | 2.00 | 23.00 |
| Salary for EFT | per person | 4,000 | 2.00 | 2.00 | 2.00 | 23.00 |
| Salary for TISS | per message | 10,000 | Tzs equavalent | Tzs equavalent | Tzs equavalent | Tzs equavalent |
| Salary for Manual | per person | 5,000 | 2.40 | 1.90 | 1.50 | 23.00 |
| Fee- Standing Instruction | SI ESTABLISHMENT | 7,080 | 4.72 | 3.54 | 2.36 | 38.94 |
| Fee-Standing Order Amendment | SI AMMENDMENT | 6,490 | 3.54 | 3.54 | 2.36 | 36.58 |
| Basic Fee-Standing Instruction | SI THIRD PART ACCOUNT | 4,720 | 2.36 | 2.36 | 1.18 | 25.96 |
| Basic Fee-Standing Instruction | SI -OTHER BANK ACCOUNT | 33,040 | 17.70 | 12.98 | 11.80 | 147.50 |
| Basic Fee-Standing Instruction | SI-OWN ACCOUNT | FREE | FREE | FREE | FREE | FREE |
| Basic Fee-Standing Instruction | SI-UNPAID STANDING ORDER (FAILURE) | 66,080 | 40.12 | 31.86 | 24.78 | 366.98 |
| Stop Payment Orders | | 47,200 | 28.32 | 22.42 | 17.70 | 261.96 |
| Fee-Inter Account Transfer(3Rd Party) OTC | | 4,720 | 2.90 | 2.00 | 1.80 | 26.00 |
| Fee-Inter Account Transfer(Other Bank) | | 10,000 | Tzs equavalent | Tzs equavalent | Tzs equavalent | Tzs equavalent |
| Bank Cheque Issued# | | 40,120 | 24.78 | 18.88 | 15.34 | 223.02 |

215074002

## HABARI KITAIFA

# Waliokwamisha ajira za watumishi sita matatani

**Na Mwandishi Wetu**

NAIBU Waziri, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, Mary Mwanjelwa, amemwagiza Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Kilindi mkoani Tanga, Gracian Makota, kufanya uchunguzi na kuwasilisha taarifa ya watumishi wote waliohusika kutowaingiza kwenye Mfumo Shirikishi wa Taarifa za Kiutumishi na Mishahara watumishi sita.

Watumishi hao ni waliopewa kibali cha ajira na Katibu Mkuu, Ofisi ya Rais (Menejimenti ya Utumishi wa Umma) mwaka 2011 na badala yake kibali hicho kutumika kuajiri watumishi wengine.

Agizo hilo alilitolea wilayani Kilindi wakati wa kikao kazi na watumishi wa halmashauri hiyo, kufuatia malalamiko yaliyowasilishwa na Mbunge wa Kilindi, Omary Kigua, kuhusu watumishi hao sita walionyimwa haki yao ya kuajiriwa tangu mwaka 2011, kilipotolewa kibali cha ajira na Ofisi ya Rais (Menejimenti ya Utumishi wa Umma).

Awali, watumishi hao walikuwa wakilipwa mshahara kutokana na vyanzo vya ndani vya mapato vya halmashauri hiyo.

Mwanjelwa alisema, hatua kali za kinidhamu zitachukuliwa kwa wale wote waliohusika kukaidi kibali halali kilichotolewa na ofisi yake kwa kuajiri watumishi wengine kinyume cha taratibu, na kuongeza kuwa watumishi waliofanya kitendo hicho hawakuwa waaminifu katika kutekeleza majukumu yao.

Mwanjelwa alifafanua kuwa ameshamwagiza Mkurugenzi wa Idara ya Usimamizi wa Rasilimaliwatu serikalini wa ofisi yake ambaye anasimamia Mfumo Shirikishi wa Taarifa za Kiutumishi na Mishahara afanye uchunguzi mara moja na kumpatia maelezo ya kina, ili afanye ulinganifu na taarifa atakayoiwasilisha Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Kilindi kwa ajili ya kuchukua hatua stahiki.

Aidha, Mwanjelwa alimtaka Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Kilindi kufanya utaratibu wa kuwaombea ajira ya mkataba kwa Katibu Mkuu, Ofisi ya Rais (Menejimenti ya Utumishi wa Umma) watumishi hao sita walioonewa, kwa kuwa umri wa kupata ajira ya kudumu serikalini umeshapita kwa kuwa wana zaidi ya miaka 45.

# Shule kongwe yaweka mkakati wa ufaulu

**Na Hamisi Nasiri,** MASASI

SHULE ya sekondari ya wavulana wa kidato cha tano na sita Ndanda wilayani Masasi, mkoani Mtwara, imetangaza rasmi kuwa na mkakati kabambe wa kuondoa kabisa ufaulu wa daraja la tatu, la nne na sifuri na kubaki na daraja la kwanza pekee, lengo ni kuendelea kuipa hadhi na sifa bora kitaaluma.

Shule hiyo ambayo ilianzishwa mwaka 1928 na baadhi ya viongozi mbalimbali wa kitaifa nchini waliowahi kusoma akiwamo Rais mstaafu, Benjamin Mkapa, mkakati wake huo ni wa kuanzia mwaka 2019.

Hayo yalisemwa wilayani Masasi na Mwalimu Mkuu wa shule hiyo, Morega Mongate, na kwamba sifa ya kitaaluma kwenye shule hiyo bado ni ya kuridhisha ngazi ya wilaya, mkoa na taifa kwa ujumla.

Hata hivyo, alisema katika miaka ya karibuni zilianza kujitokeza baadhi ya changamoto, na kuwapo mwelekeo wa kufanya vibaya wameamua kuanza kutekeleza mkakati huo ili kulinda hadhi yake ya ufaulu mzuri.

"Kutokana na kuingiwa na wasiwasi uongozi wa shule kwa kushirikiana na bodi ya shule kwa 2019 na kuendelea tumejiwekea mkakati wa kuondoa kabisa alama ya ufaulu wa daraja la tatu, la nne na sifuri kwa matokeo ya wanafunzi wanaomaliza kidato cha sita kuanzia mwaka huu na kuendelea," alisema Mongate.


| | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|
| **INTERNATIONAL BUSINESS CENTRE** | | | | | | |
| **INWARD PAYMENT** | | | | | | |
| Telegraphic Transfer/SWIFT | | 0.25% Min $11 Max $35 | 0.25% Min $11 Max $35 | | | |
| Drafts/Bills (Clean Bill Collection) | | $150 | $150 | | | |
| Bills and drafts negotiated and subsequently returned unpaid | | $150 | $150 | | | |
| **OUTWARD PAYMENTS** | | | | | | |
| SWIFT Charges for tracing remittances | | $50 | $50 | | | |
| Telegraphic Transfer/SWIFT | Oversee charge is charged depending on made of payment customer has choose. | 0.295% of Value Min $50, Max 150 (excluding oversee charge of $29.5) | 0.295% of Value Min $50, Max 150 (excluding oversee charge of $29.5) | | | |
| Telegraphic Transfer/SWIFT( For TT done from TZS accounts) | This price is inclusive of all charges | $59 flat | $59 flat | | | |
| Cancellation of TT/Recall of funds | | $75 | $75 | | | |
| Amendment TT | | $75 | $75 | | | |
| Transfers though TISS | | TZS10 000 | Equiv 10 000 | | | |
| Drafts/Bills/Cheques | | 1.18% of the amount min 100 000, Max 400 000 | 1.18% of the amount min $59, Max $236 | 1.18% of the amount min 50, Max $200 | 1.18% of the amount min 40, Max 160 | 1.18% of the amount min 560, Max 2240 |
| **LETTER OF CREDIT** | | | | | | |
| **OUTWARD** | | | | | | |
| Establishment fee | | 1% on establishment per quarter and part thereoff min 300 plus SWIFT $35 | 1% on establishment per quarter and part thereoff min 300 plus SWIFT $35 | | | |
| Amendmen of LC terms and condition only /Cancelation | | US$150 | US$150 | | | |
| Extensions for increases of amounts | | 1% on establishment per quarter and part thereoff min 300 plus SWIFT $35 | 1% on establishment per quarter and part thereoff min 300 plus SWIFT $35 | | | |
| Discrepance Fee | | $100 | $100 | | | |
| **Documentary fee** | | | | | | |
| Handling commission | | US$ 120 | US$ 120 | | | |
| Payment commission | | US$ 55 | US$ 120 | | | |
| Cancellation fee | | $75 | $75 | | | |
| Couries Service | Outside TZ | USD 60 | USD 60 | | | |
| | Inside Tz | USD 50 | USD 50 | | | |
| **INWARD (EXPORT)** | | | | | | |
| Advising | Account holder | Account holder USD 120 | Account holder USD 120 | | | |
| | Non Account holder | Non Account holder USD 150 | Non Account holder USD 150 | | | |
| Advising Of Amendment | Account holder | Account holder USD 60 | Account holder USD 60 | | | |
| | Non Account holder | Non Account holder USD 100 | Non Account holder USD 100 | | | |
| **BILLS FOR COLLECTION** | | | | | | |
| **OUTWARD** | | | | | | |
| Documentary Bills for collection (Payment) | | SWIFT charge $35 | SWIFT charge $35 | | | |
| Doc handling fee | | $150 | $150 | | | |
| Courier Services | | $50 | $50 | | | |
| Tracer Fees | | $50 | $50 | | | |
| Clean bills for collection | | $150 | $150 | | | |
| **INWARD** | | | | | | |
| Documentary Bills for collection (doc handling) | | $125 | $125 | | | |
| Clean bills for collection | | $125 | $125 | | | |
| Delivery of documents free of payments, in terms of remitting bank's instructions | | $50 | $50 | | | |
| Avalizing | | 1% min $150 however subject to adequate Security and approval | 1% min $150 however subject to adequate Security and approval | | | |
| Negotiation fee | | | | | | |
| Confirmation | | | | | | |
| Courier charges | | $50 | $50 | | | |
| **GUARANTEES** | | | | | | |
| **Outward (Local only)** | | | | | | |
| Establishment fee | | 1% on establishment per quarter and part thereoff min 300 | 1% on establishment per quarter and part thereoff min 300 | | | |
| Guarantee Amendment | | US$150 | US$150 | | | |
| Extensions and increases to amounts | | 1% on establishment per quarter and part thereoff min 300 | 1% on establishment per quarter and part thereoff min 300 | | | |
| **Inward Guaratees/Counter Guarantees ( Local and International)** | | | | | | |
| Advising | Account holder | Account holder USD 120 | Account holder USD 120 | | | |
| | Non Account holder | Non Account holder USD 150 | Non Account holder USD 150 | | | |
| Establishment Fee | | 1% on establishment per quarter and part thereoff min 300 | 1% on establishment per quarter and part thereoff min 300 | | | |
| Advising of Amendment | Account holder | Account holder USD 60 | Account holder USD 60 | | | |
| | Non Account holder | Non Account holder USD 100 | Non Account holder USD 100 | | | |
| Extention for increase of amount | | 1% on establishment per quarter and part thereoff min 300 | 1% on establishment per quarter and part thereoff min 300 | | | |
| Guarantee amendment | | USD 100 | USD 100 | | | |
| **LOAN** | | | | | | |
| Processing/ Arrangement/ Appraisal fee | | | | | | |
| Personal Loans | | 2.00% | 2.00% | | | |
| Overdrafts | | 2% of the facility min 100 000. | 1.5% of the facility min $100 | | | |
| Mortgage Finance | | 1.77% | 1.77% | | | |
| Asset Finance | | 1.18% | 1.18% | | | |
| Early repayment | | 5.9% of the oustanding balance | 5.9% of the oustanding balance | | | |
| Early repayment (2nd Partial settlement) | | 3% of the oustanding balance | 3% of the oustanding balance | | | |
| Valuation fees | | As per valuer | As per valuer | | | |
| Base/Prime Lending Rate | | 21% | 10% | | | |

215074002

Stanbic Bank Moving Forward™
A member of Standard Bank Group

# Dar wafurahia ukombozi maji

**Na Frank Monyo**

WANANCHI zaidi ya 200,000 wa mtaa wa Msakuzi, Kata ya Kwembe Ubungo, wameishukuru serikali na Mamlaka ya Majisafi na Majitaka Dar es Salaam (Dawasa) kwa kuwafikishia huduma ya majisafi ambayo waliikosa tangu uhuru.

Wakizungumza juzi, wakati wa uzinduzi wa kizimba cha maji katika kata hiyo, Fredy Masha, alisema wanaona ni kama ndoto maji kutoka kwenye bomba, kwa kuwa muda mrefu wamekuwa wakipata shida ya maji na kuingia gharama kubwa kwa kununua maji kwenye magari.

"Tunaishukuru sana serikali na Dawasa kwa kutuletea maji katika mtaa wetu, tulikuwa tunapata shida sana kila siku tulikuwa fedha nyingi kununulia maji, lakini kwa hivi sasa tutapumua baada ya kuyaona maji katika mabomba yetu," alisema Masha.

Naye Francisca Mbelwa, alisema wamekunywa maji ya chumvi kwa muda mrefu na kuyanunua kwa bei ya juu, hivyo sasa ni furaha kwa kuwa hawakuamini kama wangekumbukwa kutokana na kuwa walishakata tamaa ya kuona maji yakitoka kwenye kuta za nyumba zao.

"Tumekunywa sana maji ya chumvi yanayotoka kwenye visima, hapo mtu kama huna hela ya kununua maji kutoka kwenye magari inabidi uvumilie tu, lakini leo tumeambiwa haya maji yatakuwa yanatoka kwa saa 24 na yatakuwa yanauzwa kwa ndoo kubwa shilingi 100, tunaishukuru sana serikali na Dawasa kwa kutuletea maji," alisema Mbelwa.

Akizungumza wakati wa uzinduzi wa mradi huo Mkuu wa Wilaya ya Ubungo, Kisare Makori, alisema moja ya jukumu ambalo Rais John Magufuli amewatuma ni kusimamia na kuhakikisha huduma muhimu za kijamii zinafika kwa wananchi hasa wanyonge.

"Katika vitu vinavyokera katika jamii ni ukosefu wa maji pamoja na umeme na ndio maana serikali ya Rais John Magufuli ina sera ya kumtua mama ndoo ya maji kichwani sambamba na kuhakikisha huduma za kijamii zinawafikia hasa watu wa chini," alisema Makori na kuongeza:

"Sio kwamba baba haruhusiwi kuchota maji bali katika adha ya kutafuta maji mama anahusika kwa nafasi kubwa. Sisi wanaume ni hodari wa kufunga kanga na kwenda bafuni kuoga tu."

Aliipongeza Dawasa kwa kupeleka maji katika mtaa huo na kwamba hatua hiyo itaondoa kero ya maji iliyokuwa inawasumbua wananchi kwa muda mrefu.

Meneja wa Dawasa Mkoa wa Ubungo, Mhandisi Pascal Fumbuka, alisema mradi wa mtaa wa Msakuzi utahudumia kaya 3,500 sawa na wananchi zaidi ya 200,000 na mpaka sasa wananchi zaidi ya 1,500 wamejitokeza kujaza fomu kwa ajili ya kuunganishwa na huduma hiyo.

"Tunatarajia kuongeza pato na kufikia shilingi bilioni 1.5 kwa mwezi na pia kupunguza wizi wa maji baada ya wananchi wa eneo hilo kuunganishiwa maji, kwa kuwa huduma ya kuunganishiwa maji wananchi ni ya mkopo na mteja ataingia mkataba na Dawasa ambapo utalipwa ndani ya mwaka mmoja," lisema Fumbuka na kuongeza:

"Katika Kata ya Kwembe Dawasa imejenga jumla ya vizimba vitatu kwa ajili ya kuhudumia wananchi wenye kipato kidogo, lengo kubwa ni kuhudumia wananchi hao wakati mwananchi mmoja mmoja akiunganishiwa maji na tumetoa maagizo ndoo ya maji itakuwa inauzwa shilingi 100 na tumeagiza kwa serikali ya mtaa asitokee mtu akauza maji juu ya bei hiyo."



Mkurugenzi Mkuu wa Baraza la Taifa la Usimamizi na Uhifadhi wa Mazingira (NEMC), Dk. Samuel Gwamaka, akiagana na Mkuu wa Shule ya Sayansi, Mazingira na Teknolojia wa Chuo Kikuu cha Dodoma (UDOM), Dk. Meserecordias Lema, baada ya kufungua warsha ya siku moja jijini Dar es Salaam. **MPIGAPICHA WETU**

# GDCS watathmini utekelezaji ilani CCM

**Na Yasmine Protace**

WASHIRIKI wa semina za Jinsia na Maendeleo (GDCS) zinazoandaliwa na TGNP Mtandao, wamekutana juzi Jijini Dar es Salaam na kufanya tathmini ya matamko katika ilani ambayo yalikuwa yakitolewa na serikali iya Chama Cha Mapinduzi (CCM) wakati wa kampeni kwa kuangalia mambo yaliyotekelezwa.

Pia washiriki walifanya uchambuzi wa mwonekano wa bajeti toka mwaka 2016 /2018, kwa kuangalia mwonekano wa vipaumbele katika mabadiliko.

Hayo yalisemwa na Clara Godson ambaye ni ofisa programu wa idara ya maarifa utafiti na uchambuzi kutoka TGNP Mtandao.

Clara alisema kuwa, katika semina hiyo, walichambua matamko na kuangalia sera katika ilani zinazofanya kazi. "Lengo kubwa la kuangalia matamko hayo tunaangalia lugha iliyopo katika ilani kama iko katika bajeti," alisema.

Aliongeza kuwa katika semina hiyo waliangalia pia masuala ya bajeti kwa wanawake inatekelezwaje.

Pia alisema washiriki walifanikiwa kujadili utekelezwaji wa ilani katika masuala ya kilimo, elimu na afya, na kwamba baadhi ya washiriki walipongeza TGNP Mtandao kwa kuwakutanisha kila Jumatano kwa kushiriki semina za jinsia na maendeleo.

Baadhi ya washiriki walioweza kupata nafasi ya kujadili matamko yaliyotolewa katika ilani ya chama tawala na utekelezwaji wake, na waliipongeza serikali ya awamu ya tano kwa kusimamia ilani yake na kuomba baadhi ya maeneo yaboreshwe.

Wakizungumzia suala la ajira, waliomba kuwapo na maboresho kutokana na idadi kubwa ya wahitimu wa vyuo na kukosa ajira.

Kuhusu elimu bure, walisema wazazi wamekuwa na mwitikio mkubwa wa kuandikisha watoto shule, lakini changamoto ni sehemu ya kuwaweka wanafunzi kwa kuwa haitoshi. Kwamba hali hiyo pia inawafanya walimu waelemewe na idadi ya wanafunzi wakati wa kuwafundisha.

Pia walipongeza kutolewa kwa vitambulisho kwa wafanyabiashara wadogo, lakini waliomba mazingira ya kufanyia biashara yaboreshwe.

# Wafugaji wapewa siri soko la maziwa

**Na George Tarimo,**
IRINGA

SERIKALI mkoani Iringa, imewataka wafugaji wa ng'ombe katika mikoa ya Nyanda za Juu Kusini kutumia fursa ya uwapo wa soko la uhakika la maziwa nchini kwa kuzalisha kwa wingi bidhaa hiyo ili kufaidika nalo wakati huu, ambapo serikali imeongeza kodi kwenye bidhaa ya maziwa yanayoingia kutoka nje.

Wito huo umetolewa na Mkuu wa Mkoa wa Iringa, Ally Hapi, kwenye mkutano maalumu wa kuwajengea uwezo wafugaji na wadau wa sekta ya maziwa ambao ni wafugaji wadogo kutoka mikoa ya Iringa na Njombe.

Hapi aliwataka wafugaji kufuga kisasa kwa kuwa mkoa wa Iringa umetenga maeneo maalum kwa ajili ya wawekezaji katika shughuli za mifugo.

Hapi alisema mkoa huo umetenga zaidi ya hekta 1,024,000 kwa ajili ya shughuli za ufugaji, Kilolo hekta 20,000, Iringa Vijijini hekta 98,000, Manispaa hekta 6,500 na Mufindi hekta 157.

Alisema atazungumza na shamba la mifugo la Sao hill ili kuwakopesha vijana na watu ambao wapo tayari kufuga kisasa mitamba wenye mimba, ili baadaye waweze kurejesha mkopo huo taratibu kwa lengo la kuinua kipato chao.

"Watanzania hawajachangamkia fursa hii ya kufuga kisasa kwasababu kiwanda cha Asas pekee kinahitaji maziwa lita 50,000 kwa siku, lakini kinapata lita 25,000 kwa siku," alisema Hapi na kuongeza: "Tunataka mfuge kisasa, ng'ombe wachache, lakini kwa faida, unawaangalia vizuri kwa kuzingatia ushauri wa wataalamu ili watoe maziwa mengi na kuondokana na kufuga.

# Waziri aagiza kiwanda nyama kikamilike Julai

**Na Zanura Mollel,** LONGIDO

WAZIRI wa Viwanda na Biashara, Joseph Kagunda, ametoa agizo kwa mmiliki wa kiwanda cha kuchakata nyama cha Elia Food Overseas, kilichoko Kata ya Eworendeke, wilayani Longido, kukamilika ifikapo Julai mwaka huu.

Alisema kiwanda hicho kimekamilika kwa asilimia 75 na hivi sasa ni Februari, haiwezekani kianze kazi Oktoba, hivyo naomba ifikapo mwezi wa saba kiwe kimekamilika na kazi zianze.

Alisema hayo alipokuwa katika ziara yake wilayani hapo alipokitembelea kiwanda hicho na kusema ifikapo mwaka 2020 Wilaya ya Longido itakuwa na viwanda vitatu vya uzalishaji.

Viwanda hivyo ni kiwanda cha ngozi katika Kata ya Kitumbeine, kiwanda cha maziwa kilichoko Longido na kiwanda cha kuchakata nyama cha Eworendeke.

Pia alifafanua kupitia viwanda hivi anategemea jamii itanufaika katika sekta ya ajira, na kumtaka mmiliki wa kiwanda cha kuchakata nyama kutoa ajira kwa wakazi wa Longido kwa asilimia 30.

"Niseme tu si ombi kuhusu kutoa ajira, naagiza asilimia 30 ajira ilenge wakazi wa eneo husika hata Longido inawasomi wa kutosha wapeni ajira, ni aibu sana unafiki kiwandani unauliza wafanyakazi wa Longido ni wa ngapi hakuna hata mmoja na kiwanda kipo hapo," alisisitiza.

Aidha, alimtaka mmiliki wa kiwanda hicho kutoa ajira kwa uwazi pasipo vificho vyovyote kwa kufanya hivyo kutajenga uhusiano mzuri na jamii iliyokuzunguka.

"Ajira iwe ya wazi na si kificho, naomba hilo ulielewe," alieleza.

Alimtaka kujenga uhusiano mzuri na vijiji, halmashauri pamoja na mkoa ili waweze kumsaidia katika kuhakikisha anapata mahitaji muhimu ndani ya jamii kwa wakati ikiwamo umeme na maji pamoja na ulinzi.

Alisema leseni ya kiwanda inamtaka mmiliki kuwa na michango kwa jamii aliyowekeza ikiwamo kusaidia miradi mbalimbali ya maendeleo mfano ujenzi wa shule pamoja na vituo vya afya.

Maeneo mengi wawekezaji kujenga wenyewe miradi hiyo na kisha kukabidhi kwa kijiji au halmashauri, niseme tu kwa sasa fedha za miradi ya maendeleo naagiza mzikabidhi halmashauri na ndiyo itakoyo panga bajeti na matumizi ya fedha hizo.

"Pelekeni halmashauri, watafuata utaratibu mzuri katika matumizi ya fedha hizo kwa mradi mkubwa, lakini thamani ya fedha iliyotumika ni kidogo, ninyi wawekezaji mtaletewa muhtasari wa mapato na matumizi juu ya fedha mliyoitoa," alisema.

Mkurugenzi wa Kiwanda cha Elia Food Overseas, Shabbir Virjee, alisema kiwanda hicho kitatoa ajira kwa vijana zaidi ya 100 na wanategemea kuanza kazi Oktoba ila kutokana na agizo la waziri watajitahidi kuhakikisha kinakamilika kwa wakati.

Alieleza ujenzi wa kiwanda hicho kilianza mwaka jana na wanategemea kuchinja mbuzi 200 kwa siku pamoja na ng'ombe 500 kwa siku.

Alifafanua watatoa elimu kwa wakazi juu ya ukataji na uchakataji wa nyama, pamoja na kutengeneza vitu mbalimbali vitokanavyo na malighafi ya mifugo ikiwamo ngozi.

Aidha, alisema atatenga eneo kwa ajili ya unenepeshaji wa mifugo kabla haijachinjwa ili kuhakikisha wanazalisha nyama yenye viwango itakoyokuwa ikisafirishwa nje ya nchi na hata ndani ya nchi.

"Usafiri mkubwa tutatumia ndege kupitia Uwanja wa Ndege wa Kimataifa wa Kilimanjaro," alidai.



Mwenyekiti wa Mtaa wa Manyara, Mji Mdogo wa Mirerani, wilayani Simanjiro Mkoa wa Manyara, Boaz Ambonya, akizungumza baada ya kutoa msaada wa magunia manne ya mahindi ya chakula cha wanafunzi wa shule za msingi Tanzanite na Songambele, jana. **PICHA: GIFT THADEY**

# Juhibu yapewa 5 ujenzi wa huduma za kijamii

**Na Jaliwason Jasson,** BABATI

BAADHI ya wajumbe wa Jumuiya ya Hifadhi ya Wanyamapori Burunge, (Juhibu), wameipongeza jumuiya hiyo kwa kusaidia kujenga miundombinu ya huduma za kijamii, huku wengine wakiomba mgao wa fedha zinatolewa kwa vijiji ziongezwe ili kuleta maendeleo.

Wakizungumza na Nipashe baada ya kupewa mafunzo ya kuwajengea uwezo viongozi hao ambao wamechaguliwa hivi karibuni kuiongoza taasisi hiyo.

Mmoja wa wajumbe kutoka Kijiji cha Sangaiwe, Magreth Jomba Yasso, alisema mgao wa fedha wanazozipata kutoka Juhibu unawatosha kwa kuwa zinawasaidia kujenga vyumba vya madarasa, vyoo na zahanati, hivyo, ameshauri uimarishwe mfumo wa kusimamia fedha hizo.

Alisema mafunzo aliyoyapata yamemsaidia kuelewa wajibu wake na kwa sasa yuko tayari kupambana na majangili watakaojitokeza kufanya uhalifu.

Alisema hata kama akikutana na ndugu yake anafanya ujangili atamripoti kwenye mamlaka husika ili kudhibiti ujangili.

Mjumbe mwingine, Pascal Mwaise, kutoka Kijiji cha Ngoley, alishauri taasisi hiyo kuwaongezea asilimia ya mgao wa fedha ili waweze kutanuka na kuongeza miradi ya kijamii kama ujenzi wa shule, vyoo, zahanati na nyumba za walimu.

Alisema kijiji hicho kimepata Sh. milioni 103 kwa mwaka huu, hivyo, akaomba Juhibu waongeze kiasi cha fedha kwa vijiji husika ili viweze kuendelea kujenga miundombinu bora kwa ajili ya maslahi ya umma kwa manufaa ya wananchi wote na kizazi kijacho.

Licha ya wajumbe hao kupongeza jitihada zinazofanywa na Juhibu, walisema mgao wa raslimali zinazotokana na uhifadhi katika maeneo hayo ukisimamiwa vizuri wana imani vijiji vyote vinavyohusika vitanufaika na hayatatokea manung'uniko dhidi ya taasisi hiyo.

Naye Spika wa Juhibu, Marcel Yenoio, alisema taasisi hiyo inalenga kustawisha uhifadhi wa wanyamapori na kuboresha uchumi wa wanachama wa vijiji husika.

Alisema wananchi watarajie uhifadhi ulio tukuka kwa ajili ya kulinda raslimali za wanyamapori ambao ndio wanawaingizia fedha kutoka kwa watalii.

Yenoio alifafanua kuwa Juhibu wanapopata fedha hizo mgao wao wanatoa asilimia 25 kwa serikali kuu, asilimia 10 wanaipa halmashauri, asilimia 65 inabaki Juhibu, ambapo wanagawana nusu kwa nusu na vijiji vilivyopo kwenye jumuiya hiyo, huku akisema asilimia 15 ya mgao wao ni ya uendeshaji wa raslimali na 10 inakuwa akiba.

# M'kiti asaidia chakula shuleni

**Na Mwandishi Wetu,** MIRERANI

MWENYEKITI wa Mtaa wa Manyara katika Mji Mdogo wa Mirerani, Boaz Ambonya, amewapa msaada wa magunia mawili ya mahindi wanafunzi wa shule za msingi Tanzanite na Songambele wapate chakula cha mchana, ili kuongeza nguvu na ari ya kupenda kusoma zaidi.

Mwalimu Mkuu wa Shule ya Msingi Tanzanite, Annusiatha Salla, alisema msaada wa chakula hicho utakuwa chachu kwa wazazi kupeleka chakula shuleni ili wanafunzi wao wapate chakula cha mchana.

Akizungumza wakati wa kukabidhi msaada huo jana, Ambonya, alisema wanafunzi watapata nguvu na ari ya kupenda kusoma zaidi na hivyo kuongeza ufaulu katika masomo yao.

Alisema baada ya kikao cha wazazi kilichofanyika hivi karibuni kwenye shule hizo kuamua kuchangia chakula, alijitolea magunia mawili kwa kila shule hizo mbili.

"Hivi sasa watoto hawatakuwa wanazunguka mtaani kutafuta chakula cha mchana, badala yake watakuwa wanasoma na muda wa kula watapata chakula shuleni kwao," alisema.

Alisema siyo jambo zuri wanafunzi kuhangaika mchana, lengo ni kuwa wale chakula shuleni wasome kwa bidii ili miaka ijayo wawe wataalamu wa sekta mbalimbali.

Salla, alisema baada ya wanafunzi hao kupata chakula hicho iwe changamoto kwa wazazi wao kupeleka chakula shuleni ili wale mchana.

Aidha, alisema wazazi wachangie chakula kama walivyoamua kwenye vikao vyao ili kuhakikisha wanafunzi wanasoma kwa bidii bila kuwa na njaa.

Mwanafunzi wa Shule ya Msingi Tanzanite, Emmanuel Mwakasege, alisema kupitia msaada huo wa chakula wanafunzi watasoma vizuri kwa kuwa watakuwa wanakula shuleni.

Mwakasege alisema baadhi ya wanafunzi walikuwa wanapata ugonjwa wa vidonda vya tumbo kutokana na kutokula mchana ila kupitia chakula hicho tatizo hilo litamalizika.

Mwanafunzi wa Shule ya Msingi Songambele, Nailat Mussa, alisema baadhi ya wanafunzi walikuwa wanakula matunda pori sababu ya njaa ila baada ya kupata chakula hicho wataondokana na kitendo hicho.





# Magari kupandisha watalii wazee mlimani

**Na Godfrey Mushi,** MOSHI

WATALII wenye umri kuanzia miaka 50 na kuendelea, sasa wataanza kutimiza ndoto yao ya kupanda Mlima Kilimanjaro kwa msaada wa magari maalum yanayotembea kwenye waya, serikali imesema.

Habari zilizopatikana jana na kuthibitishwa na Naibu Waziri wa Maliasili na Utalii, Constantine Kanyasu, zinaeleza kuwa serikali iko katika hatua za mwisho za kukamilisha mpango huo ambao ni moja ya mkakati wake wa kuongeza idadi ya watalii katika Hifadhi ya Taifa ya Mlima Kilimanjaro.

Kanyasu alitangaza ujio wa matumizi ya magari hayo, wakati akizungumza na menejimenti ya Hifadhi ya Taifa ya Mlima Kilimanjaro.

Kilimanjaro ndio mlima mrefu kuliko yote Afrika ukiwa na urefu wa mita za mraba 5,895 kutoka usawa wa bahari, na mrefu kuliko yote duniani ambao umesimama peke yake (free Standing Mountain).

"Moja ya mkakati wetu wa kuongeza idadi ya watalii ni huu tunaokuja nao wa kuanzisha magari yatakayokuwa yakitembea kwenye waya (cable cars) kwa ajili ya kutumiwa na watalii wenye umri mkubwa kuanzia miaka 50 wanaotaka kupanda Mlima Kilimanjaro. Mara nyingi watu wenye umri huo, baadhi yao hawawezi kupanda kwa njia ya kawaida," alisema Kanyasu.

Alisema mkakati huo utalenga zaidi kundi la watalii wenye bima za maisha zinazowaruhusu kusafiri na ndege kubwa zenye rubani wawili ambazo zitatua moja kwa moja kwenye hifadhi pamoja na wale wasioweza kusafiri kwa njia ya barabara kwa muda mrefu.

Naibu Waziri Kanyasu alieleza kwamba nchi imekuwa ikikosa fedha nyingi zinazotokana na watalii wa kundi hilo ambao ndio wengi wanaokuja nchini kwa ajili ya kutalii baada ya kustaafu.



Naibu Waziri wa Mifugo na Uvuvi, Abdallah Ulega (wa pili kulia), akisikiliza maelezo kutoka kwa Ofisa Mtafiti Mkuu wa Taasisi ya Chanjo za Mifugo Kibaha (TVI- Tanzania Vaccine Institute), Dk. Siha Mdemu (kulia), kuhusu chanjo ya homa ya mapafu ya ng'ombe (CBPP) ambayo inazalishwa katika taasisi hiyo wakati wa ziara yake mkoani Kibaha juzi. Kushoto ni Mbunge wa Kibaha Mjini, Sylvester Koka. **PICHA: HALIMA KAMBI**

# Mgogoro wa ardhi Bakwata, wananchi waisha

**Na Godfrey Mushi,** SIHA

SERIKALI imetangaza kumaliza mgogoro wa kugombea ardhi ekari 100, kati ya wananchi wa Kijiji cha Mkumbaro katika Wilaya ya Siha na Baraza la Waislamu Tanzania (Bakwata) la Mkoa wa Kilimanjaro.

Umiliki wa shamba hilo uliozua mgogoro kwa zaidi ya miaka minne sasa, umerejeshwa rasmi katika milki ya Bakwata.

Akizungumza jana wakati wa kukabidhi shamba hilo kwa Kaimu Shekhe Mkuu wa mkoa wa Kilimanjaro, Shaban Mlewa, Mkuu wa Wilaya ya Siha, Onesmo Buswelu, alisema baada ya serikali kufanya uchunguzi wa mapitio ya nyaraka, wamejiridhisha kwamba Bakwata ndio wamiliki halali wa ardhi hiyo.

"Shamba hili halina mgogoro tena na sasa ni mali ya Bakwata Mkoa wa Kilimanjaro, kama kuna mtu aliwadanganya wananchi wa Kijiji cha Mkumbaro, Kata ya Songu, kwamba limefutiwa hati ya umiliki, alete nyaraka. Nasisitiza tena wamiliki hawa wataendelea na shughuli zao kama kawaida bila kuingiliwa na mtu yeyote," alisema Buswelu.

Julai 6, mwaka 2016, Rais John Magufuli, wakati akihutubia Baraza la Idd El Fitri jijini Dar es Salaam, aliahidi kuwasaidia Waislamu kurudisha mali walizonyang'anywa ama kurubuniwa.

Rais Magufuli alinukuliwa akisema kuwa, serikali yake inapenda kuona mali za Waislamu zinarudi mikononi mwa Waislamu.

Baada ya makabidhiano hayo, Kaimu Shekhe Mkuu wa Mkoa wa Kilimanjaro, Mlewa, aliishukuru serikali kwa kutatua mgogoro huo uliodumu kwa takribani miaka minne.

Taasisi hiyo ya Bakwata na wananchi wa Mkumbaro waliingia katika mgogoro mwaka 2014 baada ya wananchi wa kijiji hicho kuvamia shamba hilo kwa kudai kuwa ni mali yao, baada ya Bakwata kushindwa kuliendeleza kwa muda mrefu.

Akifafanua zaidi kuhusu uhalali wao wa umiliki, Katibu wa Bakwata mkoani hapa, Awadhi Lema, alisema shamba hilo walipewa mgawo na serikali kwa ajili ya matumizi mbalimbali ya kimaendeleo, ambapo kila taasisi ya dini ilipatiwa ekari 200.

# Tanapa yawaita viongozi wa dini uhifadhi

**Na Godfrey Mushi,** MOSHI

SHIRIKA la Hifadhi za Taifa (Tanapa), limewaita viongozi wa dini katika vijiji 92 vinavyoizunguka Hifadhi ya Taifa ya Mlima Kilimanjaro (Kinapa), kuunganisha nguvu ya uhifadhi wa rasilimali asili na vita dhidi ya uharibifu wa mazingira ambao umegeuka tishio kwa ustawi wa jamii katika mkoa huo.

Kamishna Msaidizi wa Uhifadhi wa Shirika hilo, Martin Loiboki, amesema kwa kuwa hifadhi inagusa maisha ya watu ya kila siku, wameona ni vyema kukutana na viongozi hao wa dini ambao wakizungumza watu wanashindwa kubishana nao na wakisema wanaaminiwa na kusikilizwa.

"Ingawa tulishakutana na kamati 60 za uhifadhi wa mazingira na wadau wengine, tumewaita na nyie tuwashirikishe hili la kulinda hifadhi yetu isiharibiwe. Ushirikishwaji wa namna hii umekuwa kichocheo kikubwa katika kujenga uelewa wa pamoja baina ya wadau wa hifadhi na hivyo kuboresha ufanisi katika usimamizi na uendeshaji wa hifadhi zetu," alisema Loiboki.

Mkuu wa Wilaya ya Moshi, Kippi Warioba, akizungumza na viongozi hao wa dini alisema jitihada za pamoja na za dhati na za haraka zinahitajika katika kukabili janga la uharibifu wa mazingira linalokua na kuongezeka kwa kasi.

"Ukataji miti ovyo kwa ajili ya matumizi mbalimbali, mioto holela, kilimo, mifugo kupita kiasi, utupaji taka ovyo, ni baadhi ya mambo yanayochangia kwa kiasi kikubwa uharibifu wa mazingira.

"Suala la uhifadhi ni mtambuka linahusisha sekta mbalimbali, hivyo ni muhimu sisi sote kwa pamoja kuunganisha nguvu ili kuhakikisha kwamba uhifadhi unakuwa endelevu na unaoleta tija kwa wananchi kiuchumi na kijamii.

Ni ukweli usipongika kuwa uharibifu wa mazingira ni tishio kwa ustawi wa jamii katika mkoa wetu wa Kilimanjaro, taifa na dunia nzima."

Mhifadhi wa Ikolojia wa Hifadhi ya Taifa ya Mlima Kilimanjaro (Kinapa), Imani Kikoti, wakati anawasilisha mada kuhusu uhifadhi alisema eneo hilo linahifadhi bioanuai kubwa za aina mbalimbali za mazingira na viumbe, alisema hifadhi hiyo ina bioanuai kama aina 2,500 za mimea, aina 140 za wanyama na aina za ndege 177.

"Vivutio vya urithi wa dunia ambayo tunatakiwa kuvilinda kwa hali na mali ni kama mimea adimu na isiyopatikana sehemu nyingine duniani, barafu ya kudumu karibu na Ikweta (300km), maporomoko ya maji kama Lauwo na Kinukamori Water Falls. Pia tunahifadhi kwa sababu kuna kasoko kuu ya mlima (crater) na uwanda wa shira," alieleza Kikoti.



Ukurasa 18

Makubwa ya Tasaf yawakonga wadau DRC wakafuata darasa



Ukurasa 16

Msuguano wa ushuru ulivyotikisa ajira, upatikanaji nguzo za umeme

# BUFE

Ijumaa Februari 22, 2019

Nipashe

BIASHARA, UCHUMI NA FEDHA



## Britam Towers: Jumba refu Afrika Mashariki

Ukurasa 15



# Urejeshaji wanyama waliopotea nusu karne Hifadhi Kitulo inavyonasa watalii wapya

**Na Nebart Msokwa,** aliyekuwa Kitulo

HIFADHI ya Taifa Kitulo iko katika Wilaya ya Makete mkoani Njombe, ikiwa katika uwanda wa baridi, katika ukanda wa milima ya Livingstone, ambayo ndiyo inatenganisha wilaya za Makete na Rungwe, katika halmashauri yake ya Busokelo.

Ili kufika mahali hapo kuna njia kuu mbili za gari. Moja inaingilia kutoka mji wa Makete na nyingine inapandishha mlima kutoka eneo la mji mdogo wa Chimala, wilayani Mbarali, ambako kuna barabara kuu ya kwenda Mbeya kutokea Iringa.

Ni miongoni mwa hifadhi changa zenye vivutio vya kipekee kwa watalii wa ndani na nje ya nchi; uwanda wenye maua ya asili yanayopafanya pabatizwe 'Bustani ya Mungu,' inayonakshiwa na ndege, pia wanyama.

INAENDELEA UK.14

UCHUMI

## Habari katika picha



Ukurasa 17

KIUCHUMI ZAIDI Ukurasa 19

Takwimu za Biashara Ukurasa 20

Muhtasari wa Soko

## Biashara

Jumla ya Mauzo (bln) 22,136.24

Mauzo 109,584,255.00
Hisa 58,317

**Kielezo**

| | | |
|---|---|---|
| TSI | 4,207.58 | +0.00 |
| DSEI | 2,296.50 | -37.11 |

**ZILIZOPANDA**

| KAMPUNI | Bei | Badiliko% |
|---|---|---|
| KA | 180 | -2.70% |
| JHL | 9,500 | +1.06% |
| SWIS | 3,760 | +7.43% |
| EABL | 5,320 | -1.66% |

**ZILIZOSHUKA**

| KAMPUNI | Bei | Badiliko% |
|---|---|---|
| TCCL | 1,200 | -11.76% |
| ACA | 5,550 | -2.63% |
| NMB | 1400 | -1.41% |
| NMG | 2,510 | -1.57% |
| KCB | 840 | +2.44% |

UCHUMI

# Urejeshaji wanyama waliopote Hifadhi Kitulo inavyonasa wata

• Waongozaji: Neema, kazi zatuelemea • DC, Diwani wawapigia debe wakazi wao • Bidhaa yaipa jina 'Bustani ya Mungu'



Sehemu ya ofisi za Hifadhi ya Taifa Kitulo. **PICHA ZOTE: NEBART MSOKWA**

**INATOKA UK.13**

Mtu anapokuwa hifadhini humo, ni rahisi kuwaona ndege hao wa kuvutia kutokana na rangi zao adimu.

Hapo katika orodha wamo korongo mweusi na korongo mayombwe, wanaodaiwa kuhama kutoka Ulaya na nchi zingine za Afrika.

Taarifa za hifadhi zinaeleza, ndege wanapatikana kuanzia mwezi Novemba hadi Aprili, kisha wanaondoka na kurudi walikotoka.

Pia, nyani wa kipekee wajulikanao kitaalamu kama 'Rungwecebus Kipunji.' Rangi zao nyeupe na nyeusi nazo ni kivutio kimgine na wanaelezwa kugunduliwa katika miaka ya hivi karibuni.

Mahali hapo panapambwa na miti mirefu aina ya mitarakwa, iliyoko pembezoni mwa mkondo wa Mto Nhumbe, ikidaiwa ni miongoni mwa miti mirefu zaidi

> **"Katika kikundi chao wanatarajia kuboresha huduma kwa watalii wanaowaongoza, ili nao kuchangia ongezeko la watalii, wao pia wakinufaika kwa kipato.**



Pundamilia wapya waliofikishwa katika Hifadhi ya Taifa Kitulo, baada ya kutoweka kwa nusu karne.

Afrika Mashariki, kimo chake kinafika mita 50.

**ILIANZIA 1870**

Mhifadhi Mkuu wa Hifadhi ya Kitulo, Pius Mzumbwe, anasema historia hiyo inaanzia mwaka 1870, baada ya mpelelezi kutoka Uingereza, Fredrick Elton, kutembelea eneo hilo.

Anasema, mpelelezi alipofika hapo aliukuta uwanda uliopambwa na milima midogo vidogo yenye nyasi fupi na maua ya kupendeza. Mara moja akaipa jina la 'Uwanda wa Elton'.

Mzumbwe anaeleza kwamba huo baadhi ya wanyama wakiwa damilia, walikuwapo pamoja n ama wengine porini.

Hata hivyo, anasema wanya walitoweka miaka 50 iliyopi sababu ya kutokuwapo ulinzi i

BIASHARA

**Msuguano wa ushuru ulivyotikisa ajira, upatikanaji nguzo za umeme Sao Hill**

Ukurasa 16

UCHUMI

**Makubwa ya Tasaf yawakonga wadau DRC wakafuata darasa**

Ukurasa 18


BIASHARA

**Diwani anuia kuwabadilisha vijana waliofunzwa kuwa wazalishaji vijijini**

Ukurasa 19


# a nusu karne alii wapya





a wakati
amo pun-
a wany-

ama hao
ita, kwa
mara wa

maliasili za eneo hilo, wakati huo hapakuwa na hadhi ya hifadhi iliyo nayo sasa.

Mhifadhi huyo anasema, mwaka 1960 eneo kubwa la hifadhi hiyo lilichukuliwa na Shirika la Umoja wa Mataifa la Chakula na Kilimo (Fao), kwa ajili ya majaribio ya kilimo kuzalisha ngano na kufugaji kondoo wa sufi.

"Majaribio hayo hayakufanikiwa kutokana na sababu mbalimbali, hivyo likabadilishwa matumizi na kuwa eneo la kufugia ng'ombe wa maziwa mradi ambao unaendelea mpaka sasa kwenye eneo lililobakia jirani na hifadhi," anasema Mzumbwe.

Anaendelea kuwa, baadhi ya wadau wa mazingira na taasisi za hifadhi, waliendelea kutoa maoni serikalini kulihifadhi eneo hilo, ili kulinda raslimali zake na serikali ikayaridhia maoni hayo na pakatangazwa hifadhi, kupitia Gazeti la Serikali Namba 279 la Septemba 14 mwaka 2005.

Anasema Hifadhi ya Taifa Kitulo, kwa sasa ina ukubwa wa kilomita za mraba 465.4 ikijumuisha Bonde la Nhumbe na Hifadhi ya Misitu ya Mlima Livingstone, iliyopo upande wa Mashariki, kuitenganisha na Wilaya ya Rungwe. Milima ya Livingstone ina historia kitaifa, kwa kuwa ndiko alikopita mpelelezi David Livingstone, katika harakati za kutaka kuiunda Afrika kuwa koloni.

### UREJESHAJI WANYAMA

Mzumbwe anasema, Shirika la Hifadhi za Taifa (Tanapa), kwa kushirikiana na Shirika la Kimataifa la Wanyamapori (WCS), wameanza kurejesha wanyama waliotoweka kwenye hifadhi hiyo miaka 50 iliyopita, ili kuiongezea vivutio vya watalii.

Anasema, mashirika hayo yameshaleta pundamilia 21 kutoka Hifadhi ya Taifa ya Mikumi, mkoani Morogoro na kwamba wataendelea kupeleka wanyama wengine wadogo kwa awamu, kulingana na bajeti yao. Mhifadhi Mkuu anasema, baada ya eneo hilo kuhifadhiwa, ulinzi upo imara na wanyama walioletwa wanatarajiwa kuzaliana, ikiwa ni kivutio cha watalii kutoka maeneo mbalimbali ndani na nje ya nchi.

"Uwepo wa wanyama hawa utaimarisha mfumo wa ikolojia ya hifadhi na kuongeza vivutio kwa watalii wetu, hivyo kuongeza mapato katika eneo letu na taifa kwa ujumla," anasema Mzumbwe.

Anataja wanyama wengine ni kama mbega mweupe na mweusi, mbweha, sungura, minde, mbuzi mawe na kipunji, anayepatikana upande wa Busokelo.

### HALI YA UTALII

Mkuu wa Idara ya Hifadhi ya Kitulo, Eva Pwele, anasema katika kipindi cha miaka mitano iliyopita, walipokea wastani wa watalii wa ndani na nje kati ya 450 na 500.

Anasema watalii hao waliokuwa wanatembelea hifadhi hiyo, kati ya 150 na 200 ni wa ndani na wanaobaki ni wageni. Eva anafafanua:

"Baada ya kurejesha pundamilia katika hifadhi hii tunatarajia idadi ya watalii iongezeke kufikia kati ya 250 na 300 kwa wazawa na 500 hadi ya 650 kwa wageni na tunatarajia kiwango cha ukusanyaji wa mapato kuongezeka mara dufu."

Bila ya kutaja kilichokusanywa na ofisi, Eva anavitaja viingilio wanavyotozwa watalii hifadhini, kuna kiwango kidogo kwa wazalendo, kuanzia miaka 16 na kuendelea; wenye umri kati ya miaka mitano mpaka 15; na chini ya miaka mitano wanaingia bure.

Anaeleza kuwa kwa wageni wanaotoka nje ya Jumuiya ya Afrika Mashariki, wanatozwa Dola 30 (Shilingi 69,000) kwa wenye umri kuanzia miaka 16 na kuendelea na Dola 10, kwa wenye umri chini ya miaka 15 (Shilingi 34,500).

Vilevile anafafanua kuwa magari yana tozo lake maalum, kulingana na uzito wake, pia kutegemea na usajili wa nchini ambayo ni kiasi kidogo na nje ya nchi, yana kiasi kikubwa.

### DC MAKETE

Mkuu wa Wilaya ya Makete, Veronica Kessy, anaipongeza Tanapa kwa juhudi zake kuboresha ikolojia ya Hifadhi ya Kitulo, ikiwamo urejeshaji wanyama akidai kuwa itasaidia ongezeko la watalii.

Veronica anawataka wanavijiji wanaozunguka hifadhi kuchangamkia fursa ya ongezeko la watalii, kujipatia kipato kwa kuzalisha bidhaa zitakazonunuliwa na watalii.

Pia, anawataka wenye nyumba za kulala wageni na hoteli jirani kuboresha mazingira na huduma zao, ili wageni waone fahari kuhudumiwa katika maeneo hayo, badala ya kwenda kulala mbali.

"Nawashauri wananchi kuchangamkia hii fursa. Watalii wanapoongezeka, hata hali ya uhitaji wa vitu mbalimbali itaongezeka. Hivyo, kwa wenye hoteli lazima wafikirie kuboresha mazingira na wazalishaji wa bidhaa mbalimbali waongeze uzalishaji," anasema mkuu wa wilaya, huku akiwahimiza Watanzania kufika mahali hapo kutalii.

### WAONGOZA WATALII

Vijana wanaofanya kazi ya kuongoza watalii, wanasema dira mpya sasa inawapa uhakika wa kazi katika kipindi chote cha mwaka, kwa kuwa awali walitegemea vivutio vichache.

Mmoja wao, Jafari Ngogo, anasema watalii walikuwa wengi katika kipindi cha maua, lakini baada ya maua kunyauka hupata watalii wachache, hivyo kufanya kipato chao cha msimu.

Anaeleza mabadiliko kwamba, idadi ya watalii Kitulo kuliko waongozaji, kwa sababu idadi yao sasa inaongezeka.

Ngogo anasema, katika kikundi chao wanatarajia kuboresha huduma kwa watalii wanaowaongoza, ili nao kuchangia ongezeko la watalii, wao pia wakinufaika kwa kipato.

"Mwaka jana tulipokea makundi ya watalii 501, lakini kati ya 350 hadi 400 nilikuwa nawaongoza mimi. Sasa tunahitaji angalau waongoza watalii wengine waongezeke. Kikundi chetu kina wanachama 10 pekee ambao hata hivyo tuna majukumu tofauti," anasema Ngogo.

### DIWANI

Diwani wa Kata ya Matamba iliko hifadhi hiyo, Efeli Ng'ondya, anawataka wananchi wa kata yake, kuutumia utalii kuwa fursa ya kuongeza uzalishaji wa bidhaa mbalimbali kwa wateja watalii watakaowafikia, huku akiangaza uwepo wa ongezeko kwa shughuli za maendeleo kwenye vijiji vya kata yake.

# Alikosa ada chuoni, akaajiriwa dukani, sanaa sasa inamtoa



Veronica Kihampa akiwa kazini. Chini; bidhaa yake. **PICHA: BBC**

SANAA ya mikono, utengenezaji picha za mapambo kwa kutumia misumari, nyuzi, na mbao, ijulikanayo kama 'String Art', haijazoeleka katika jamii nyingi nchini na hata Afrika Mashariki kwa ujumla.

Veronica Kihampa (23), ni msichana aliyeamua kujikita katika kutengeneza mapambo na imefikia hatua ni ajira yake mpya, baada ya kulazimika kuacha kazi aliyoajiriwa dukani.

"Niliamua kuacha kazi ya kuajiriwa, ili kujikita zaidi katika utengenezaji wa picha hizi za mapambo, kwa kuwa zinanilipa zaidi kuliko kazi niliyokuwa nimeajiriwa," anasema.

Msichana huyo, anatengeneza picha nyumbani kwao na akiita sehemu yake hiyo ya kazi kwa jina la 'Ms Craft.' Awali aliajiriwa katika duka la kuoka na kuuza keki, jijini Dar es Salaam.

Mjasiriamali huyo, pia alishindwa kuendelea na masomo katika Chuo cha Ustawi wa Jamii, Dar es Salaam akiwa mwaka wa kwanza, baada ya kukosa ada, katika ngazi ya shahada.

Vifaa anavyotumia kutengeneza picha hizo ni mbao ambazo anazinunua kisha anaipiga msasa na kuziandaa kwa mchoro anaotaka kutengeneza na kisha anazigongea misumari, baada ya hapo anafuma nyuzi za rangi tofauti, ili kupata picha za kuvutia.

Picha anazotengeneza, zinatumika kama mapambo katika ofisi majumbani na wateja wengi wanazinunua kwa ajili ya kuwapa wengine zawadi.

Veronica anaeleza kuwa, licha ya kufanyia kazi zake nyumbani, anatumia mitandao ya kijamii kuwafikia wateja wengi kwa wakati mmoja na wamekuwa wanaongezeka, tofauti na awali alipoanza kazi hiyo. Anasema, wanunuzi wake wakubwa wa bidhaa hiyo ya sanaa ni kinamama. Anaeleza: "Wanawake wengi ndio wanunuzi wa kazi zangu, ambao hununua kwa ajili ya zawadi."

"Ila kwa upande wa wanaume ni wachache sana, wanahesabika na walionunua wengi wanataka kwa ajili ya ofisini, tofauti na wanawake wanaonunua kwa ajili ya zawadi," anafafanua. **BBC**



**BEI YA MAZAO** >> MCHELE 186739.13/- | ULEZI 144400.00/- **FEDHA** >> RAND 162.26 | KSH 22.92 | USH 0.63

BIASHARA

WAPANDA MITI TANGU 1939

# Msuguano wa ushuru ulivyotikisa ajira, upatikanaji nguzo za umeme Sao Hill

• Wawekezaji watii mwafaka, mambo katika zama zake

**Na George Tarimo,** Iringa

SERIKALI kupitia Wizara ya Maliasili na Utalii na Wakala wa Huduma za Misitu Tanzania (TFS), ina jukumu la kuanzisha na kusimamia mashamba ya miti ya serikali, ikiwa njia ya kukuza mapato na kuboresha maliasili.

Hivi sasa, serikali ina jumla ya mashamba ya miti 19 yanayosimamiwa na TFS na kwa asilimia kubwa yanachangia sana kwenye miradi yake nchini.

Mashamba hayo ni pamoja na Sao Hill, Shume, Meru, North Kilimanjaro, Mbizi na Rubare, Buhindi, Kawetire, Kiwira, Korongwe, Longuza, Mtibwa, North Ruvu, Rondo, Rubya, Ukaguru, Wino na West Kilimanjaro.

### SAO HILL

Shamba la Sao Hill lililoko wilayani Mufindi mkoani wa Iringa, ndilo kubwa zaidi, ambako ndiko kunakipande kikubwa, baadhi ya maeneo wilayani Kilombero, mkoani Morogoro.

Historia yake inaonyesha shamba hilo lilianzishwa mwaka 1939 kwa majaribio na hadi 1951, upandaji wa miti ulianza na ukaendelezwa kati ya mwaka 1960 hadi 1990, likifikisha ukubwa hekta 135,903 zilizohifadhiwa kwa ajili ya upandaji miti na hifadhi ya misitu asilia.

Takwimu zake pia zinaonyesha kuwapo hekta 56,500 zilizopandwa miti, hekta 52,500 zimepandwa miti laini aina ya misindano; hekta 4,000 zimepandwa miti migumu aina ya mikalatusi; hekta 48,000 ni hifadhi ya misitu ya asili; hekta 1,700 ni maeneo ya makazi; huku hekta, 29,503 ni eneo la hifadhi ya mazingira asilia na vyanzo vya maji.

### MIPANGO ILIYOPO

Malengo ya kuanzishwa mashamba hayo, ni kwamba kuna chanzo cha mapato ya serikali, utoaji ajira kwa wananchi, uzalishaji mbao na nguzo; uboreshaji hali ya Mufindi; pamoja na utunzaji mazingira.

Shamba lina bustani tatu ambazo ni Usokami, Kitasengwa na Irundi, zenye uwezo wa kuzalisha zaidi ya miche kati ya milioni nane na kumi.

Katika kuboresha mazingira nchini, serikali kwa kushirikiana na wadau wa maendeleo, wakiwamo wawekezaji wa ndani na nje, taasisi mbalimbali, inakusudia kupanda miti ya shughuli za maendeleo, ikiwamo nguzo za umeme.



Magari yakipakia nguzo kwa ajili ya kupelekwa sehemu mbalimbali za nchi, kukidhi mahitaji ya umeme.

> “Iwapo jambo hilo litatekelezwa litakuwa na athari kubwa kwao, kwa kuwa wanaendesha maisha yao kwa kutegemea kiwanda hicho.



Mkurugenzi wa kampuni ya kuzalisha na kusambaza nguzo za umeme Qwihaya, Benedicto Mahenda, akizungumza kiwanda hapo. **PICHA ZOTE: MAKTABA.**

### MVUTANO USHURU

Mwishoni wa mwaka jana, serikali wilayani Kilolo iliingia mvutano na kampuni ya Newforestry, ikidai kiasi cha kodi shilingi bilioni 2.9, kwamba inatokana na shughuli za uzalishaji mazao ya misitu na biashara ya nguzo unaofanywa na kampuni hiyo, kati ya mwaka 2012 hadi 2018.

Wakati Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri Wilaya Kilolo, Aloyce Kwezi, anasema deni linatokana na malimbikizo ya kodi na ushuru wa mazao ya misitu zikiwamo nguzo, kampuni hiyo ilipinga na kufanya iingiliwe kati na mamlaka za juu za serikali.

Usuluhisho uliishia kampuni hiyo kutakiwa kulipa ushuru kiwango cha asilimia tano, ambalo lilihitimishwa kwa Mkuu wa Mkoa wa Iringa, Ally Hapi, kutembelea viwanda vyote vya kuzalisha nguzo na baadaye aliwaita na kukutana nao ofisini kwake.

Ni sakata linalodaiwa kuwa ana athari katika upatikanaji nguzo za umeme, shughuli inayofanywa na Wakala wa Usambazaji Umeme nchini (REA), baada ya kukutana nao, baadhi ya wazalishaji nguzo mkoani Iringa, walikubali kulipa kama walivyoagizwa.

### WAZALISHAJI NGUZO

Ni wastani wa mwezi sasa, wazalishaji nguzo kiwanda cha Qwihaya, kilichokuwa kimesimamisha shughuli zake, kikisubiri ufumbuzi huo wa mvutano wa ushuru, kilianza tena shughuli zake.

Mkurugenzi wa kampuni hiyo ya kuzalisha na kusambaza nguzo za umeme, iliyoko Mafinga, Benedicto Mahenda, anasema awali nguzo za umeme zilitoka nje ya nchi, kama Afrika Kusini na Kenya, hivi sasa zinatoka nchini.

Anasema viwanda vya kuzalisha nguzo nchini, katika Mkoa wa Iringa viko vinane na kimoja jijini Tanga na anaongeza, wajibu wao kama wafanyabiashara kuhakikisha wanazingatia sheria zilizowekwa na serikali.

Pia, Mahenge anasema wao wawekezaji wanaomba kuelimishwa vyema masuala ya tozo za mazao ya misitu, ili kuepuka mgongano usio wa lazima.

“Sasa sio muda wa kufanya kazi kwa mazoea, tunaomba kama kuna sheria nyingine, ni vizuri watuambie, ili kesho na keshokutwa, tunapoomba tenda wawe wanajuwa vinavyotakiwa.

“Sisi kama wafanyabiashara hatutaki presha wala hatuna lengo la kukwepa, ila ni suala la kutokujuwa sheria na watendaji hawajui ni kitu gani na kubaki kufanya kazi kwa mazoea,” anasema Mahenda.

Qwiahaya anataja changamoto kubwa inayokabiliwa ni ukosefu wa dawa za kutengenezea nguzo, bati na misumari anayoiita ya ‘U’.

Anataja ushirikiano wa kampuni yake iliyoajiri watu 300,000 na maisha ya jamii, kwamba imejenga vyumba vya madarasa kwa baadhi ya shule za msingi na sekondari, makanisa, kufadhili vilabu vya soka na wasanii.

Islam Huwel, ambaye ni msimamizi wa kiwanda cha Polls Industry, anaeleza utayari wao kushirikiana na serikali katiika ulipaji kodi, ili iendelee kuwawekea mazingira rafiki ya uwekezaji, nao waongeze uzalishaji wa nguzo unaoendana na mahitaji nchini.

Katibu wa Wafanyakazi wa New Forestry, Oddo Nkwera, anasema kutokana na athari iliyojitokeza, kiwanda kiliwapatia wafanyakazi wake likizo isiyo na malipo, hadi mgogoro utakapomalizika.

Alisema iwapo jambo hilo litatekelezwa litakuwa na athari kubwa kwao, kwa kuwa wanaendesha maisha yao kwa kutegemea kiwanda hicho.

### DC

Mkuu wa Wilaya ya Mufindi, Jamhuri William, anasema wilaya imeshatoa magari zaidi ya 48 kusafirisha nguzo kupeleka sehemu mbalimbali nchini na kulipa baadhi ya madeni anayodaiwa.

William anasema, wawekezaji wote wilayani pia wameshaanza kulipa madeni. Anafafanua: “Nawaomba wafanyabiashara wa Mufindi zingatieni sheria, kanuni na taratibu katika kufanya biashara na kufanya hivi mtakuwa mmechangia mapato ya serikali, ili serikali iweze kutoa huduma bora kwa wananchi,” anasema William.

Anazitaka kampuni za nguzo zenye miradi kuongeza usafirishaji nguzo ili kukidhi mahitaji husika.

***Mwandishi anapatikana kwa anwani: georgetarimo5040759@gmail.com au simu +225-719057666.***

# Biashara katika picha




Meneja Uhusiano na Mawasiliano wa Kampuni ya simu ya Zantel Tanzania, Rukia Mtingwa (wa tatu kushoto), akiangalia majina ya washindi wakati wa droo ya pili ya promosheni ya tumia EzyPesa ushinde iliyofanyika jijini Dar es Salam jana. Kushoto ni Msimamizi kutoka wa Bodi ya Michezo ya Kubahatisha nchini, Jehud Ngolo na Meneja wa Zantel Kitengo cha Bidhaa EZYPESA, Leonard Kameta. Wateja 30 walijishindia simu za kisasa za mkononi (Smartphones). **NA MPIGAPICHA WETU**



Wachuuzi wa pipi wakiwa wamepumzika baada ya pilikapilika za kusaka wateja katika eneo la stendi kuu ya mabasi ya Ubungo, jijini Dar es Salaam jana. **PICHA MIRAJI MSALA**



ijana wakitafuta wateja wa kuwauzia vitu mbalimbali kwa kutangaza na kipaza sauti katika eneo la Goba Tegeta A, jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: MIRAJI MSALA**

**BEI YA MAZAO >> MAHINDI 52000.00/-| MAHARAGE 178043.48/-**

BIASHARA

# Makubwa ya Tasaf yawakonga wadau DRC wakafuata darasa

- Waomba wakufunzi, wanafunzi, 'notsi'zao
- Kikundi Tujikwamue: 'Senti' hadi 'maelfu'

**Na Elizabeth Zaya**

WASWAHILI wanasema 'penye nia pana njia.' Ni usemi uliotumiwa na kikundi cha wanawake cha vikoba kiitwacho 'Tujikwamue' katika barabara ya Mwinyi, Kilakala, wilayani Temeke, Dar es Salaam.

Hao ni wanufaika wa mpango wa uhawilishaji fedha katika wilaya hiyo ya Temeke, ambao baada ya kuingizwa katika mpango huo, 'walijiongeza' na kuunda kikundi cha kujiwekea akiba kutoka sehemu ya fedha ya ruzuku wanayopewa na Mfuko wa Maendeleo ya Jamii (TASAF).

Katibu wa kikundi hicho, Chamsia Ng'onde, anasema baada ya kuanza kupata awamu ya kwanza ya ruzuku hiyo ya Tasaf, mwaka 2016, walishauriwa na maofisa kutoka katika mfuko huo kujiwekea akiba. Anasema, pia waliwashauriwa kuanzisha vikundi vya miradi midogo ya kujiingizia kipato.

"Wakati wanatupatia ushauri huo, tulikuwa tunaona kama ni utani, kwa sababu tuliona pesa ni ndogo. Lakini, walipotuita katika semina na kutufundisha matumizi ya kila pesa tuliyokuwa tukipata, tulianza kuona kwamba inawezekana," anasema Ng`onde na kuongeza:

"Tulifundishwa kutumia mpaka shilingi 500 tunayoipata na ndipo tulipoona tunaweza kuanzisha kikundi cha kujiwekea akiba kila wiki na tulifanya hivyo, kwa kuanza kuweka akiba ya shilingi 1000 kila wiki. Tuliendelea hivyo, mpaka tukaongeza hadi shilingi 2000 kwa wiki."

#### MWANZO UWEKEZAJI

Ng`onde anasema, baada ya kufikia kiwango hicho, walianza kukopeshana shilingi 10, 000 kwa riba ya shilingi 1000, waliojipangia kuzirudisha kwa muda wa wiki mbili.

Anasema, ilikuwa hatua ya mwanzo kabisa iliyowasaidia kila mmoja kuanzisha miradi midogo ya kujiongezea kipato.

"Tuliendelea kufanya hivyo mpaka mwaka 2017. Tulitoka hapo na kuanza kukopeshana shilingi 200,000 hadi mwaka 2018, faida iliongezeka kutokana na faida tunayoipata katika riba ya mikopo na tukafanikiwa kuwekeza katika ardhi kwa kununua ekari 12 katika eneo la Bupo Mkuranga, mkoani Pwani," anaeleza, kuwa wameshapiga hatua wanatafuta shamba lingine waendeleze kilimo.

"Kikundi kimetusaidia sana kubadilisha mawazo ya kukata tamaa tuliyokuwa nayo awali. Zamani tulikuwa tumekata tamaa, lakini sasa hivi tukikutana wanakikundi tunajadiliana namna ya kuweka hisa, jamii na dharura na tunajadili kwamba biashara gani tuifanye, ili tujikwamue kimaisha," anasema Ng`onde.



Mkurugenzi Mtendaji wa Tasaf, Ladislaus Mwamanga (aliyeshika kitabu), akiangalia bidhaa zilizotengenezwa na walengwa wa Mpango wa Kunusuru Kaya Maskini (Tasaf), katika eneo la Makangarawe, wilayani Temeke, Dar es Salaam. **PICHA: MTANDAO**

> **"Mimi kupitia ujasiriamali ambao nafanya kwa sasa, nina uwezo wa kuwalipia wanangu usafiri na kwa mwezi nalipa zaidi ya Shilingi 60,000.**

Ngonde anafafanua: "Kwa hiyo, tumekuwa ni wengine kabisa, tumebadilika kimawazo na mtazamo na hata yale mawazo ya kujiona maskini tusiyoweza lolote yameisha kabisa."

Anasema, Tasaf kupitia kikundi hicho, wanapelekewa wataalamu wa kuwafunza ujasiriamali na sasa wana ujuzi mkubwa wa kutengeneza bidhaa mbalimbali, zikiwamo nguo, sabuni na vyakula.

Kwa mujibu wa Ngonde, bidhaa zao kwa sasa wanazitumia kushiriki katika maonyesho mbalimbali ya biashara, ikiwamo Nanenane, Sabasaba na sehemu nyingine zenye mkusanyiko wa watu.

"Kikubwa ambacho kila mwanakikundi akiulizwa sasa hivi akiseme, hawezi kuacha kuishukuru serikali kupitia Tasaf kwa kuleta mpango huu wa kuzisaidia familia zinazoishi katika mazingira magumu. Bila ya mpango huu, sijui tungekuwa wapi?" Anatamka Ng`onde.

#### MAFANIKIO BINAFSI

Ng`onde anajitambulisha binafsi, kwamba ana watoto watano kwa sasa, anaweza kuwahudumia kwa urahisi tofauti na ilivyokuwa awali.

"Ninashukuru kwamba serikali imeondoa ada, pia Tasaf inagharimia katika mahitaji ya sare za shule za watoto wangu na mahitaji madogo, anasema katibu huyo, anayefafanua:

"Mimi kupitia ujasiriamali ambao nafanya kwa sasa, nina uwezo wa kuwalipia wanangu usafiri na kwa mwezi nalipa zaidi ya Shilingi 60,000."

Mama huyo anasema, kupitia kuinuliwa na Tasaf, anasimulia kwamba kupitia Tasaf amejenga nyumba yenye vyumba vinne katika mtaa huo wa Kilakala, akitaja vyanzo vya kipato ni miradi midogo aliyoianzisha, baada ya ujuzi na wataalamu wa maendeleo ya jamii.

"Unavyoniona hapa mimi, nimejenga nyumba ina vyumba vinne vya kulala hapa Kilakala na kama unataka twende ukashuhudie. Sijamalizia, lakini nimeshahamia naishi na wanangu.

"Sikutaka kuendelea kulipa tena kodi katika nyumba ya kupanga, kwa sababu nilipata shida sana na sitamani. Kukumbuka, nitaendelea kuishi humu huku namalizia kuikarabati," anaeleza.

Ng`onde anasema, nyumbani kwake ana miradi binafsi ya kufuga kuku na sungura, wote ni zao la mafunzo ya ujasiriamali kutoka kikundi cha vikoba vya walengwa wa Tasaf.

Ng`onde anasema, ni hatua inayomfanya kuwa mfano wa kujifunzia kwa kaya nyinginezo zinazoishi katika hali ngumu aliyopitia.

#### WAGENI WAVUTIWA

Mafanikio ya miradi ya Tasaf kwa kaya maskini, hivi sasa yamekuwa mvuto, kwasababu kuna watu kutoka nchi nyinginezo zenye miradi ya kuwezesha kaya maskini, wanamtembelea nchini kushuhudia.

Mkurugenzi wa Mfuko huo wa Maendeleo ya Jamii wa Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo (DRC), Ruphin Bo Elongo, anakiri Tasaf imepiga hatua kubwa, tofauti na nchini kwao.

"Tanzania wako mbali sana katika uwezeshaji wa kaya maskini. Ni nchi ambayo haipaswi kubezwa kwa hatua hizi walizopiga katika kupunguza umaskini na ndio maana tumeamua kuja kujifunza kutoka kwao.

"Tunaamini tukirudi kwetu tutafanya uboreshaji mkubwa na sisi kutokana na haya tuliyojifunza kutoka Tasaf Tanzania," anasema Elongo.

"Tumekuwa tukiambiwa tu kwamba wamefanya vizuri katika kusaidia kaya maskini, kwa hiyo tuliona tusiishie kuambiwa tu na ndiyo maana tukaamua kwamba tuje kujionea wenyewe, tuwaone walengwa na tuzungumze nao, ili tuelewe zaidi namna kazi inavyofanyika.

"Tumeona kazi ambazo walengwa wanafanya ni nzuri sana kwa sababu imewasaidia kutoka hali ya umaskini na wamejisaidia kimaisha kupiga hatua kwenda mbele," anasema mkurugenzi huyo.

Elongo anasema wanajipanga kuwatumia wanufaika wa Tasaf, kwenda kutoa elimu nchini kwao namna, wanavyotumia ruzuku kidogo kuanzisha miradi yenye manufaa.

"Tumetembelea walengwa wa mpango unaoendeshwa na Tasaf, kwa kweli wametupa 'challenge' (changamoto) tumebaki tunajiuliza ni kwa namna gani na sisi tutafika hapo walipofika wao.

"Tumejadiliana kwamba tuwaombe Tasaf, watupe baadhi ya maofisa, ili waje watuonyeshe mbinu walizotumia hasa namna ya walengwa wanavyojimudu katika kutumia kiwango kidogo cha fedha ya ruzuku kufanyia ujasiriamali na kujiongezea kipato."

FEDHA >> USD 2299.45| Pauni 2999.63| Euro 2608.04

UCHUMI

# Diwani anuia kuwabadilisha vijana waliofunzwa kuwa wazalishaji

**Na Amri Lugungulo,** Kisarawe



Kiongozi wa kikundi cha Vijana Tujikwamue na Umaskini' cha Mbezi Kwa Yusuph, Kata ya Msigani, Rechnold Msaki, akizungunza katika mkutano. Kulia ni Jabir Mahmoud wa jukwaa la vijana Temboni. **PICHA ZOTE: MTANDAO**

KISARAWE ni miongoni mwa wilaya nchini iliyoko Mkoa wa Pwani, iliyobahatika vijana wake 102 wanaotoka katika vikundi 23, kupata fursa za mafunzo mbalimbali ya kuwajenga, ili kuweza kujiendesha kiuchumi.

Lakini, maarifa hayo wanayoyapata yanayeyuka, baada ya muda kutokana na kukosa uongozi wa kuwasimamia vijana hao wa wayatumie maarifa waliyoyapata kwa vitendo.

Katika kata ya Kurui, ambako diwani wake ni Mussa Kunikuni, anasema vijana wake wamekuwa wakipata mafunzo mbalimbali, yakiwamo ya ufundi uashi, useremala, kufuga nyuki, upishi, ufundi umeme, lakini kila wanapoyapata, huyeyuka.

Sababu kuu inatajwa ni kukosekana usimamizi wa kuwawezesha kutumia maarifa hayo wajiendeshe kiuchumi.

Hivi sasa vijana wengi waliopata fursa hiyo, ni wale wanaoendekeza kuishia maisha tegemezi na kwamba, baada ya kupata mafunzo hayo, walipewa vifaa vya kuvitumia, ili viwawezeshe kufanyia kazi za kujiendesha kiuchumi.

Lakini, kama hawana usimamizi thabiti, wanashindwa kupata fursa ya kuvitumia vifaa wanavyopewa kufanya kazi na inapofika hatua, wanakosa fursa hiyo, baadhi ya vijana hukimbilia mijini kutafuta kazi, kwa kutumia maarifa waliyoyapata mafunzoni, kuendesha mashirika mbalimbali yasiyo ya kiserikali au taasisi za watu binafsi na za umma.

Ni maisha ambayo, kila wanapokwenda mijini, vijana hao hutaabika kutafuta kazi na hata wanapopata kazi, malipo yao huwa ni madogo, kiasi cha kwamba hushindwa kukimu mahitaji ya kila siku, wakiangukia tena katika hali ngumu ya kimaisha.

Baadhi ya vijana wanaobaki vijijini, nao wanashindwa kutumia maarifa waliyo nayo, kutokana na kila mmoja kuendelea kuishi 'kivyake' na wakidumu katika mfumo wa maisha tegemezi.

Vijana hao mara nyingi wamekuwa wakigawanyika katika vikundi wakati wa mafunzo, kwa mtindo wa vijiji au kwa mfumo wa fani.

**SOMO LA KURUI**

Kata ya Kurui, ina vijiji vinne ambavyo ni: Kidugalo, Kurui, Mtakayo na Zegero, fani kuu zikiwa uashi, useremala, upishi, ususi, ufinyanzi, ufugaji nyuki, kuku, na kilimo cha mboga.

Hivyo, diwani huyo baada ya kubaini tatizo la vikundi vingi kufa au hafavinyi kazi, alibuni wazo la kuepusha balaa hilo la kufa kwa vikundi.

> **"Naomba wadau wengine wa aina mbalimbali kuendelea kuwasaidia vijana hao, ili kujiendesha kiuchumi kuepukana na kukimbilia mijini, ambako wanapata mateso makubwa, ikiwamo kukosa kazi na kunyanyasika.**



Diwani wa Kata ya Kurui, Kisarawe, Mussa Kunikuni.

Mbinu na mikakati aliyobuni ni kwamba aliitisha mkutano katika kijiji cha Mtakayo, kwa kushirikisha vijana wote waliowahi kupata mafunzo yaliyoendeshwa na shirika la Plan International, hivi karibuni.

Mafunzo hayo yaliitwa YEE yaliyokuwa na ratiba ya mafunzo yakiwamo upishi, ushonaji na ufundi bodaboda yaliyodumu kwa muda wa miezi sita mwaka jana kwenye vijiji vya Mtakayo na Kurui.

Kutokana na wasiwasi wa kufa makundi hayo, diwani huyo aliitisha mkutano wa vikundi Januari 20 mwaka huu, na kuwashauri kutengeneza katiba ya vikundi vyao vyote na kuchagua viongozi, kisha wakapate usajili, kuhakikisha vijana wote wa kata hiyo wanajiendesha kichumi na kutoa hamasa ya aina mbalimbali, ikiwamo na elimu ya afya na mapambano dhidi ya Ukimwi.

Diwani Kunikuni anasema hatua hiyo ya kukutana na vikundi, aliifikia baada ya Ofisa Maendeleo Jamii wa Wilaya, kuwaita Madiwani wa Halmashsuri ya Wilaya Kisarawe, akitaka vikundi vyote vilivyopata mafunzo, wao madiwani wakawe walezi wao.

Diwani huyo anavisifu vikundi kadhaa vilivyopata mafunzo yaliyotolewa na mashiriki mbalimbali na kupata usimamizi, kwamba vinaendelea vizuri na kuleta tija ndani ya kaya hiyo.

Miongoni mwa vikundi vinavyoendelea kuleta tija na ambavyo vilipata mafunzo kwa ufadhili wa Shirika la Care International ni Jumuiya ya Mikopo na Maenddeleo (RUCDO), Baraza la Uwezeshaji Vijana Kiuchumi Kurui (BUVIKKU).

"Naomba wadau wengine wa aina mbalimbali kuendelea kuwasaidia vijana hao, ili kujiendesha kiuchumi kuepukana na kukimbilia mijini, ambako wanapata mateso makubwa, ikiwamo kukosa kazi na kunyanyasika," anasema.

Aidha, analishukuru Shirika la Plan International kwa msaada wa kuwapa mafunzo vijana hao.


# Takwimu za Biashara

Na Edward Ntwale & Elias Samweli

Bei ya Mazao Ya Chakula kwa Sh/kilo 100 Februari 20, 2019

| Mkoa | Arusha | D'Salaam | Dodoma | Kagera | Kilimanjaro | Kigoma | Manyara | Mbeya | Morogoro | Rukwa |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| Mahindi | 43,000 | 70,000 | 45,000 | 60,000 | 48,000 | 50,000 | 54,000 | 40,000 | 49,000 | 50,000 |
| Mchele | 200,000 | 230,000 | 190,000 | 185,000 | 180,000 | 160,000 | 200,000 | 185,000 | 170,000 | 160,000 |
| Mtama | 40,000 | 60,000 | 35,000 | 100,000 | 80,000 | 70,000 | 42,000 | 105,000 | 100,000 | 80,000 |
| Uwele | 42,000 | 70,000 | 32,000 | 110,000 | NA | 60,000 | 100,000 | NA | 100,000 | NA |
| Ulezi | 73,000 | 140,000 | 85,000 | 150,000 | 180,000 | 150,000 | 120,000 | 115,000 | 180,000 | 200,000 |
| Ngano | 80,000 | 130,000 | 160,000 | NA | 108,000 | 150,000 | 120,000 | 120,000 | 150,000 | 110,000 |
| Maharage | 150,000 | 210,000 | 165,000 | 150,000 | 180,000 | 145,000 | 150,000 | 180,000 | 180,000 | 200,000 |
| Viazi Mviringo | 78,000 | 75,000 | 66,000 | 75,000 | 65,000 | 90,000 | 62,500 | 50,000 | 80,000 | 80,000 |

## Mwenendo wa Shilingi




## Mafuta

Bei : Kuanzia Februari 6, 2019

| MKOA | DSM | Arusha | Kibaha | Dodoma | Geita | Katavi | Kigoma | Moshi | Lindi | Mwanza |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| Petroli | 2,120 | 2,255 | 2,125 | 2,179 | 2,286 | 2,329 | 2,352 | 2,245 | 2,110 | 2,271 |
| Dizeli | 2,080 | 2,299 | 2,084 | 2,139 | 2,245 | 2,288 | 2,311 | 2,289 | 2,089 | 2,230 |
| M'Taa | 2,046 | 2,286 | 2,050 | 2,105 | 2,211 | 2,254 | 2,277 | 2,276 | 2,105 | 2,196 |

## Soko la Hisa la Dar es Salaam Kikao cha Februari 20, 2019

### Muhtasari

| | | |
|---|---|---|
| TSI | 3,533.65 | +0.00 |
| DSEI | 2,125.40 | -17.30 |

| | |
|---|---|
| Thamani za Hisa (bln) | 20,486.56 |
| Mauzo | 64,647,000.00 |
| Hisa | 297,970 |

### Zilizopanda na Zilizoshuka

| Kampuni | Bei | Badiliko |
|---|---|---|
| EABL | 4,560 | -2.98% |
| KCB | 940 | -3.09% |
| KA | 185 | -2.63% |
| ACA | 6,750 | +2.27% |

### Viwango vya kubadilisha

| Fedha | Nunua | Uza |
|---|---|---|
| EUR | 2,591.28 | 2,617.65 |
| USD | 2,268.07 | 2,290.76 |
| KES | 22.38 | 22.56 |
| GBP | 2,947.82 | 2,977.52 |

### Bei za hisa hadi kikao cha Februari 20, 2019

| Kampuni | Bei ya mwisho | Bei Iliyopita | Ba'liko % |
|---|---|---|---|
| ACA | 6,750 | 6,600 | +2.27 |
| CRDB | 135 | 135 | +0.00 |
| DCB | 340 | 340 | +0.00 |
| DSE | 1,300 | 1,300 | +0.00 |
| EABL | 4,560 | 4,700 | -2.98 |
| JHL | 9,700 | 9,700 | +0.00 |
| KA | 185 | 190 | -2.63 |
| KCB | 940 | 970 | -3.09 |
| MBP | 490 | 490 | +0.00 |
| MCB | 500 | 500 | +0.00 |
| MKCB | 800 | 800 | +0.00 |
| MUCOB | 400 | 400 | +0.00 |
| NICO | 170 | 170 | +0.00 |
| NMB | 2,340 | 2,340 | +0.00 |
| SWALA | 490 | 490 | +0.00 |
| SWIS | 2,340 | 2,340 | +0.00 |
| TBL | 11,700 | 11,700 | +0.00 |
| TCC | 17,000 | 17,000 | +0.00 |
| TCCL | 640 | 640 | +0.00 |
| TICL | 385 | 385 | +0.00 |
| TOL | 660 | 660 | +0.00 |

## VIWANGO VYA KUBADILISHA FEDHA

| FEDHA | KUNUNUA | KUUZA |
|---|---|---|
| KENYA SHS | 22.74 | 22.92 |
| UGANDA SHS | 0.58 | 0.63 |
| RWANDAN FRANC | 2.53 | 2.56 |
| BURUNDI FRANC | 2.18 | 2.20 |
| USD | 2276.68 | 2299.45 |
| POUND STG | 2969.02 | 2999.63 |
| EURO | 2581.99 | 2608.04 |
| CANADIAN $ | 1726.46 | 1743.20 |
| SWITZ. FRANC | 2276.00 | 2298.07 |
| JAPANESE YEN | 20.56 | 20.76 |
| SWEDISH KRONOR | 244.30 | 246.63 |
| NORWEG. KRONOR | 265.25 | 267.75 |
| DANISH KRONOR | 346.06 | 349.49 |
| AUSTRALIAN $ | 1629.19 | 1645.95 |
| INDIAN RPS | 32.00 | 32.31 |
| PAKISTAN RPS | 15.58 | 16.31 |
| ZAMBIAN KWACHA | 189.01 | 192.02 |
| MALAWIAN KWACHA | 2.91 | 3.11 |
| MOZAMBIQUE-MET | 36.20 | 36.50 |
| ZIMBABWE $ | 0.43 | 0.43 |
| SDR | 3158.72 | 3190.30 |
| GOLD (T/O) | 3061250.96 | 3093634.04 |
| S. AFRICAN RAND | 160.71 | 162.26 |
| UAE DIRHAM | 619.86 | 626.04 |
| SINGAPORE $ | 1684.68 | 1701.03 |
| HONK KONG $ | 290.06 | 292.96 |
| SAUD ARABIAN RIAL | 607.08 | 613.10 |
| KUWAIT DINAR | 7500.93 | 7573.20 |
| BOTSWANA PULA | 213.10 | 217.07 |
| CHINESE YUAN | 338.76 | 341.98 |
| MALAYSIA RINGGIT | 560.21 | 564.98 |
| SOUTH KOREA WON | 2.03 | 2.05 |
| NEWZEALAND | 1563.40 | 1579.26 |

## Interbank Foreign Exchange Market (IFEM)

| Tarehe | Idadi (Mn USD) | Juu | Chini | Wastani |
|---|---|---|---|---|
| **20/Feb/2019** | **3.90** | **2,310.00** | **2,297.30** | **2,299.45** |
| 19/Feb/2019 | 4.70 | 2,306.00 | 2,297.25 | 2,297.65 |
| 18/Feb/2019 | 1.55 | 2,307.00 | 2,293.97 | 2,295.23 |
| 15/Feb/2019 | 1.53 | 2,308.50 | 2,293.95 | 2,295.19 |

## Inter-bank Local Money Markets

| Tarehe | Kiasi (million-TZS) | Juu | Chini | Wastani (WAR) |
|---|---|---|---|---|
| **20/Feb/2019** | **23,700** | **4.85** | **4.50** | **4.76** |
| 19/Feb/2019 | 48,800 | 5.00 | 4.50 | 4.60 |
| 18/Feb/2019 | 44,800 | 6.00 | 4.50 | 4.53 |
| 15/Feb/2019 | 25,100 | 5.00 | 4.25 | 4.68 |
| 14/Feb/2019 | 27,900 | 5.20 | 3.00 | 4.76 |
| 13/Feb/2019 | 36,200 | 5.50 | 4.00 | 5.03 |

# Britam Towers: Jumba refu Afrika Mashariki

JUMBA refu la Britam Tower, lililoko jijini Nairobi nchini Kenya, limepokea tuzo inayopewa majumba marefu duniani ya Emporis Skyscraper Award.

Ni jumba la pekee barani Afrika kushiriki katika tuzo hiyo, miongoni mwa majengo 10 bora duniani katika historia ya tuzo hiyo inayofikia miaka 19.

Hatua hiyo, inalifanya jumba hilo lililojengwa na kampuni ya Britam Properties kuwa jumba refu zaidi katika eneo la Afrika Mashariki na Kati, likiwa na kimo cha mita 200. Britam Tower, ilitathminiwa pamoja na mengine mengi ya barani Ulaya, Asia na Marekani, kama vile Generali Tower mjini Milan, jumba la Chicago's 150 North Riverside na Riverpoint.

Nafasi ya kwanza ilichukuliwa na jumba la Lotte World Tower mjini Seoul, Korea Kusini. Tuzo ya The Emporis Skyscraper ni tuzo maarufu duniani miongoni mwa ujenzi wa majumba marefu.

Washindi huchaguliwa na jopo la wataalamu wa usanifu kutoka sehemu mbalimbali za duniani, huku majumba yaliyoteuliwa kuwania tuzo hiyo, yanaposhinda kwa vigezo vya mvuto na ufanisi wao.

Katika eneo la Upper Hill jijini Nairobi, jumba hilo lenye ghorofa 31, linatoa mandhari ya kupendeza kuwezesha kuona maeneo ya kati la mji mkuu wa Nairobi na viunga vyake, ikiwamo mbuga ya wanyamapori ya Nairobi.

Ujenzi wake ulikamilika Novemba 2017 na sasa linamilikiwa na kampuni ya bima ya Britam Life Assurance.

Ni jengo refu ambalo mkazi wake anapokuwa katika upeo wa juu yake, anaweza kuuona Mlima Kilimanjaro na Mlima Kenya. Majumba mengine marefu duniani ni Eiffel Tower lililoko jijini, Paris, Time Warner lililoko New York, Marekani lenye urefu wa mita 200 na Gherkin mjini London, Uingereza lenye urefu wa mita 180.



Awali jumba la Uap, Old Mutual la jijini Nairobi, ndilo lilishikilia nafasi ya jumba refu zaidi Afrika Mashariki likiwa na ghorofa 33 na kimo cha mita 163. Lilikuwa linafuatiwa katika orodha hiyo na Twin Tower jijini Dar es Salaam, lenye ghorofa 35 na urefu wa mita 153.

Hata hivyo, Kenya inatarajiwa kuwa na jumba refu zaidi barani Afrika, baada ya Rais Uhuru Kenyatta, kuweka jiwe la msingi la ujenzi wa ghorofa la Pinnacle Tower.

Jengo hilo litakalojengwa katika eneo la Upper Hill jijini Nairobi, litakuwa na ghorofa 70 na urefu wa futi 900, hivyo basi kulifanya kuwa refu zaidi barani.

Jumba hilo litakuwa na ofisi za kibiashara, nyumba za kukodisha na hoteli, mbali na duka la jumla na kituo cha burudani.

Jumba refu zaidi barani Afrika la Carlton Center, lililoko mjini Johannesburg, nchini Afrika Kusini na limeshika chati hiyo kwa kipindi cha miaka 39 .

Jumba la Pinnacle Towers nchini Kenya, litakuwa miongoni mwa majengo marefu duniani.

Dubai Burj Khalifa, ndio jumba refu zaidi duniani likiwa na urefu wa mita 800. **BBC**





# Mtendaji adaiwa kuchapa viboko wananchi

**Na Nebart Msokwa,** RUNGWE

WANANCHI wa Kata ya Kinyala, Rungwe mkoani Mbeya, wamemlalamikia Ofisa Mtendaji wao, Undule Mwasyonge, kuwa amekuwa akiwadhalilisha kwa kuwacharaza bakora kama watoto wadogo.

Walitoa malalamiko hayo juzi wakati wa shehehe za maadhimisho ya miaka 42 ya kuzaliwa kwa Chama Cha Mapinduzi (CCM), ambayo kwa Wilaya ya Rungwe yalifanyika katika Kijiji cha Igembe na kuhudhuriwa na viongozi mbalimbali.

Kutokana na hali hiyo, wananchi hao waliuomba uongozi wa CCM wilaya kuwasaidia kumwondoa kwa madai kuwa si muungwana na amekuwa akiwacharaza viboko hadharani wanapokuwa na makosa.

Mmoja wa wananchi hao, Lazaro Mwasalwiba, alisema kiongozi huyo amekuwa akitumia vibaya madaraka yake kwa kuacha kuhamasisha maendeleo na badala yake kutumia muda mwingi kuwanyanyasa wananchi anaowaongoza.

Alisema vitendo hivyo vimekuwa vikiwakatisha tamaa, hivyo baadhi kutamani hata kuhamia kata zingine jirani wakimwogopa mtendaji huyo kuwa atawashughulikia.

"Ndugu viongozi tunaomba mtusaidie kumwondoa mtendaji wetu maana kwa muda mrefu amekuwa akituchapa viboko kama watoto wadogo kitu ambacho tunatafsiri kama udhalilishaji maana hata watoto wetu wakati mwingine huwa wanapata taarifa," alisema Mwasalwiba.

Mwenyekiti wa CCM Wilaya ya Rungwe, Sam Mwakapala, alisema alishawahi kupata taarifa za kiongozi huyo kuwanyanyasa wananchi kwa kuwashushia kipigo na akaeleza kuwa alifikiri alishaacha baada ya kutahadharishwa na viongozi.

Alisema kutokana na malalamiko ya wananchi hao, atahakikisha kiongozi huyo anaondoka katika kata hiyo ili wananchi waendelee kufanya shughuli zao kwa amani na utulivu.

Mwakapala alisema chama hicho hakiko tayari kuona wananchi wake wananyanyaswa na mtu kwa namna yoyote, huku akiwataka wananchi hao waendelee kufanya shughuli zao za maendeleo kwa amani wakisubiri hatua zaidi dhidi ya mtendaji huyo.

"Namwagiza Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya, amwondoe mara moja mtendaji huyo na ampeleke sehemu ambayo watakuwa tayari kuchapwa, lakini kwa hapa hatufai tena na atupishe kabisa," alisema Mwakapala.

Alisisitiza kuwa zama hizi si za kupigana na badala yake watu wanamaliza migogoro yao kwa majadiliano ya mezani, huku akidai kuwa hata ng'ombe siku hizi hawachapwi viboko kama anavyowafanyia wananchi ofisa mtendaji huyo.

Naye Katibu wa CCM Wilaya ya Rungwe, Rehema Ndelenzunye, aliwataka wananchi kujitokeza na kushiriki shughuli za maendeleo ikiwamo ujenzi wa vyumba vya madarasa, zahanati, vituo vya afya na miundombinu mingine ya umma.

Alisema watajitokeza kwa wingi, itakuwa rahisi hata wao kujivunia maendeleo pamoja na kuionyesha serikali kuwa wanaiunga mkono katika kutekeleza Ilani ya Uchaguzi ya CCM.



Mkuu wa Kikosi cha Usalama Barabarani Mkoa wa Mbeya, SSP Jumanne Mkwama (wa pili kulia), akimkabidhi cheti mmoja wa madereva waliohudhuria mafunzo ya udereva yanayotolewa na Chuo cha Polisi cha Ufundi Dar es Salaam, katika hafla iliyofanyika jijini Mbeya juzi. **PICHA: NEBART MSOKWA**

## Mamilioni yamwagwa miradi ya maendeleo

**Na Grace Mwakalinga,** MBEYA

HALMASHAURI ya Wilaya ya Mbeya imetoa vifaa vyenye thamani ya Sh. milioni 58 vya ujenzi kutoka kwenye mfuko wa jimbo, lengo likiwa kutekeleza miradi mbalimbali ya maendeleo ambayo imeibuliwa na wananchi. Akizungumza ofisini kwake jana, Ofisa Mipango wa Halmashauri hiyo, Filbert Mbwilo, alisema fedha hizo zimetumika kununua vifaa mbalimbali vya ujenzi vikiwamo mabati, saruji pamoja na nondo na kwamba vitaelekezwa kwenye zahanati, shule na vituo vya afya.

Alitaja maeneo ambayo yatanufaika na fedha hizo kuwa ni kata ya Santilya, Mshewe, Ijombe, Igoma na Igale yataongezewa nguvu baada ya wao kuibua miradi mbalimbali na kuanza kuitekeleza.

"Fedha za mfuko wa jimbo zinatolewa kwa ajili ya kuchochea shughuli za maendeleo ambazo tayari zimekwishaanzishwa na wananchi katika maeneo yao na inapobidi mfuko huo huanzisha miradi mipya. Tunaendelea kuwasisitiza wananchi waendelee kuanzisha miradi ya maendeleo serikali itakuja kuwaunga mkono," alisema Mbwilo. Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri hiyo, Steven Katemba, alisema fedha za mfuko wa jimbo hazitatolewa kwa wananchi ambao hawajitolea kufanya shughuli yoyote ya maendeleo.

Alisema fedha hizo zitapelekwa sehemu ambayo tayari wananchi wameanzisha mradi na kwamba halmashauri nayo kupitia mapato yake ya ndani itawasaidia. Katika hatua nyingine, Katemba alisema halmashauri imetoa mikopo ya zaidi ya Sh. milioni 200 kwa vikundi 15 vya wanawake, vijana na walemavu. Alisema mbali na kutoa mikopo ya fedha kwenye baadhi ya vikundi pia wametoa vifaa kama mashine na pikipiki ili kuwawezesha wananchi kuongeza tija katika uzalishaji wa mazao yao na kurejesha mikopo kwa wakati.

# Chanzo cha ajali madereva 'kenge' na 'nyoka'

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

JESHI la Polisi Kikosi cha Usalama Barabarani mkoani Mbeya, limesema ajali nyingi za barabarani zimekuwa zikitokea na kugharimu maisha ya watu kutokana na madereva 'kenge' na 'nyoka' kuendelea kuendesha vyombo vya moto.

Mkuu wa Kikosi cha Usalama Barabarani wa Mkoa wa Mbeya, Mrakibu Mwandamizi wa Polisi (SSP) Jumanne Mkwama, alisema hayo juzi alipokuwa anafunga programu ya mafunzo ya siku 10 kwa udereva yanayotolewa na Chuo cha Polisi cha Ufundi cha Dar es Salaam kwa madereva wa magari binafsi, bajaji na pikipiki.

Mkwama alisema madereva 'kenge' na 'nyoka' ni wale wasiobadilika kulingana na mazingira ya barabara wanazozitumia kuendesha vyombo vya moto pamoja na kutofuata alama za usalama barabarani.

Alisema Jeshi la Polisi linaendelea kupambana na madereva wa aina hiyo kwa kutoa elimu, kuwatoza faini za papo kwa papo, kuwafungulia mashtaka mahakamani pamoja na kwamba kwa wale wanaokithiri wanapunguziwa madaraja kwenye leseni zao za udereva.

"Tunataka madereva 'vinyonga' yaani wanaoweza kubadilika kulingana na hali ya barabara pamoja na maelekezo ya alama za usalama barabarani. Sasa kwa wale madereva 'kenge' na 'nyoka' tutaendelea kuwapunguzia madaraja ili tutakapofunga leseni zao warudi kutembea kwa miguu au wakaendeshe baiskeli," alisema Mkwama.

Alisema kwa sasa jeshi hilo limeweka mikakati kuwa kuondokana na ajali za barabarani ni lazima na si ombi, hivyo wote wanaosababisha ajali za makusudi wataendelea kushughulikiwa kwa mujibu wa sheria.

Aliwataka madereva walioijitokeza kwenye mafunzo hayo kuzingatia maelekezo waliyoyapata na kwamba wanatakiwa kusoma sheria za usalama barabarani ya mwaka 1973 na pamoja na sheria zingine zinazoendana na hiyo ikiwamo ya vyombo vya moto vyenye magurudumu mawili na matatu ya mwaka 2010.

Alisema Jeshi la Polisi halipendi kukimbizana na madereva wanaovunja sheria za usalama barabarani, lakini huwa inawabidi kutokana na ukorofi wa baadhi ya watu hao, huku akikiri kuwa baadhi ya askari wa usalama barabarani huwa wanawaonea madereva kutokana na ubinadamu.


Mratibu wa mafunzo hayo kutoka katika Chuo cha Ufundi cha Polisi, Edward Mwenisongole, alisema lengo la kutoa mafunzo hayo ni kuwasaidia madereva ambao wanaendesha vyombo vya moto lakini hawakupitia kwenye vyuo vinavyotambuliwa na serikali.

Alisema mafunzo hayo yalianza muda mrefu na kwamba mpaka sasa wameshayatoa kwenye mikoa 15 ya Tanzania Bara ili kupunguza ajali za barabarani ambazo sio za lazima.

Katika mafunzo hayo ya awali madereva waliohitimu walikuwa 110, huku wengi wao waliojitokeza wakiwa madereva wa magari binafsi na 25 pekee.

Alisema mafunzo hayo yanatolewa bila gharama za aina yoyote kwa madereva huku akieleza kuwa wanakusudia kutoa elimu hiyo kwa madereva 3,000 katika Mkoa wa Mbeya pekee.

"Sisi sote ni wadau wa usalama barabarani na ndio maana Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi na Kamanda wa Kikosi cha Usalama Barabarani, waliagiza madereva wote wapatiwe mafunzo," alisema Mwenisongole.





# Watoa msaada kisheria wajadili utoaji wa haki

**Na Augusta Njoji, Dodoma**

WAKUU wa Mashirika yanayojishughulisha na utoaji wa msaada wa kisheria wanakutana Dodoma, kujadili mbinu stahiki za kupanua wigo wa utoaji wa huduma za kisheria nchini, lengo kuu likiwa ni kuwakwamua Watanzania maskini kutoka katika matatizo mbalimbali ya kisheria na kuwasaidia kupata haki zao.

Kongamano hilo linawakutanisha pamoja wakurugenzi na wajumbe wa bodi kutoka katika mashirika ya msaada wa kisheria yanayotekeleza miradi ya huduma za kisheria maeneo mbalimbali nchini chini ya ufadhili wa Shirika la Legal Services Facility (LSF).

"Mkutano huu unatoa fursa kwa wadau wa utoaji wa huduma za kisheria, hasa wale wanafadhiliwa na LSF, kujadili mafanikio, changamoto mbalimbali na njia bora za katika utoaji wa huduma za kisheria na namna na kufikisha huduma za kisheria kwa Watanzania wengi wahitaji, hasa waishio vijijini," alisema Meneja Mradi wa LSF, Ramadhan Maselle, wakati wa ufunguzi mkutano huo.

"Kwa mwaka 2018 tumeweza kufikia watu zaidi ya milioni tatu kulinganisha na mwaka 2017, ambapo watu milioni 1,400,000 walifikiwa katika kupata elimu ya sheria.

"Na kwa upande wa msaada wa kisheria mwaka 2018 tulifikia watu 76,000 kulinganisha na mwaka 2017, ambapo 65,000 walifikiwa hivyo ni wazi kabisa kumekuwa na ongezeko katika kuwafikia na kubadili mtazamo, maisha ya wananchi kwa kuwawezesha kupata stahiki zao kwa maendeleo bora ya kijamii na kiuchumi kila mwaka," alisema. Lengo kuu la kongamano hilo kwa mujibu wa Maselle ni kuhakikisha huduma za kisheria na wasaidizi wa kisheria zinawafikia Watanzania wengi wenye matatizo ya kisheria, mpaka chini kabisa katika ngazi za vijiji.

Washiriki wa mkutano pia watapata nafasi kujadili kwa mapana na marefu miradi ya LSF, mbinu za kufanya miradi/shughuli inayotekelezwa na vituo vya msaada wa kisheria, mashirika na wadau mbalimbali chini ya ufadhili wa LSF iwe endelevu.

"Mijadala na mikakati utokanayo na mkutano huu yataisaidia LSF, mashirika yanayofadhiliwa na LSF na wadau wengine kupata uelewa mpana kuhusu mbinu mbadala zitakazosaidia kupata fedha na raslimali fedha kutoka katika vyanzo mbalimbali mbadala kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya usaidizi wa kisheria na hatimaye kuwakwamua Watanzania maskini kutoka katika matatizo mbalimbali ya kisheria yanayowakabili," alisisitiza Masele.

Aidha, katika kongamano, LSF itatoa vyeti vya utendaji bora kwa vituo vinane vya watoa huduma za msaada wa kisheria ambao wamefanya vizuri mwaka 2018, ambavyo ni pamoja na Kibondo Kigoma, Makete Njombe, Katuka Dodoma, Toje Tanga, Kyela Mbeya, Ukerewe Mwanza, Serengeti Mara na Micheweni Zanzibar.

Mkutano huo unatarajia kuhudhuriwa na washiriki 106, ikiwa ni pamoja na viongozi wa mashirika yanayofadhiliwa na LSF, wajumbe wa bodi wa mashirika husika, viongozi wa serikali kutoka katika wizara mbalimbali kama Tamisemi, Wizara ya Sheria na Katiba, Wizara ya Afya, Wizara ya Ardhi na waandishi wa habari.




Meneja Uwezeshaji wa Shirika la Legal Aid Facility (LSF), Bryceson Munuo, akizungumza mjini Dodoma na wakuu wa bodi na mashirika yanayotoa huduma za msaada wa kisheria yanayofadhiliwa na LSF, katika mkutano wa mwanzo wa mwaka unaowakutanisha washiriki kutoka katika mikoa yote ya Tanzania Bara na Zanzibar. **PICHA: IBRAHIM JOSEPH**

# Bodaboda walalamikiwa kuwarubuni wanafunzi

**Na Augusta Njoji,** MPWAPWA

IMEELEZWA kuwa kukosekana kwa uzio katika Shule ya Sekondari ya Wasichana ya Mazae iliyoko Wilaya ya Mpwapwa mkoani Dodoma, kumesababisha wanafunzi hao kurubuniwa na vijana wanaoendesha bodaboda.

Hayo yalisemwa jana wilayani humo na Mwenyekiti wa bodi ya shule hiyo, Leo Mzeru, wakati akizungumza kwenye mafunzo ya kuwajengea uwezo walimu na wenyeviti wa bodi za shule namna ya kuwalinda wanafunzi na aina zote za ukatili wanapokuwa shuleni. Mafunzo hayo yaliandaliwa na shirika lisilo la kiserikali la Utu wa Mtoto (CDF) chini ya mradi wa Foundation for Local Initiative (CFIL) kutoka nchini Canada.

Mzeru alisema hali hiyo inahatarisha usalama na ulinzi wa watoto hao na wanaweza kujikuta wakipata mimba za utotoni na kwamba vijana wanaoendesha bodaboda wamekuwa wakiwarubuni wasichana hao kwa kuwa hakuna uzio unaowazuia kuingia shuleni hapo.

"Hili la kukosa uzio sio geni, tumekuwa tukipiga kelele mara kwa mara, lakini mamlaka husika hazichukui hatua yoyote ya kujenga uzio huo wakati wanajua kuwa shule hii iko mbugani," alisema. Alisema shule hiyo ni ya kitaifa na ina wanafunzi wa kuanzia kidato cha kwanza hadi cha sita, lakini haina uzio. "Sasa ukiwaweka wasichana wenye umri wa miaka 17 hadi 19 mahali ambapo hakuna uzio ni hatari sana, kwa sababu hawa wasichana wako kwenye umri wa balehe," alisema na kuongeza.

"Kukosekana kwa uzio huo kunahatarisha hali ya ulinzi na usalama kwa watoto hao hasa wa kidato cha tano na sita wanaoishi mabwenini kwa sababu huibiwa hadi nguo zao wanazoanika nje na wanakijiji," alisema. Alisisitiza kuwa Halmashauri ya Wilaya ya Mpwapwa haipaswi kupuuza ombi la bodi hiyo la kujenga uzio katika shule hiyo, kwa sababu ni muhimu kwan kuwa shule hiyo iko mbugani na chochote kinaweza kutokea wakati wowote. Naye Mkuu wa shule hiyo, Consolata Shangaluka, alisema ingawa shule hiyo ina walinzi wanaolinda, lakini kuwapo kwa nyumba za walimu ni muhimu kwa sababu ya dharura zinazoweza kujitokeza usiku wa manane.

Alisema shule hiyo haina nyumba ya walimu hata moja iliyopo karibu kwasababu walimu wote wanaishi mbali na shule kutokana na kukosekana kwa nyumba za walimu shuleni hapo.

Kwa upande wake, Meneja Miradi wa Shirika la CDF, Evance Rwamuhuru, alisema wameamua kutoa mafunzo hayo kwa walimu na wenyeviti wa bodi za shule baada ya kuona kuna ukatili wa aina mbalimbali unaoendelea katika mazingira ya shule.

# Vyama vya ushirika zaidi ya 2,000 vyasajiliwa

**Na Ibrahim Joseph,** DODOMA

VYAMA vya Ushirika 2,377 vimesajiliwa ndani ya kipindi cha miaka minne kuanzia mwaka 2015 hadi Septemba 2018.

Hayo yalisemwa jana na mrajisi ambaye pia ni Mtendaji Mkuu wa Tume ya Maendeleo ya Ushirika Tanzania, Tito Haule, katika taarifa yake aliyoitoa kwa vyombo vya habari jijini hapa.

Haule alisema vyama hivyo vimesajiliwa baada ya tume hiyo na wadau wengine kutoa elimu kwa wananchi kuhusu umuhimu wa ushirika.

"Kufuatia uhamasishaji uliofanywa na tume pamoja na wadau wengine wa ushirika kutoa elimu kwa makundi mbalimbali ya kijamii nchini vyama vya ushirika 2,377 vimesajiliwa,"alisema.

Aidha, alisema tume hiyo iliratibu mafunzo kwa viongozi 190,watendaji 407, na maofisa ushirika 100 katika nyanja mbalimbali ikiwamo ufungaji wa vitabu vya hesabu za vyama vya ushirika.

Alisema katika mafunzo hayo wahusika walifundishwa majukumu ya wajumbe wa bodi, utatuzi wa migogoro, mikataba na ajira, haki, wajibu na maadili ya viongozi, sheria usimamizi na uendeshaji wa vyama vya ushirika.

Alibainisha kuwa matokeo ya utoaji elimu hiyo ilisaidia utendaji wa viongozi hao wa vyama vya ushirika nchini kuimarika zaidi katika utendaji wao.

Kadhalika, mrajisi huyo alisema kutokana na kuimarika kwa usimamizi wa vyama hivyo na matumizi ya mifumo ya kimasoko, imechangia kuboresha mfumo wa uuzaji na ushindani wa mazao ya kimkakati na mazao mengine ya kibiashara ikiwamo kakao, ufuta na miwa.

# DRC yakunwa na miradi ya Tasaf

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

NAIBU Katibu Mkuu Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais, Abdallah Hassan Mitawi, amesema ni faraja kwa nchi zingine kufika Zanzibar kujifunza inavyosimamia miradi yake ikiwamo inayotekelezwa na Mfuko wa Maendeleo ya Jamii (Tasaf).

Mitawi alisema hayo jana alipokuwa akizungumza na waandishi wa habari baada ya kuzungumza na ujumbe kutoka Jamhuri yua Kidemokrasi ya Congo (DRC) ambao umefika Zanzibar kujifunza mambo mbalimbali katika miradi ya mfuko huo. Alisema ujumbe huo umeletwa na Benki ya Dunia kujifunza Tasaf inavyofanya kazi, hivyo kuendelea kupata sifa kimataifa. Kwa mujibu wa Mitawi, Tasaf imeleta matokeo chanya katika kupunguza umaskini kutokana na walengwa kuendesha shughuli mbalimbali za maendeleo na kujikwamua na umaskini.

Pia alisema Tasaf imesaidia kuwakutanisha wananchi bila ya kujali itikadi zao za kisiasa tofauti na miaka ya nyuma. Alisema wakati huo kulikuwa na watu wenye mitazamo tofauti na kushindwa kukaa pamoja kufanya kazi.

Naye mkuu wa msafara wa timu hiyo, Adolphe Mpwa Idole, alisema wamefarijika kuona jinsi utekelezaji wa miradi ya Tasaf na kuzungumza na walengwa wa mradi huo ambao baadhi yao wamepiga hatua kubwa ya maendeleo. Alisema wamejifunza mambo mengi kupitia mradi huo na imekuwa fundisho kwao kutokana na mambo mbalimbali waliyoyaona ikiwamo miradi ya kijamii katika kujikomboa kiuchumi na kuondokana na umaskini.

Nao walengwa wa Tasaf walisema hali zao za kiuchumi hivi sasa zimeimarika baada ya kuwezeshwa na kubuni miradi mbalimbali ya kimaendeleo kwa lengo la kujikomboa na umaskini.

Fatma Daudi Haji, mmoja wa walengwa hao kutoka kijiji cha Mtende Mkoa wa Kusini Unguja, alisema baada ya kuwezeshwa na Tasaf hivi sasa amejikita katika ufugaji wa kuku wa kienyeji na anafanya biashara ndogo ndogo ambazo zinamsaidia kupata kipato.

"Nashukuru biashara yangu ya kuuza maandazi inanisaidia na pia nafuga kuku. Fedha ninazozipata zimekuwa zikinisaidia kuhudumia watoto wangu kwa ajili ya chakula na mahitaji mingine ya shule," alisema. Ujumbe kutoka Congo ulitembelea miradi ya upandaji wa miti aina ya mivinje na mikoko, ufugaji wa samaki na bwawa la kuhifadhia maji ya mvua kwa ajili ya kilimo na ufugaji.



Mkurugenzi Mkuu wa Mamlaka ya Maji Zanzibar (ZAWA), Mussa Ramadhan Haji (kulia), akitoa maelezo ya uimarishaji wa huduma ya majisafi na salama katika Miradi ya Usambazaji wa Maji, Wilaya ya Kusini Unguja, wakati wa majumuisho ya ziara ya Rais wa Zanzibar, Dk. Ali Mohamed Shein, juzi. **PICHA: IKULU ZANZIBAR**

# Wakabiliwa na changamoto ya elimu

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

LICHA ya Serikali ya Zanzibar kuimarisha sekta ya elimu na kuhakikisha elimu ya msingi hadi sekondari inatolewa bure, imebainika kuwa kumekuwa na changamoto nyingi katika upatikanaji wa huduma hiyo hasa kwa watoto wanaoishi katika mazingira magumu.

Mkuu wa Utawala na Rasilimali Watu wa Kijiji cha Kulelea Watoto Yatima na Wanaoishi katika Mazingira Magumu (SOS), Salum Abrahman, alisema hayo jana katika kikao cha pamoja cha kamati za shule zilizomo katika mradi wa Boresha Familia katika Kijiji cha SOS Zanzibar.

Alisema wamegundua watoto wanaowasaidia ambao wako nje ya kijiji cha SOS, maendeleo yao ya kielimu si mazuri kuliko wale wanaolelewa katika kijiji.

Wanafunzi hao, alisema ufaulu wao si mzuri kutokana na changamoto nyingi zilizoko shuleni ikiwamo idadi kubwa ya wanafunzi madarasani hali inayosababisha kushindwa kufahamu kile ambacho amefundishwa na mwalimu shuleni.

"Tusipojenga msingi bora na imara wa elimu kwa watoto wetu, mwisho wa siku tutajenga ukuta badala ya kuziba ufa," alisema Abraham. Wakizungumza katika kikao hicho, walimu wa shule za msingi na sekondari za Wilaya ya Magharibi 'A', walisema miundombinu ya upatikanaji wa elimu si rafiki kwa wanafunzi shuleni.

Walisema hali hiyo inasababisha ufaulu mdogo na Zanzibar kuwa miongoni mwa shule zinazofanya vibaya katika mitihani ya taifa ya kidato cha nne na sita.

"Tunamshukuru Rais wetu kutangaza elimu bure, lakini hivi sasa tumekuwa

na changamoto kubwa kama vile uhaba wa fedha shuleni na hatuna vifaa zikiwamo mashine za kuchapishia mitihani. Fedha ambazo walizokuwa wakichangia wanafunzi, zilikuwa zikisaidia katika kuwaandaa wanafunzi na mitihani ya majaribio," alisema mmoja wa walimu hao (jina linahifadhiwa).

Walimu hao walisema idadi kubwa ya wanafunzishuleni kulinganisha na vyumba vya madarasa na uhaba wa madawati pia ni changamoto inayokabili sekta ya elimu na imesababisha wanafunzi kukaa chini.

"Darasa moja lina wanafunzi 150 na chumba kimoja kina madawati sita tu, vyumba vyenyewe vinavuja inabidi inaponyesha mvua watoto tunawaruhusu warudi nyumbani kwao kwa sababu hatuna sehemu ya kuwaweka," aliongeza.

Changamoto nyingine, kwa mujibu wa walimu hao ni wanafunzi kutozingatia masomo, hali ngumu ya familia kwa baadhi ya wanafunzi na kutokuwa na ushirikiano kati ya wazazi na walimu.

Walisema wazazi wengi hawafuatilii maendeleo ya watoto wao hata wanapoitwa shuleni hushindwa kufika kutokana na kutingwa na shughuli za kutafuta kipato.

# Wakulima wa mwani wajawa matumaini

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

RAIS wa Zanzibar, Dk. Ali Mohamed Shein, amewataka wakulima wa mwani hasa kinamama kuwa na subira wakati serikali yao ikitafuta mwarobaini wa bei ya zao hilo.

Mbali na suala la bei, Dk. Shein, pia amesema serikali ina mpango wa kujenga kiwanda cha mwani hali ambayo itapaisha bei ya zao hilo.

Dk. Shein aliyasema hayo jana, wakati akizungumza na viongozi wa CCM wa Wilaya ya Kusini Unguja na kufanya majumuisho ya ziara yake kwa wilaya hiyo.

Alisema anaelewa kuwa bei ya mwani imekuwa changamoto kubwa na tangu alipoingia madarakani, amekuwa akilifanyia kazi suala hilo, lakini sasa limepata mwarobaini wake. Kwa mujibu wa Dk. Shein, serikali yake imeshafanya mazungumzo na kampuni kubwa ya mwani ya Indonesia na wameshakubaliana kujenga kiwanda kikubwa cha kuongeza thamani ya zao hilo Zanzibar.

Alisema kuwa hatua hiyo imekuja baada ya ziara yake aliyoifanya nchini humo mwishoni mwaka jana. Alisema katika ziara hiyo alikutana na viongozi wa wafanyabiashara wa zao hilo na kukubaliana kuanzisha ushirikiano jambo ambalo linakwenda vizuri na hatua iliyobaki ni kutia saini makubaliano ya ushirikiano huo ili kuanza mchakato.

Kufanikisha suala hilo, alisema kutasaidia kwa kiasi kikubwa kupanda chati zao la mwani katika visiwa vya Zanzibar na kusababisha wakulima kufaidika na kilimo hicho kwa kuwa bei itakuwa juu na kusaidia kuimarisha pato la wakulima na pato la serikali.

Aidha, Rais Dk. Shein, aliwahakikishia wananchi wa majimbo ya Paje na Makunduchi kuwa uhaba wa maji safi na salama unatafutiwa ufumbuzi na muda si mrefu litakuwa historia.

# RATIBA

## CAPITAL TELEVISION

**Mon 18 Feb**
06:00 Al jazera
08:00 CNN International News
09:00 Al Jazeera
10:00 Kumekucha
10:30 Kumekucha Michezo
11:30 Kumekucha Kishindo
12:00 Turning the spotlight rpt:
12:30 Drive it rpt
13:00 Series rpt : Grapes of justice
13:45 Series rpt: Ode To Joy
14:30 Usafiri wako rpt
15:00 Cookery rpt: Culinary Delight
15:30 Toyota world of wildlife rpt
16:00 CNN International
17:00 Eco@Africa rpt
17:30 Meza huru
19:00 The Décor rpt
19:30 Business edition
20:00 Series: Grapes of Justice
20:45 The Monday Agenda
21:30 Capital Prime News
22:00 Kipima Joto
00:00 Al Jazeera

**Tues 19 Feb**
06:00 Al Jazeera
08:00 CNN International News
09:00 Al Jazeera
10:00 Kumekucha
10:30 Kumekucha Michezo
11:30 Kumekucha Kishindo
12:00 The Decor rpt
12:30 Mizengwe rpt
12:45 Aibu Yako
13:00 Series rpt: Grapes of justice
13:45 Series rpt: Ode To Joy
14:15 Local pgm rpt: Business Edition
15:00 Bundesliga kick off
15:30 Out and About rpt
16:00 Capchat rpt
17:00 Ripoti Maalum rpt
17:30 Meza huru
19:00 Innovation
19:30 Ripoti Maalum
20:00 Series: Grapes of Justice
20:45 Series: Ode To Joy
21:30 Capital Prime
22:00 Turning the Spotlight rpt
22:30 Iron Chef rpt
23:30 Al Jazeera

**Wed 20 Feb**
06:00 Al jazeera
08:00 CNN International News
06:00 Al Jazeera
08:00 CNN International News
09:00 Al Jazeera
10:00 Kumekucha
10:30 Kumekucha Michezo
11:30 Kumekucha Kishindo
12:00 Turning the Spotlight rpt
12:30 Culinary delight rpt
13:00 Series rpt: Grapes of Justice
13:45 Series rpt: Ode To Joy
14:30 Local Pgm: The Monday Agenda Rpt
15:15 Capchat rpt
16:15 CNN International
17:00 Innovation rpt
17:30 Meza Huru
19:00 Sports Gazette
19:30 Business edition rpt
20:00 Series: Grapes of Justice
20:45 Series: Ode To Joy
21:30 Capital Prime News
22:00 Dakika 45:
22:45 The Décor
23:15 Al Jazeera

**Thurs 21 Feb**
06:00 Al Jazeera
08:00 CNN International News
09:00 Al Jazeera
10:00 Kumekucha
10:30 Kumekucha Michezo
11:30 Kumekucha Kishindo
12:00 Sports Gazette
12:30 Out n' about rpt:
13:00 Series rpt: Grapes of Justice
13:45 Series rpt: Ode To Joy
14:30 Business Edition rpt
15:00 Korean Drama rpt: Emperor of the sea
16:00 Dakika 45 rpt
17:00 In good shape
17:30 Meza Huru
19:00 Turning the spotlight
19;30 Usafiri wako
20:00 Series: Grapes of Justice
20:45 Series: Ode To Joy
21:30 Capital Prime News
22:00 Capchat rpt
23:00 Al Jazeera

**Frid 22 Feb**
06:00 Al Jazeera
08:00 CNN International News
09:00 Al Jazeera
10:00 Kumekucha
10:30 Kumekucha Michezo
11:30 Kumekucha Kishindo
12:00 Innovation rpt
12:30 The Decor rpt
13:00 Series rpt: Grapes of Justice
13:45 Series rpt: Ode To Joy
14:30 Ripoti Maalum rpt
15:00 Korean Dram rpt: Emperor of the sea
16:00 CNN International
16:30 The Monday Agenda rpt
17:30 Meza Huru
19:00 Drive it
19:30 Eco@Africa
20:00 Aibu yako
20:15 Local Pgm: Business Edition
20:45 Series: Ode To Joy
21:30 Capital Prime News
22:00 Malumbano ya hoja rpt
00:00 Al Jazeera

**Sat 23 Feb**
08:00 CNN International
09:00 Drive It rpt
09:30 Turning the Spotlight rpt
10:00 Culinary delight rpt
10:30 Innovation rpt
11:00 Out n'about rpt
11:30 Sports Gazette rpt
12:00 Usafiri wako rpt
12:30 Eco@Africa rpt
13:00 Business edition rpt
13:30 Korean Drama rpt: Emperor of the sea
14:30 Telenovela rpt: Ode To Joy
17:15 Ripoti Maaalum rpt
17:45 Bundesliga kick off
18:15 Capchat rpt
19:15 Mizengwe
19:30 The Decor
20:00 Iron Chef.
21:00 Out n' about
21:30 Movie: Delirious
23:00 Grapes of Justice rpt
01:00 Al Jazeera

**Sun 24 Feb**
08:00 CNN International
09:00 In good shape
10:00 Capchat rpt
11:00 Sports Gazette rpt
11:30 Iron chef rpt
12:00 Out n about rpt
12:30 Bundesligga Kick Off rpt
13:00 Ripoti Maalum
13:30 Series rpt: Grapes of Justice
15:15 Aibu yako
15:30 Drive it rpt
16:00 Dakika 45 rpt
16:45 Mizengwe rpt
17:00 The Decor rpt
17:30 Meza huru
19:00 Turning the Spotlight rpt
19:30 Cookery pgm:Culinary Delights
20:00 Korean Drama rpt: Emperor of the sea
21:00 Shift
21:15 Capchat live
22:15 Telenovela: Ode To Joy
00:00 Al Jazeera

## ITV Daima WEEKLY-SCHEDULE

**MONDAY 18 Feb**
05:30 Uwanja wa Mazoezi
06:00 Habari
06:40 Kumekucha
07:30 HABARI
08:00 Kumekucha Michezo
08:55 Habari za saa
09:00 Kumekucha Kishindo
09:30 Isidingo
09:55 Habari za saa
10:00 Watoto wetu
10:30 Igizo: Hatua
10:55 Habari za saa
11:00 Kimya Milele
11:55 Habari za saa
12:00 Al Jazeera
12:30 Jungu kuu rpt
12:55 Habari za saa
13:00 Mjue Zaidi
13:55 Habari za saa
14:00 Telenovela: Destiny (Destino)
14:55 Habari za saa
15:00 Meza Huru
16:30 Watoto Wetu
17:00 The Base
18:00 Jiji Letu
18:10 Aibu yako rpt
18:15 Huduma ya kwanza
18:30 Shamba shape up
19:00 Afya ya Jamii
19:30 Isidingo
20:00 Habari
21:05 Dakika 45
22:00 Telenovela: Destiny (Destino)
23:00 Habari
23:30 The Base
00:30 Al Jazeera
02:00 CNN International

**TUESDAY 19 Feb**
05:30 Uwanja wa Mazoezi
06:00 Habari
06:40 Kumekucha
07:30 HABARI
08:00 Kumekucha Michezo
08:55 Habari za saa
09:00 Kumekucha Kishindo
09:30 Isidingo
09:55 Habari za saa
10:00 Watoto wetu
10:30 Hawavumi lakini wamo
10:55 Habari za saa
11:00 Hawavumi lakini wamo
11:15 Igizo: Mtego
11:55 Habari za saa
12:00 Al Jazeera
12:30 Afya ya jamii rpt
12:55 Habari za saa
13:00 Uchumi na biashara
13:30 Kipindi Maalum rpt : TFDA
13:55 Habari za saa
14:00 Huduma ya kwanza
14:15 Telenovela: Destiny (Destino) rpt:
14:55 Habari za saa
15:00 Meza Huru
16:30 Watoto wetu
17:00 The Base
18:00 Jiji Letu
18:15 Korean drama rpt: The Great Queen Seonduk
19:00 Jarida la wanawake
19:30 Isidingo
20:00 Habari
21:00 Kipindi maalum:
22:15 Telenovela: Destiny (Destino)
23:00 Habari
23:30 The Base
00:30 CNN International

**WEDNESDAY 20 Feb**
05:30 Uwanja wa Mazoezi
06:00 HABARI
06:40 Kumekucha
07:30 HABARI
08:00 Kumekucha Michezo
08:55 Habari za saa
09:00 Kumekucha Kishindo
09:30 Isidingo
09:55 Habari za saa
10:00 Watoto wetu
10:30 Shamba shape up
10:55 Habari za saa
11:00 Korean: The Great Queen Seonduk
11:55 Habari za saa
12:00 Al Jazeera
12:30 Jarida la wanawake rpt
12:55 Habari za saa
13:00 Dakika 45
13:55 Habari za saa
14:00 Telenovela rpt: Destiny (Destino):
14:55 Habari za saa
15:00 Meza Huru
16:30 Watoto Wetu
17:00 The Base
18:00 Jiji Letu
18:15 Mapishi rpt
18:30 Ijue Sheria
19:00 Kipindi Maalum: TFDA
19:30 Isidingo
20:00 Habari
21:00 Aibu Yako! Hata wewe?
21:10 Kipindi Maalum : Tanesco
21:40 Kipindi Maalum:
22:15 Telenovela: Destiny (Destino)
23:00 Habari
23:30 The Base
00:30 Al Jazeera
02:00 CNN International

**THURSDAY 21 Feb**
05:30 Uwanja wa Mazoezi
06:00 HABARI
06:40 Kumekucha
07:30 HABARI
08:00 Kumekucha Michezo
08:55 Habari za saa
09:00 Kumekucha Kishindo
09:30 Isidingo
09:55 Habari za saa
10:00 Watoto wetu
10:30 Igizo: Hatua
10:55 Habari za saa
11:00 Igizo: Hatua
11:15 Usafiri wako
11:55 Habari za saa
12:00 Al jazeera
12:30 Ijue Sheria
12:55 Habari za saa
13:00 Sanaa na wasanii rpt
13:30 Jungu Kuu
13:55 Habari za saa
14:00 Telenovela rpt: Destiny (Destino)
14:55 Habari za saa
15:00 Meza Huru
16:30 Watoto Wetu
17:00 The Base
18:00 Jiji Letu
18:15 Huduma ya kwanza rpt
18:30 Kipindi Maalum: Ewura
19:00 Usafiri wako
19:30 Isidingo
20:00 Habari
21:00 Malumbano ya hoja
23:00 Habari
23:30 The Base
00:30 CNN International

**FRIDAY 22 Feb**
05:30 Uwanja wa Mazoezi
06:00 HABARI
06:40 Kumekucha
07:30 HABARI
08:00 Kumekucha Michezo
08:55 Habari za saa
09:00 Kumekucha Kishindo
09:30 Isidingo
09:55 Habari za saa
10:00 Watoto wetu
10:30 Hawavumi lakini wamo
10:55 Habari za saa
11:00 Hawavumi lakini wamo
11:20 Usafiri wako
11:55 Habari za saa
12:00 Al Jazeera
12:30 Kipindi Maalum rpt: TCRA
12:55 Habari za saa
13:00 Kipindi maalum: Tanesco
13:30 Kipindi Maalum rpt - Ewura
13:55 Habari za saa
14:00 Mapishi
14:15 Telenovela rpt: Destiny (Destino)
14:55 Habari za saa
15:00 Meza huru
16:30 Watoto wetu
17:00 The Base
17:30 Ibada ya kiislamu
18:00 Jiji Letu
18:15 Igizo: Mizengwe
18:30 Uchumi na biashara
19:00 Kipindi maalum: TCRA
19:30 Isidingo
20:00 Habari
21:05 Kipima joto
23:00 Habari
23:30 The Base
00:30 CNN International

**SATURDAY 23 Feb**
05:30 Uwanja wa Mazoezi
06:00 HABARI
06:40 Kumekucha
07:00 Habari
08:00 Al Jazeera
09:00 Watoto wetu
10:00 Mjue Zaidi rpt
11:00 Jungu kuu rpt
11:30 Usafiri wako
12:00 Shamba Shape up
12:30 Telenovela rpt: Destiny (Destino)
14:45 Igizo rpt: Riziki
15:15 Igizo rpt: Hatua
15:45 Igizo rpt: Mizengwe
16:00 Igizo rpt: Kimya Milele
16:30 Igizo: Mtego rpt
17:00 Shamsham za Pwani
18:00 Jiji Letu
18:15 Mapishi
18:30 Igizo: Riziki
19:00 Sanaa na wasanii
19:30 Jungu Kuu
20:00 Habari
21:00 Igizo: Kimya Milele
21:30 Hawavumi lakini wamo
22:30 Isidingo rpt
01:00 CNN International

**SUNDAY 24 Feb**
05:30 Uwanja wa Mazoezi
06:00 HABARI
06:40 Kumekucha
07:00 Habari
08:00 Al jazeera
09:00 Watoto Wetu
10:00 Isidingo
11:45 Aibu Yako
11:50 Hawavumi lakini wamo rpt
12:50 Bongo Movie rpt: Green Light 2
14:00 Tamasha la Michezo
15:00 Mwangaza
16:00 Korean drama: The great queen Seonduk
16:45 Mjue zaidi
17:30 Kipindi cha kikristo
18:00 Jiji Letu
18:15 Mapishi
18:30 Mizengwe rpt
18:45 Matukio ya wiki
19:30 Igizo: Mtego
20:00 Habari
21:05 Mizengwe
21:00 Bongo Movie: Kisasi cha utata
22:00 Telenovela rpt: Destiny (Destino)









## RADIO One WEEKLY-SCHEDULE

| TIME | MONDAY PROGRAMME |
|---|---|
| 05.00 AM | HALI YA HEWA / KUMEPAMBAZUKA |
| 06.00 AM | AMKA NA BBC |
| 06.30 AM | NIPASHE |
| 06.50 AM | MATANGAZO |
| 07.00 AM | NEWS BULLETIN |
| 7:10 AM | MATANGAZO |
| 07.15 AM | TAARIFA ZA BARABARANI |
| 07.25 AM | UDONDOZI WA MAGAZETI |
| 07.40 AM | KUMEPAMBAZUKA II |
| 08.00 AM | HABARI NYEPESI |
| 08.10 AM | KUMEPAMBAZUKA III |
| 09.00 AM | HABARI ZA BIASHARA |
| 09.10 AM | MATANGAZO |
| 09.20 AM | BRAND TALK |
| 10.00 AM | NEWS BRIEF |
| 10.03 AM | DEATH ANNOUNCEMENTS |
| 10.10 AM | YALIYOMO YAMO |
| 13.00 HRS | NEWS BULLETIN |
| 13.10 HRS | DEATH ANNOUNCEMENTS |
| 13:30 HRS | DJ SHOW |
| 16.00 HRS | NEWS BRIEF |
| 16.03 HRS | DEATH ANNOUNCEMENTS |
| 16.30 HRS | HOJA YA LEO |
| 18.30 HRS | DIRA YA DUNIA BBC |
| 19.30 HRS | SPOTI LEO |
| 20.00 HRS | NEWS BULLETIN |
| 20.10 HRS | RADIO ONE DOCTOR |
| 21.00 HRS | NEWS BRIEF |
| 21.05 HRS | DAKIKA 45 |
| 22.00 HRS | NEWS BULLETIN (24 HRS) |
| 22.15 HRS | AFRO TIZII |
| 23.00 HRS | NEWS BRIEF |
| 23.03 HRS | AFRO TIZII |
| 01:00 -03:00HRS | YALIYOMO YAMO ( MARUDIO ) |
| 03:00 - 05:00HRS | DK 45 ( MARUDIO ) |
| 23.00 HRS | |

| TIME | TUESDAY PROGRAMME |
|---|---|
| 05.00 AM | HALI YA HEWA / KUMEPAMBAZUKA I |
| 06.00 AM | AMKA NA BBC |
| 06.30 AM | NIPASHE |
| 06.50 AM | MATANGAZO |
| 07.00 AM | NEWS BULLETIN |
| 7:10 AM | MATANGAZO |
| 07.15 AM | TAARIFA ZA BARABARANI |
| 07.25 AM | UDONDOZI WA MAGAZETI |
| 07.40 AM | KUMEPAMBAZUKA II |
| 08.00 AM | HABARI NYEPESI |
| 08.10 AM | KUMEPAMBAZUKA III |
| 09.00 AM | HABARI ZA BIASHARA |
| 09.10 AM | MATANGAZO |
| 09.20 AM | BRAND TALK |
| 09.30 AM | KUMEPAMBAZUKA SHERIA |
| 10.00 AM | NEWS BRIEF |
| 10.03 AM | DEATH ANNOUNCEMENTS |
| 10.10 AM | YALIYOMO YAMO |
| 13.00 HRS | NEWS BULLETIN |
| 13.10 HRS | DEATH ANNOUNCEMENTS |
| 13:30 HRS | DJ SHOW |
| 16.00 HRS | NEWS BRIEF |
| 16.03 HRS | DEATH ANNOUNCEMENTS |
| 16.30 HRS | HOJA YA LEO |
| 18.30 HRS | DIRA YA DUNIA BBC |
| 19.30 HRS | SPOTI LEO |
| 20.00 HRS | NEWS BULLETIN |
| 20.10 HRS | UCHUNGUZI KAMILI |
| 21.00 HRS | NEWS BRIEF |
| 21.05 HRS | DURU ZETU |
| 22.00 HRS | NEWS BULLETIN (24 HRS) |
| 22.15 HRS | AFRO TIZII |
| 23.00 HRS | NEWS BRIEF |
| 23.03 HRS | AFRO TIZII |
| 01:00 - 03:00HRS | YALIYOMO YAMO ( MARUDIO ) |
| 03:00 - 05:00HRS | HOJA YA LEO ( MARUDIO ) |

| TIME | WEDNESDAY PROGRAMME |
|---|---|
| 05.00 AM | HALI YA HEWA / KUMEPAMBAZUKA I |
| 06.00 AM | AMKA NA BBC |
| 06.30 AM | NIPASHE |
| 06.50 AM | MATANGAZO |
| 07.00 AM | NEWS BULLETIN |
| 7:10 AM | MATANGAZO |
| 07.15 AM | TAARIFA ZA BARABARANI |
| 07.25 AM | UDONDOZI WA MAGAZETI |
| 07.40 AM | KUMEPAMBAZUKA II |
| 08.00 AM | HABARI NYEPESI |
| 08.10 AM | KUMEPAMBAZUKA III |
| 09.00 AM | HABARI ZA BIASHARA |
| 09.10 AM | MATANGAZO |
| 09.20 AM | BRAND TALK |
| 09.30 AM | KUMEPAMBAZUKA MICHEZO |
| 10.00 AM | NEWS BRIEF |
| 10.03 AM | DEATH ANNOUNCEMENTS |
| 10.10 AM | YALIYOMO YAMO |
| 13.00 HRS | NEWS BULLETIN |
| 13.10 HRS | DEATH ANNOUNCEMENTS |
| 13:30 HRS | DJ SHOW |
| 16.00 HRS | NEWS BRIEF |
| 16.03 HRS | DEATH ANNOUNCEMENTS |
| 16.30 HRS | HOJA YA LEO |
| 18.30 HRS | DIRA YA DUNIA BBC |
| 19.30 HRS | SPOTI LEO |
| 20.00 HRS | NEWS BULLETIN |
| 20.10 HRS | UCHUNGUZI KAMILI |
| 21.00 HRS | NEWS BRIEF |
| 21.05 HRS | DURU ZETU |
| 22.00 HRS | NEWS BULLETIN (24 HRS) |
| 22.15 HRS | AFRO TIZII |
| 23.00 HRS | NEWS BRIEF |
| 23.03 HRS | AFRO TIZII |
| 01:00-03:00HRS HRS | YALIYOMO YAMO ( MARUDIO ) |
| 03:00 - 05:00HRS | HOJA YA LEO ( MARUDIO ) |

| TIME | THURSDAY PROGRAMME |
|---|---|
| 05.00 AM | HALI YA HEWA / KUMEPAMBAZUKA I |
| 06.00 AM | AMKA NA BBC |
| 06.30 AM | NIPASHE |
| 06.50 AM | MATANGAZO |
| 07.00 AM | NEWS BULLETIN |
| 7:10 AM | MATANGAZO |
| 07.15 AM | TAARIFA ZA BARABARANI |
| 07.25 AM | UDONDOZI WA MAGAZETI |
| 07.40 AM | KUMEPAMBAZUKA II |
| 08.00 AM | HABARI NYEPESI |
| 08.10 AM | KUMEPAMBAZUKA III |
| 09.00 AM | HABARI ZA BIASHARA |
| 09.10 AM | MATANGAZO |
| 09.20 AM | BRAND TALK |
| 09.30 AM | KUMEPAMBAZUKA UKIMWI |
| 10.00 AM | NEWS BRIEF |
| 10.03 AM | DEATH ANNOUNCEMENTS |
| 10.10 AM | YALIYOMO YAMO |
| 13.00 HRS | NEWS BULLETIN |
| 13.10 HRS | DEATH ANNOUNCEMENTS |
| 13:30 HRS | DJ SHOW |
| 16.00 HRS | NEWS BRIEF |
| 16.03 HRS | DEATH ANNOUNCEMENTS |
| 16.30 HRS | HOJA YA LEO |
| 18.30 HRS | DIRA YA DUNIA BBC |
| 19.30 HRS | SPOTI LEO |
| 20.00 HRS | NEWS BULLETIN |
| 20.10 HRS | UCHUNGUZI KAMILI |
| 21.00 HRS | NEWS BRIEF |
| 21.05 HRS | MALUMBANO YA HOJA |
| 23.00 HRS | NEWS BRIEF |
| 23.03 HRS | AFRO TIZII |
| 01:00-03:00HRS | YALIYOMO YAMO ( MARUDIO ) |
| 03:00-05:00HRS | HOJA YA LEO ( MARUDIO ) |

| TIME | FRIDAY PROGRAMME |
|---|---|
| 05.00 AM | HALI YA HEWA / KUMEPAMBAZUKA I |
| 06.00 AM | AMKA NA BBC |
| 06.30 AM | NIPASHE |
| 06.50 AM | MATANGAZO |
| 07.00 AM | NEWS BULLETIN |
| 7:10 AM | MATANGAZO |
| 07.15 AM | TAARIFA ZA BARABARANI |
| 07.25 AM | UDONDOZI WA MAGAZETI |
| 07.40 AM | KUMEPAMBAZUKA II |
| 08.00 AM | HABARI NYEPESI |
| 08.10 AM | KUMEPAMBAZUKA III |
| 09.00 AM | HABARI ZA BIASHARA |
| 09.10 AM | MATANGAZO |
| 09.20 AM | BRAND TALK |
| 10.00 AM | NEWS BRIEF |
| 10.03 AM | DEATH ANNOUNCEMENTS |
| 10.10 AM | HIZI NAZO |
| 13.00 HRS | NEWS BULLETIN |
| 13.10 HRS | DEATH ANNOUNCEMENTS |
| 13:30 HRS | DJ SHOW |
| 16.00 HRS | NEWS BRIEF |
| 16.03 HRS | DEATH ANNOUNCEMENTS |
| 16.30 HRS | HOJA YA LEO |
| 18:30 HRS | DIRA YA DUNIA BBC |
| 19.30 HRS | SPOTI LEO |
| 20.00 HRS | NEWS BULLETIN |
| 20.10 HRS | UCHUNGUZI KAMILI |
| 21.0O HRS | NEWS BRIEF |
| 21.05HRS | KIPIMA JOTO |
| 23.00 HRS | WEEKEND SHOW |
| 01:00 - 03:00HRS | HIZI NAZO ( MARUDIO ) |
| 03:00 - 05:00HRS | HOJA YA LEO ( MARUDIO ) |

| TIME | SATURDAY PROGRAMME |
|---|---|
| 05.00 AM | HALI YA HEWA / KUMEPAMBAZUKA I |
| 06.00 AM | AMKA NA BBC |
| 06.30 AM | NIPASHE |
| 06.50 AM | COMMERCIALS |
| 07.00 AM | NEWS BULLETIN |
| 07.15 AM | NEWSPAPERS REVIEW |
| 07.30 AM | KUMEPAMBAZUKA KISWAHILI |
| 09.00 AM | WATOTO SHOW |
| 10.00 AM | NEWS BRIEF |
| 10.03 AM | DEATH ANNOUNCEMENTS |
| 10.15 AM | MIWANI YA MAISHA |
| 11:00 AM | MTAA WA MAGOMA |
| 13.00 HRS | NEWS BULLETIN |
| 13.10 HRS | DEATH ANNOUNCEMENTS |
| 13:30 HRS | CHAGUO LAKO |
| 15:00 HRS | MUZIKI NA MICHEZO |
| 16.00 HRS | NEWS BRIEF |
| 16.03 HRS | DEATH ANNOUNCEMENTS |
| 16.15 HRS | MIDUNDO MOTOMOTO |
| 18:00 HRS | BONGO TEN |
| 19.30 HRS | SPOTI LEO |
| 20.00 HRS | NEWS BULLETIN |
| 20.15 HRS | CHEMSHA BONGO |
| 21.00 HRS | NEWS BRIEF |
| 21.03 HRS | WEEK END SHOW I |
| 22.00 HRS | NEWS BULLETIN (24 HRS) |
| 22.15 HRS | WEEK END SHOW II |
| 23.00 HRS | NEWS BRIEF |
| 23.03 HRS | WEEK END SHOW III |
| 01:00-03:00HRS | KISWAHILI ( MARUDIO ) |
| 03:00-05:00HRS | MUZIKI & MICHEZO ( MARUDIO ) |

| TIME | SUNDAY PROGRAMME |
|---|---|
| 05.00 AM | HALI YA HEWA / KUMEPAMBAZUKA I |
| 06.00 AM | AMKA NA BBC |
| 06.30 AM | NIPASHE |
| 06.50 AM | COMMERCIALS |
| 07.00 AM | NEWS BULLETIN |
| 07.15 AM | NEWSPAPERS REVIEW |
| 07.30 AM | KUMEPAMBAZUKA - FAMILIA |
| 10.00 AM | NEWS BRIEF |
| 10.03 AM | DEATH ANNOUNCEMENTS |
| 10.15 AM | SUNDAY SPECIAL |
| 11: 00 HRS | TOP 20 |
| 13.00 HRS | NEWS BULLETIN |
| 13.10 HRS | DEATH ANNOUNCEMENTS |
| 13.30 HRS | NANI ZAIDI |
| 16.00 HRS | NEWS BRIEF |
| 16.03 HRS | DEATH ANNOUNCEMENTS |
| 16.30 HRS | MAMBO YA PWANI |
| 18:00 HRS | AFRICAN PANORAMA |
| 19.30 HRS | SPOTI LEO |
| 20.00 HRS | NEWS BULLETIN |
| 20:10 HRS | MBAVU ZANGU |
| 21.00 HRS | NEWS BRIEF |
| 21.03 HRS | MAMBO MSETO |
| 22.00 HRS | NEWS BULLETIN (24 HRS) |
| 22.15 HRS | RAFIKI I |
| 23.00 HRS | NEWS BRIEF |
| 23.03 HRS | RAFIKI II |
| 01:00 - 03:00 | FAMILIA ( MARUDIO ) |
| 03:00 - 05:00 HRS | RED CARPET ( MARUDIO ) |

## CAPITAL RADIO 2017 101.3 FM
## FAHARI YA MSIKILIZAJI/THE LISTENERS PRIDE

**MONDAY**
05:00-09:00HRS MORNING JAM
09:00-13:00HRS LETE RAHA
13:00-14:00HRS DW-RADIO
14:00-16:00HRS CLUB 101
16:00-18:00HRS DALA DALA
18:00-18:10HRS HABARI
18:10-20:00HRS BOZOUK TIME
20:00-21:00HRS HALI HALISI
21:00-22:00HRS SPORTS
22:00-01:00HRS LADHA LAINI

**TUESDAY - FRIDAY**
05:00-09:00HRS MORNING JAM
09:00-13:00HRS LETE RAHA
13:00-14:00HRS DW-RADIO
14:00-16:00HRS CLUB 101
16:00-18:00HRS DALA DALA
18:00-18:10HRS HABARI
18:10-21:00HRS BOZOUK TIME
21:00-21:30HRS SPORTS
21:30-01:00HRS LADHA LAINI
01:00-05:00HRS MUSIC & JINGLES

**SATURDAY**
05:00-07:30HRS MUZIKI
07:30-09:00HRS DK 90 DUNIANI
09:00-10:00HRS MUZIKI
10:00-12:00HRS KADOGOO
12:00-13:00HRS BONGO HITS 1
13:00-14:00HRS DW RADIO
14:00-15:00HRS BONGO HITS 2
15:00-16:00HRS ZAIDI YA UMJUAVYO
16:00-18:00HRS THE SPLASH
18:00-21:00HRS LAID BACK
21:00-21:30HRS SPORTS
21:30-01:00HRS AK 47 LIVE
01:00-05:00HRS MUSIC

**SUNDAY**
05:00-07:30HRS MUZIKI
07:30-09:00HRS GOSPEL MUSIC
09:00-11:00HRS THE SUNDAY
11:00-13:00HRS TOP TWENTY
13:00-14:00HRS DW RADIO
14:00-15:00HRS CAPITAL MICHEZONI
15:00-16:00HRS UKURASA WA MBELE
16:00-18:00HRS UNLIMITED REQUEST
18:00-21:00HRS JIACHIE
21:00-21:30HRS SPORTS
21:30-01:00HRS LADHA LAINI

## Uganda yasisitiza uhusiano mzuri na Rwanda

**KAMPALA,** Uganda

SERIKALI ya Uganda imetupilia mbali madai kwamba uhusiano wake na utawala wa Rwanda umezorota.

Uganda imelazimika kutoka ufafanuzi huo bada ya kuwapo kwa taarifa zinazoeleza kuwa kuna mgogoro kati ya mataifa hayo jirani, ilhali Rwanda inaikosoa Uganda kwa kuwasaidia wapinzani wake walio chini ya vuguvugu la Rwanda National Congress.

Hivi karibuni Rais wa Rwanda, Paul Kagame, alinukuliwa akisema kuwa mgogoro kati ya nchi zao unaendelezwa kwa sababu Uganda imeamua kuamini uvumi unaosambazwa na raia wa Rwanda walioko Afrika Kusini badala ya kuamini kile ambacho serikali yake inaiambia.

Hata hivyo, Msemaji wa serikali ya Uganda, Ofwono Opondo, amekanusha madai kwamba Uganda hutegemea uvumi katika kufuatilia masuala ya uhusiano wake na nchi zingine.

"Ni jambo la kuchekesha kwa yoyote kusema kwamba serikali ya Uganda, haina taasisi zake za kupata habari za kuchunguza badala ya kwenda na habari za uzushi. Hususan habari za Rwanda zilizojitokeza kutoka Afrika Kusini au taifa lolote," alisema Opondo na kuongeza.

Madai ya kuwapo kwa mgogoro unaofukuta kati ya Uganda na Rwanda yameendelea kuripotiwa kwenye vyombo mbalimbali vya habari.

Wakati huu mawaziri wa serikali ya Rwanda na hata Rais Kagame wamenukuliwa wakielezea masikitiko yao kuhusu kuyumbayumba kwa uhusiano kati ya nchi hizo mbili. **BBC**

## Watu 70 wateketea kwa moto Bangladesh

**DHAKA,** Bangladesh

MOTO mkubwa umelipuka katika vitongoji vya zamani sehemu ya Mughal katika mji mkuu wa Bangladesh, Dhaka na kuua watu wasiopungua 70.

Taarifa iliyotolewa na Shirika la Zimamoto nchini Bangladesh, ilieleza kuwa moto huo ulianzia katika ghala ambamo kemikali za kutengeneza bidhaa za nyumbani zimekuwa zikihifadhiwa kinyume cha sheria na baadaye ukaenea katika majengo mengine kwa kasi kubwa.

Miongoni mwa waliofariki ni watu waliokuwa katika sherehe ya harusi, na wengine waliokuwa kwenye migahawa.

Shughuli za uokozi zimekuwa ngumu kutokana na msongamano wa magari katika mitaa ambayo gari la zimamoto lilishindwa kupita katika kitongoji hicho.

Kamanda wa Kikosi cha Zimamoto nchini Bangladesh, Ali Ahmed, alisema bado wanaendelea kutafuta wahanga wa moto huo, na kwamba idadi ya waliokufa inaweza kuongezeka.

Moto huo ulianzia katika mtaa wa Chawkbazar majira ya saa nne usiku saa za Bangladesh. **DW**

# Tume ya Uchaguzi Nigeria yawatoa hofu wapigakura

**LAGOS,** Nigeria

ZIKIWA zimebakia siku tatu kabla ya kufanyika kwa uchaguzi mkuu nchini Nigeria, Tume ya Uchaguzi nchini humo INEC imewaondoa hofu wananchi kwa kuwaeleza uchaguzi lazima utafanyika siku ya Jumamosi.

Tangu kuahirishwa kwa uchaguzi Februari 16, Nigeria inaendelea kukumbwa na mgogoro wa uchaguzi. Hata hivyo, INEC inakabiliwa na shinikizo.

Vyama viwili vikuu vya siasa ambavyo mwezi uliopita viliwataka wafuasi wao kuwa watulivu, sasa vinaendesha vita vya maneno makali dhidi ya INEC.

**Vyama viwili vikuu vya siasa vinaishtumu INEC kushindwa kuandaa uchaguzi huru, wa kuaminika na wa wazi.**

Vyama hivyo vinaishtumu INEC kushindwa kuandaa uchaguzi huru, wa kuaminika na wa wazi.

Wakati huo huo, INEC imewahakikisha kuwa uchaguzi utafanyika Jumamosi ya Februari 23.

INEC inashtumiwa kuegemea upande wa upinzani, huku upinzani ukiishtumu kuwa chini ya udhibiti wa serikali.

Chama tawala cha All Progressives Party, APC, na chama cha upinzani cha People's Democratic Party, PDD, vinashangazwa uamuzi wa INEC wa kusogeza mbele uchaguzi mkuu dakika chache kabla ya zoezi la kupiga kura kuanza Jumamosi ya wiki iliyopita.

INEC ilisema imefikia uamuzi wa kuahirisha uchaguzi baada ya kutafakari kwa kina kuhusu masuala ya usafirishaji wa vifaa na kufika kwa wakati kwenye vituo, changamoto ambayo tume hiyo inasema isingewezekana kuwa na uchaguzi huru, haki na wakuaminika.

Hata hivyo, Mwenyekiti wa INEC, Mahmood Yakubu, akizungumza na wanahabari usiku wa kuamkia siku ya upigaji kura, alisema kwa ratiba ilivyo, isingewezekana tena kwa uchaguzi huo kufanyika kwa wakati. **RFI**



Rais wa Marekani, Donald Trump (kulia), akiwa na mtoto wa Mfalme wa Saudi Arabia, Salman bin Abdelaziz, wakati wa ziara yake katika taifa hilo la kifalme. **PICHA: ALLIANCE**

# Maaskofu Katoliki wakutana kujadili unyanyasaji kingono

**VATICAN,** Italy

KIONGOZI wa Kanisa Katoliki, Papa Francis, amefungua mkutano wa kilele mjini Vatican wa kupambana na unyanyasaji wa kingono dhidi ya watoto, akisema dunia inatarajia hatua madhubuti kupiga vita unyanyasaji huo kanisani.

Amesema watu watakatifu wa Mungu wanatizama na kusubiri sio tu kukosolewa kwa unyanyasaji wa kingono dhidi ya watoto, lakini wanasubiri kuona hatua na mikakati dhabiti ikichukuliwa dhidi ya suala hilo.

Akizungumza katika hotuba yake alipokuwa anaufungua mkutano huo ulioanza jana na kutarajiwa kumalizika siku ya Jumapili, Papa aliwataka maaskofu kuja na majibu yanayofaa na thabiti ya kupambana na unyanyasaji huo wa kingono dhidi ya watoto.

Washiriki 190 kutoka duniani kote wanatarajia kukutana kwa siku tatu jijini Roma.

Ni mkutano muhimu kwa Kanisa Katoliki linalokabiliwa na kashfa ya udhalilishaji wa kingono kwa watoto.

Mwishoni mwa majira ya joto, baada ya kufichuliwa kashfa mpya ya viongozi wa kanisa wanaojihusisha na vitendo vya udhalilishaji kwa watoto nchini Marekani, Papa Francis na baraza lake la makardinali waliamua kuitisha mkutano wa kimataifa.

Katika mkutano huo watashiriki wakuu 114 wa mabaraza ya maaskofu wa Kanisa Katoliki; 36 kutoka Afrika, 32 kutoka Ulaya, 24 kutoka Amerika na 18 kutoka Asia.

Mwanzoni mwa mwezi huu Papa Francis alikiri kuwa makasisi wa Kanisa Katoliki wanawatumia watawa kama watumwa wa ngono.

Ilikuwa ni mara ya kwanza kwa Papa Francis kukiri hadharani kuhusu dhuluma za kingono dhidi ya watawa wa kanisa hilo kubwa zaidi duniani.

Papa alitoa tamko hilo kwa wanahabari akiwa kwenye ziara yake kihistoria katika eneo la mashariki ya kati.

Alikiri kuwa makasisi na maaskofu wamekuwa wakiwanyanyasa watawa, na kwamba kanisa litashughulikia suala hilo. **RFI**

# Wema akana kusambaza picha ngono mtandaoni

**Na Hellen Mwango**

MSANII wa filamu nchini, Wema Sepetu (30), amekana mahakamani tuhuma za kuchapisha video ya ngono katika ukurasa wake kwenye mtandao wa Instagram.

Hata hivyo, Wema amekiri majina na anwani yake wakati akisomewa maelezo ya awali jana katika Mahakama ya Hakimu Mkazi Kisutu, Dar es Salaam, mbele ya Hakimu Mkazi Maira Kasonde.

Wakili wa Serikali, Glory Mwenda, alidai kuwa kesi hiyo imepangwa kwa ajili kusikiliza maelezo ya awali dhidi ya mshtakiwa.

Wakili wa utetezi, Ruben Simwanza, alidai utetezi uko tayari kusikiliza maelezo hayo. Mwenda alidai kuwa Wema anakabiliwa na shtaka moja la kuchapisha video ya ngono katika mtandao wa jamii wa Instagram.

Alidai kuwa alitenda kosa hilo Oktoba 15, mwaka jana, katika maeneo mbalimbali ya Jiji la Dar Es Salaam kwa kusambaza video za ngono kupitia ukurasa wake wa Instagram, picha zisizokuwa na maudhui.

Wakili huyo, alidai Wema ambaye ni mkazi wa Mbezi Salasala, anamiliki ukurasa katika mtandao wa jamii wa Istagram wenye jina la Wemasepetu.

Alidai siku hiyo ya tukio, mshtakiwa alirekodi video ya ngono ambayo haina maudhui kupitia simu yake ya kiganjani, akitumia laini ya Vodacom yenye namba 0755 555 655.

Wakili huyo alidai kuwa baada ya kurekodi video hiyo, Oktoba 25, mwaka jana, mshtakiwa huyo aliisambaza katika akaunti yake ya Istagram, wakati akijua kufanya hivyo ni kinyume cha sheria.

Mwenda alidai kuwa video hiyo aliyorekodi na Wema, ilikuwa inaonyesha kuwa Wema alikuwa ananyonyana ndimi na mwanamume, huku akijua kuwa kitendo hicho ni kinyume cha maadili ya Kitanzania.

Hata hivyo, Oktoba 25, mwaka jana maofisa wa Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania (TCRA), waliiona video hiyo na kuripoti katika kituo cha Polisi Kijitonyama.

Upande wa mashtaka ulidai kuwa baada ya maofisa wa TCRA kuripoti tukio hilo, Wema alikamatwa Oktoba 29 na kupelekwa katika kituo cha Kikuu cha Polisi (Central) na kuhojiwa.

Baada ya kuhojiwa polisi, Wema alikana kuhusiana na tukio hilo na Novemba Mosi, alifikishwa katika Mahakama ya Hakimu Mkazi Kisutu na kufunguliwa shtaka moja la kusambaza video ya ngono katika mitandao ya kijamii.

Aliposomewa maelezo hayo, alikubali majina yake mawili, anwani yake na sehemu anayoishi. Pia alikubali kuwa anamiliki akaunti ya Istagram yenye jina la Wemasepetu.

Alikiri kukamatwa Oktoba 29, 2018 na kupelekwa Kituo Kikuu cha Polisi kwa ajili ya kuhojiwa, alifikishwa Mahakama ya Kisutu, Novemba Mosi, 2018, kujibu shtaka linalomkabili.

Upande wa mashtaka ulidai kuwa unatarajia kuwa na mashahidi watano katika kesi hiyo na Hakimu Kasonde alisema kesi hiyo itaanza kusikiliza mashahidi wa Jamhuri Machi 18, mwaka huu.



Mkuu wa Idara ya Wateja mmoja mmoja wa Benki ya Standard Chartered Afrika na Mashariki ya Kati, Jaydeep Gupta (kushoto), Ofisa Mtendaji Mkuu wa SCB Tanzania, Sanjay Rughani (wa pili kushoto), Balozi wa SCB Tanzania, Vanessa Mdee (kulia), Mkuu wa Wateja wa benki hiyo nchini, Ajmair Riaz, wakishuhudia uzinduzi wa huduma za kidijitali wa benki hiyo, jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: SELEMANI MPOCHI**

# Acacia, Barrick zagongana bil. 682/-

INATOKA UK. 2

Alibainisha kuwa baada ya muungano huo wa Rand Gold na Barrick Gold, sasa kampuni mpya ya Barrick Gold imekuwa kubwa inayoongoza kwa umiliki wa rasilimali za dhahabu duniani ikimiliki rasilimali tano kati ya 10.

Kutokana na uwezo huo, alisema Barrick Gold Corporation sasa imeweza kujiimarisha zaidi kiuwekezaji na utaalamu na iko tayari kushirikiana na Tanzania kuhakikisha rasilimali ya dhahabu iliyoko inaleta manufaa kwa pande zote mbili, yaani Watanzania na mwekezaji.

Kwa upande wake, Waziri wa Katiba na Sheria Prof. Palamagamba Kabudi, ambaye aliongoza timu ya majadiliano kwa niaba ya serikali ya Tanzania na kampuni ya Barrick Gold, alisema nyaraka za makubaliano hayo zimekamilika na kwamba sasa kinachosubiriwa ni utekelezaji wa makubaliano hayo unaotarajiwa kukamilika ifikapo mwisho wa mwezi ujao.

Baada ya muungano wao (Rand Gold na Barrick Gold Corporation) hii sasa ni timu mpya na tumewaona ni watu ambao sasa wako tayari kutekeleza yale yote yaliyokubaliwa na sasa ni kwa kila upande kwenda kwenye vyombo vyake vinavyohusika kufanya uamuzi wa mwisho ili utekelezaji ufanyike," alisema Prof. Kabudi.



# Uporaji bodaboda kwa mtutu washamiri Dar

INATOKA UK. 2

ghafla niliwekewa bastola kwenye mbavu, nikajikuta nawauliza mmetumwa roho yangu au ni hii pikipiki? alisema Ally Kayombo wakati akielezea kuhusu mkasa uliomkuta.

"Hawakunijibu walikuwa watatu mmoja wapo aliyeshika silaha akaniuliza kwani hujui? Nikashuka nikaamrishwa nigeuke nitembee nisiangalie nyuma, huku mmoja akiliza miguu kunifuata," alisema.

Anasema baada ya mwendo kiasi hakusikia tena vishindo nyuma yake akageuka na kubaini pikipiki haipo wala gari la wahalifu.

"Wakati naporwa ilikuwa ni saa 3 asubuhi eneo la Makuburi nawaona watu kuomba msaada nikaogopa kufumuliwa kwa risasi," alisema Kayombo na kuongeza:

"Niliamua kuisalimisha roho yangu, kwa kuwa licha ya kwamba nimepitia mafunzo ya mgambo sikuona kama yangenisaidia kwa jinsi ambavyo walijipanga, pikipiki nitatafuta nyingine lakini, roho ikitoka imetoka."

Masoud Ramadhan huku akiwa na majeraha ya kupigwa na vitu vyenye ncha kali alisema kuwa anashukuru Mungu amenusurika kwa mara nyingine tena.

Alisema Novemba mwaka jana alinusurika kuuawa na kuporwa pikipiki baada ya kumshusha mteja akawa anasubiri mteja amlipe, mara pikipiki nyingine ikasimamishwa alipoangalia vizuri akaona mmoja ana bastola mkononi.

"Kwa kuwa nilikuwa sijazima pikipiki nikakanyaga mafuta akafyatua risasi ikanipata kwenye bega ila haikugusa mfupa, hivyo nikamudu kuendelea kukimbia hadi nilipotokezea sehemu nyingine," alisema.

Ramadhani alisema aliomba kupelekwa kituo cha polisi, ambapo baada ya kufika polisi walipomwona walimsaidia kwa kumchukua wao wenyewe na kumpeleka Hospitali ya Serikali Mbezi kwa matibabu.

Ramadhani alieleza kuwa tukio la pili la kushambuliwa kwake lilitokea Februari 18, mwaka huu, wakati akiwa njiani anarejea kumshusha abiria wake saa 8 usiku.

Alisema akiwa kwenye barabara inayotengenezwa katika eneo la katikati ya Suka na Temboni aliipita pikipiki iliyokuwa imesimamishwa, lakini dereva na abiria wamepanda.

"Nikiwa katika mwendo, ghafla nikashtuka pikipiki inagongwa, nikayumba na kuanguka, wakaniwahi na kuanza kunishambulia, lakini kuna gari likatokea likawasha taa kali, wakati mmoja wao akijaribu kuiwasha pikipiki yangu ili akimbie nayo akashindwa maana iligoma kuwaka," alisema Ramadhani huku akiugulia maumivu.

**KAULI YA POLISI**

Kamanda wa Mkoa wa Polisi Kinondoni, Mussa Taibu, alisema tukio la Mpakani kwa Msuguri wamepata taarifa zake na mengine yote yaliyoripotiwa polisi wanaendelea kuyafanyia kazi ili kuwabaini wahusika.

"Nawasisitiza madereva wa bodaboda kuwa makini na abiria wanaowabeba hasa usiku, ikiwezekana wawapige picha ndipo wawapeleke, anayekataa atakuwa na lake baya, pia wasikubali kwenda kwenye maeneo ambayo yana mazingira hayaeleweki," alisema kamanda huyo.

Kwa mujibu wa taarifa ya Polisi Kanda Maalum ya Dar es Salaam ya mwaka 2017, pikipiki zilizoibwa ni 1,778, zilizopatikana ni 127.

## TANGAZO

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

### HUDUMA MBALIMBALI

**MKOPO WA HARAKA NA NAFUU** Pata mkopo wa dharura ndani ya siku 2. Kwa wafanyakazi na Wafanyabiashara kutoka ENTERPRISE FINANCE LIMITED (EFL). Kwa mawasiliano Zaidi piga: 0768 928516 / 0653 258662. KARIBU EFL.

### MASHAMBA/VIWANJA

**KIWANJA KINAUZWA,** Kipo Kisongo Arusha jirani na Braebun School Kina upana wa 43,urefu 93 . Bei Milioni 40 kimepimwa. Maji, barabara na umeme vipo. Mawasiliano:-0755 907 520.

**SHAMBA LA ACRE 2 LINAUZWA** liko kilometre 3 toka chanika mjini ,mtaa wa > zogo ally kata ya homboza wilaya ya kisarawe bei ni milioni 43. No ya cm ni 0653019311

### MAGARI/VIPURI


**LOOKING FOR TOYOTA** NOAH for hiring long term contract. price 30,000 - 40,000 per day. Please call 0627301010 for details.

### NAFASI ZA KAZI

**TUNAAJIRI WASICHANA WA MAUZO (SALES).** SIFA KIDATO CHA NNE. UMRI KUANZIA MIAKA 25 – 38 AWE MTANZANIA. MASLAHI MAZURI. PIGA SIMU NAMBA 0714 634046.

*Uza Chenye Thamani Kubwa*
*Kwa Kutangaza Nasi*
*Kwa Bei Poa*
*Tupigie 0767 223311*


### KUPOTEA KWA VYETI



**MESHUKI L. LANGOY** anatangaza kupotelewa na vyeti vifuatavyo; Cheti cha kidato cha nne chenye **Index Namba S0949-0201** kilichotolewa na Baraza la Mitihani la Taifa mwaka 2009 katika Shule ya Sekondari Irkisongo, Cheti cha Diploma kilichotolewa na chuo cha Arusha Technical College chenye namba ya usajiri **A0100062** kilichotolewa mwaka 2014, Cheti cha kuzaliwa chenye Namba **BB/No.011741** Na kitambulisho cha Taifa cha Uraia.
Yeyote atakaeviona atoe taarifa kituo chochote cha polisi kilicho karibu . Taarifa Polisi **SO/RB/715/2019**

XXXXXXXX


### VYETI VIMEPOTEA



**ZEBIUS SIAME** anatangaza kupotelewa na Cheti cha IV namba **S0119-0106** cha KIBAHA SEKONDARI mwaka 2010. Cheti cha kidato cha sita namba **S0103-0724** cha BIHAWANA SEKONDARI mwaka 2013. Bsc in Applied Zoology namba **BSCAZ0000022** cha University of Dar e salaam mwaka 2016. Transcript of Examinations Result namba **2013-04-02670.** Certificate of Birth namba 1831318. Yeyote atakayeviona atoe taarifa kituo cha polisi. Taarifa ya polisi: **MB/RB/29667/2018.**

115073602

### KUPOTELEWA NA CHETI CHA KIDATO CHA NNE



**Mashinagwi Jeck** wa Sokomatola Mbeya, anatangaza kupotelewa na Cheti cha Kidato cha Nne chenye **Index namba S.2830-0080** Mwaka 2010 katika Shule ya Sekondari Nyakaliro.

Yeyote atakayekiona atoe taarifa Kituo cha Polisi. Taarifa ya Polisi **MB/RB/953/2019.**

215073402

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA**

**USIMAMIZI WA MIRATHI**
**(S.M.M.1984 NYONGEZA)**
**YA 5 KANUNI YA 2**

**Katika mahakama ya mwanzo MJINI MOROGORO**

**Usimamizi wa mirathi No;44/2019**

**Ombi la MIRAJI OMARI KIBWANA Kuteuliwa msimamizi wa mirathi marehemu HADIJA ISSA SELEMAN**

Watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote na mirathi ya marehemu kuwa wanaarikwa kuja na kuudhuria shaurini mnamo tarehe 05/03/2019 kabla ya muombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo.

Wosia ya marehemu huyo upo Mahakamani waweza kukaguliwa tarehe 20/02/2019.

215074102

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**KATIKA BARAZA LA ARDHI NA NYUMBA WILAYA YA ILALA**
**(MWALIMU HOUSE GHOROFA YA 6)**
**SHAURI LA MADAI NAMBA 339 YA MWAKA 2018**
**RICHARD ERNEST LYIMO.......................MWOMBAJI**
**DHIDI YA**
**BERTHA SHADRACK NATAI NA WENZAKE**
**WATATU.....................WAJIBU MAOMBI**

**KUITWA SHAURINI**

**SAID RAMADHANI SEIF NA DOLPHIN GENERAL BUSINESS ENTREPRISES CO. LTD** } **..................POPOTE MLIPO**

**RICHARD ERNEST LYIMO** amewasilisha shauri mbele ya Baraza la Ardhi na Nyumba (W) Ilala lililopo (Mwalimu House Grorofa ya sita). Maombi hayo yamepangwa kutajwa tarehe 07/03/2019. Hivyo basi mnatakiwa ninyi wenyewe au wakili wenu kuleta utetezi ndani ya siku 21 kuanzia tarehe ya tangazo hili kutolewa. Vielelezo vyote vinavyohusu shauri tajwa vinapatikana katika Masijala ya wazi ya Baraza la Ardhi na Nyumba (W) Ilala. Endapo hamtatekeleza haya, maombi hayo yatasikilizwa upande mmoja na uamuzi/amri kutolewa.

Imetolewa na kutiwa muhuri wa Baraza leo tarehe 14 mwezi Februari, mwaka 2019.

115073502

### KADI YA GARI IMEPOTEA

**LEDY SLAA STORE** anatangaza kupotelewa na kadi ya gari aina ya SUZUKI CARRY iliyosajiliwa kwa namba **T 355 DFP.** Engine No. **F6A3424,** Chassis No **DB52T183424.** Kwa atakayeiona atoe taarifa kituo cha polisi kilichopo karibu nae. Taarifa ya polisi: **USR/TR/RB/61/2019.**

215074402

*Kwa Habari Motomoto*
*usikose Gazeti lako la The Guardian*
*kila siku*
*Tutumie E-mail: advertise@guardian.co.tz,*
*au piga simu: 0767 223311*

## JE UNAHANGAIKA PA KUUZA BIDHAA YAKO?

# Nipashe

NI JIBU LAKO NJOO UTANGAZE BIDHAA YAKO

KWA BEI NAFUU SANA

Tutumie E-mail: advertise@guardian.co.tz, Tupigie 0767 223311

TAHADHARI: Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha, au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji THE GUARDIAN LIMITED hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.




# UNAI ASEMA OZIL ATAJIHUKUMU MWENYEWE

**LONDON,** England

UNAI Emery amempa changamoto Mesut Ozil, kuthibitisha kiwango chake na kuongeza kwamba Mjerumani huyo ameshikilia funguo yake mwenyewe ya majaliwa yake hapo katika dimba la Emirates.

Ozil amekuwa katikati ya mjadala kuhusu kiwango na majaliwa yake msimu huu, huku uvumi mwingine ukisema kwamba Emery hajavutiwa na kiwango chake cha uchezaji.

Ameanza katika mechi 13 za Ligi msimu huu, huku majeraha yakitajwa kumfanya ashindwe kucheza mara kwa mara na pia ameshindwa kupenya kwenye kikosi cha kwanza.

Wakati alipoulizwa kama atampa nafasi Ozil kuendelea kucheza hapo Arsenal, Emery, alisisitiza kwamba kiungo huyo anatakiwa kujiimarisha yeye mwenyewe.

Akinukuliwa na gazeti la Telegraph alisema: "Kwanza, ufunguo uko mikononi mwake mwenyewe.

"Na anajitahidi wiki hii. Nilimwambia kwenye majadiliano yetu kujifua na kurudisha kiwango chake kwenye mazoezi.

"Wakati unapofanya mazoezi na kiwango chako kuimarika unaweza kutusaidia sisi kwenye mechi zetu. Sasa wiki hii ni nzuri kwa wachezaji wote kwa sababu tupo katika wakati muhimu zaidi kwenye msimu.

"Namwangalia yeye na anafanya mazoezi kama tunavyotaka sisi. Najua anataka kucheza. Lakini anahitaji kiwango chake kuimarika, kuwepo kwenye mazoezi kwa ajili ya mechi.

"Bila majeraha, bila ugonjwa wowote. Nafikiri tunaweza kuuona ubora wa Mesut ukitusaidia sisi."

Emery alikuwa akizungumza kuelekea kwenye mchezo wa Europa, ambapo Arsenal ilitarajiwa kucheza na BATE Borisov jana Alhamisi.

Washikabundi hao wakiwa bila Ozil, walifungwa 1-0 kwenye mchezo wa kwanza na hivyo sasa wanatakiwa kuishinda timu hiyo kutoka nchini Belarus ili kufuzu hatua ya mtoano.

# *Ronaldo: Nimetwaa mara tano, Atletico Madrid hawajawahi*

**MADRID,** Hispana

CRISTIANO Ronaldo ameonekana kuwajibu Atletico Madrid baada ya timu yake ya Juventus kufungwa mabao 2-0 kwenye mchezo wa kwanza wa Ligi ya Mabingwa Ulaya hatua ya 16 bora.

Ronaldo aliondoka uwanjani akiwaonyesha mashabiki wa Atletico Madrid alama ya tano kwa maana yeye ameshinda mara tano kombe hilo, wakati timu hiyo haijawahi.

Mchezaji huyo wa zamani wa Real Madrid aliondoka Hispania akiwa hana furaha baada ya kikosi hicho cha kocha, Diego Simeone kupata ushindi huo usiku Jumatano.

Kuna wakati mchezo huo ukiendelea, Ronaldo aliwajibu mashabiki waliokuwa wakimzomea kwenye Uwanja wa Wanda Metropolitano kwa kuwaonyesha vidole vitano vya mkono sawa na idadi ya mataji ya Ligi ya Mabingwa aliyoshinda, manne akishinda akiwa na Madrid na moja akiwa na Manchester United.

Na Ronaldo aliendelea kuonyesha vidole vitano kwenye jezi yake wakati akitoka uwanjani baada ya mchezo huo.

"Nimeshinda mataji matano ya Ligi ya Mabingwa Ulaya na hawa jamaa wana sifuri," alisema akiwaambia waandishi wa habari baada ya mchezo huo.




# Barcelona walikataa kumsajili Benzema

**BARCELONA,** Hispania

BARCELONA ilikataa nafasi ya kumsajili Karim Benzema kutoka Lyon mwaka 2008, baada ya ripoti kuonyesha kuwa tabia ya mshambuliaji huyo ingekuwa hatari kwao.

Wakati akiwa katika klabu yake hiyo ya utotoni, Benzema alijiimarisha mwenyewe na kuonekana kama mmoja wa wachezaji watakaokuja kuishangaza duniani.




Angeweza kwenda Barcelona, lakini wapinzani wakubwa wa Real Madrid, walimsajili kwa kiasi cha pauni milioni 30 na kutua kwenye dimba la Bernabeu mwaka 2009. Na habari hizi za Barcelona kuwa ilitaka kumsajili Benzema zimeandikwa na gazeti la Marca, ambalo limebainisha kwamba, mshambuliaji huyo alikuwa chaguo la kwanza la usajili wa Barcelona wakati huo.

Liliandika: "Barcelona walimhitaji mshambuliaji huyu mwaka 2008 wakati Pep Guardiola alipowasili katika dimba la Camp Nou na hakumtaka Samuel Eto'o.

"Txiki Begisristain, ambaye wakati huo alikuwa mkurugenzi wa ufundi wa Barcelona, alitumwa kumfuatilia na alikwenda nyumbani kwa Benzema mjini Lyon, ili kumshawishi asajiliwe na klabu, huku kila mmoja pale Camp Nou aliamini kwamba angejiunga nao.

"Hata hivyo, Begisristain hakufurahishwa na mazingira aliyoyakuta. Hakupendezwa na marafiki wa mshambuliaji huyo aliokuwa nao na hivyo akaitaarifu klabu kwamba kumsajili mchezaji huyo ni hatari kwa tabia zake."

## HABARI MICHEZO

# Kane arudi mazoezini Tottenham

**LONDON,** England

HARRY Kane amerudi jumla kwenye mazoezi na Tottenham, huku akikaribia kupona kabisa kifundo cha mguu alichoumia.

Kane alikuwa nje ya dimba tangu alipoumia enka kwenye mchezo dhidi ya Manchester United Januari na awali alitarajiwa kuwa nje ya uwanja hadi Machi mwaka huu.

Nahodha huyo wa Timu ya Taifa ya England amekosa mechi saba kwa Spurs, ukiwamo wa wiki iliyopita wa ushindi wa mabao 3-0 dhidi ya Borussia Dortmund, kwenye mchezo wa kwanza wa Ligi ya Mabingwa Ulaya hatua ya mtoano wa timu 16.

Lakini Kane amerudi haraka tofauti na matarajio, huku Spurs waithibitisha Jumatano kwamba mshambuliaji wao amerudi kwenye mazoezi na kikosi.

Kurudi kwake sasa kunaweza kumfanya Kane akacheza dhidi ya Burnley mchezo wa Ligi Kuu England kesho Jumamosi.






# GUARDIOLA: CITY BADO INA KAZI NGUMU

**MUNICH,** Ujerumani

PEP Guardiola ameionya Manchester City, haiwezi kushinda Kombe la Ligi ya Mabingwa Ulaya kama wanawazawadia wapinzani wao mabao kama walivyofanya wakati wakiibuka na ushindi wa 3-2 dhidi ya Schalke.

City ilipata ushindi katika mchezo huo wa kwanza wa hatua ya mtoano wa timu 16 nchini Ujerumani, ingawa ushindi wao ulitakiwa kusubiri bao la kusawazisha la Leroy Sane aliyetokea benchi dakika ya 85 kabla ya Raheem Sterling kufunga la ushindi dakika ya 90.

Schalke walitanguliwa kufungwa kwa bao la Sergio Aguero kabla ya kuongoza kwa 2-1 shukrani kwa mabao ya penalti yaliyofungwa na Nabil Bentaleb, ya kwanza likitokana na Nicolas Otamendi aliyeunawa mpira eneo la hatari na faulo ya Fernandinho. Halafu Otamendi akapata kadi ya pili ya njano iliyozaa kadi nyekundu kwa kumchezea vibaya Guido Burgstaller, na Guardiola alibainisha kwamba City wanatakiwa kujiona kama waliopata bahati kupata ushindi huo wa mchezo wa kwanza.

"Matokeo ni mazuri kwa uhakika, mabao matatu ugenini ni kitu kizuri," alisema Guardiola akiwaambia waandishi wa habari baada ya mchezo huo.

"Tuliwapa (Schalke) bao la kwanza, tukawapa bao la pili na tukapata kadi nyekundu. Katika hatua hiyo, bado hatupo tayati kupigana kwa ajili ya Ligi ya Mabingwa Ulaya, lakini matokeo ni mazuri.

"Najua ni vigumu kucheza nchini Ujerumani. Hawakupiga mashuti ya kulenga goli, lakini walifunga mabao mawili kwa penalti.

# *Allegri: Juventus haijafa bado*

**MADRID,** Hispania

KOCHA Massimiliano Allegri amesisitiza kwamba kikosi chake bado 'hakijafa' licha ya kufungwa mabao 2-0 na Atletico Madrid kwenye mchezo wa kwanza wa Ligi ya Mabingwa Ulaya, hatua ya mtoano wa timu 16 juzi Jumatano.

Juve walifungwa kwa mabao ya 'usiku' kutoka kwa Jose Gimenez na Diego Godin na awali walifungwa bao na mchezaji wao wa zamani Alvaro Morata, lakini lilikataliwa na teknolojia ya maamuzi ya video, VAR huku Juve sasa ikikabiliwa na wakati mgumu wa kufuzu hatua ya robo fainali kwenye mchezo wa pili utakaopigwa mwezi ujao mjini Turin, Allegri amedai kwamba kikosi chake kililazimika kucheza vibaya dhidi ya wenyeji wao.

"Kipindi cha pili kilikuwa kibaya kwetu, tulifanya makosa yaliyowapa wao nafasi," alisema akiiambia Sky Sport Italia. "Atletico ni timu nzuri walitufanya tuondoke bila kupiga mashuti ya maana langoni mwao.


"Tulishajiweka kwenye hatari sisi wenyewe wakati tulipopoteza zaidi mpira, lakini ukweli ni kwamba hatukupiga mashuti ya kulenga bao. Atletico walicheza kwa hamasa kubwa na wakatukamata haraka.

"Sasa tuna nafasi ya kubadilisha matokeo kwenye mchezo wa pili. Tunatakiwa kuwa na imani, tutakuwa na wachezaji wengine ambao watakuwa wanarudi uwanjani.

"Tulijua kwamba ingekuwa ngumu, kwamba Atletico Madrid wanakulazimisha kucheza vibaya. Tulicheza mpira kwa haraka kipindi cha kwanza, lakini kipindi cha pili tulishindwa.



# DONDOO OKA
## MAGAZETI Y LAYA




# RASHFORD, UNITED SASA KIMEELEWEKA

●●● Inaelezwa kuwa mshambuliaji huyo amekubali kusaini mkataba mpya...

**MANCHESTER,** England

HABARI za uhakika zinasema kuwa Marcus Rashford yuko tayari kusaini mkataba mnono wa miaka sita katika klabu yake ya Manchester United.

**Mshambuliaji huyo wa Timu ya Taifa ya England alikuwa katika wakati mgumu wakati wa Jose Mourinho, lakini amekuwa mchezaji muhimu wa United tangu kutua kwa kocha wa muda, Ole Gunnar Solskjaer.**

Gazeti la The Mirror limeandika kuwa, mazungumzo kati ya Rashford na klabu hiyo yamekwenda vizuri na sasa anajiandaa kusaini mkataba mpya ambao utamfanya akae klabuni hapo hadi kipindi cha majira ya joto mwaka 2025.

Mkataba huo mpya atakaosaini Rashford utamfanya pia alipwe mshahara wa pauni 200,000 kwa wiki.

Mkataba wa sasa wa Rashford unatarajiwa kumalizika mwakani, ingawa una kipengele kinachoruhusu kusaini mkataba mwingine wa mwaka mmoja.

Taarifa zilieleza kuwa Rashford alikuwa ana hatihati na hatima yake ndani ya Old Trafford wakati United ilikuwa ikiongozwa na Mourinho, lakini sasa mshambuliaji huyo mwenye umri wa miaka 21 ana furaha.

Rashford sasa anachezeshwa nafasi ya mbele na Solskjaer na tayari amefunga mabao nane kwenye mechi 15 alizocheza mpaka sasa.

Katika muda ambao amekaa katika kikosi cha United, Rashford ameshinda taji la Ligi ya Europa, Kombe la FA na Kombe la Ligi.

United pia iko katika mchakato wa kuhakikisha David De Gea anasaini mkataba mpya, lakini golokipa huyo bado hajawa tayari kuweka saini mkataba huo mpya ambao utamfanya aendelee kukaa kwa muda mrefu klabuni hapo.

Inaelezwa kuwa Mhispania huyo amesema atakuwa tayari kusaini mkataba mpya endapo United itamlipa kiasi cha pauni milioni 90, mkataba wa sasa wa mlinda mlango huyo unatarajiwa kumalizika mwisho wa msimu wa 2019/20.

Taarifa zinaelezwa kuwa United imempa ofa ya mkataba wa miaka mitano na itamlipa mshahara wa pauni 350,000 kwa wiki kipa huyo ambaye anatajwa kuwaniwa na Juventus na Paris Saint-Germain.

Kikosi cha Solskjaer kiko katika nafasi ya nne katika msimamo wa Ligi Kuu England na Jumapili kitawakaribisha Liverpool.

## ZISIKUPITE

### MADRID KUMTOA BALE

REAL Madrid itamruhusu mshambuliaji wa Wales, Gareth Bale, kuondoka katika kipindi cha majira ya joto ili kupata nafasi ya kumnasa straika wa Chelsea na Timu ya Taifa ya Ubelgiji, Eden Hazard (28) au kiungo wa Tottenham na Timu ya Taifa ya Denmark, Christian Eriksen (27). ***(Marca)***

### HUDSON-ODI ATAKIWA PSG

PARIS St-Germain inajipanga kumsajili mshambuliaji wa Chelsea na Timu ya Taifa ya Vijana ya England (U-19), Callum Hudson-Odoi (18), ambaye pia anawaniwa na Bayern Munich. ***(Sun)***

### BLANC KUMRITHI SARRI

KOCHA wa zamani wa Timu ya Taifa ya Ufaransa na Paris St-Germain, Laurent Blanc, anatarajiwa kuwa mmoja wa makocha wenye nafasi ya kurithi mikoba ya Maurizio Sarri kama Chelsea itaamua kumfukuza Mtaliano huyo wiki ijayo. (London Evening Standard)

### RAKITIC KUTUA MILAN

BARCELONA iko katika mazungumzo ya kumuuza kiungo wa Timu ya Taifa ya Croatia, Ivan Rakitic kwa Inter Milan ya Italia, lakini vigogo hao wa Hispania wanahitaji kulipwa kiasi cha pauni milioni 39 ili kumtoa nyota huyo mwenye umri wa miaka 30. ***(AS)***

### RODRIGUEZ AIKACHA ARSENAL

MATUMAINI ya Arsenal kumsajili mshambuliaji wa Colombia, James Rodriguez yamezimwa na nyota huyo mwenye umri wa miaka 27 ambaye anaichezea kwa mkopo Bayern Munich, kueleza kuwa anataka kurejea katika klabu yenye asili ya wazazi wake ya Real Madrid mwishoni mwa msimu huu. ***(Mirror)***

### BARCA, ARSENAL KUCHUANA

BARCELONA imeungana na Arsenal katika mbio za kuwania saini ya kiungo wa Lyon ya Ufaransa, Houssem Aouar, ambaye ana umri wa miaka 20. ***(Sun)***

### VIEIRA AIVUTIA LYON

KIUNGO wa zamani wa Arsenal, Patrick Vieira (42), anafuatiliwa na Lyon baada ya kufanikiwa kuipa matokeo mazuri klabu ya Nice ambayo anaiongoza. ***(Sun)***

### ALMIRON ALITAKIWA UTD

KIUNGO mshambuliaji wa Paraguay, Miguel Almiron, alikaribia kusajiliwa na Manchester United kabla ya kutua Newcastle, wakala wa mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 25 amesema. ***(Newcastle Chronicle)***

### MTOTO WA THURAM SOKONI

CHELSEA na Liverpool zimeonyesha nia ya kumnasa kinda, Khephren Thuram (17), ambaye ni mtoto wa mchezaji wa zamani wa Timu ya Taifa ya Ufaransa, Lilian Thuram. Nyota huyo ambaye yuko katika kikosi cha U-18 cha Ufaransa anakaribia kusaini mkataba wa kuitumikia Monaco. ***(Mail)***

### ALUKO KUKIPIGA CHINA

MSHAMBULIAJI wa Reading na Timu ya Taifa ya Nigeria, Sone Aluko (30), anatarajia kukamilisha mchakato wa kujiunga na klabu ya Beijing Renhe ya China. ***(Mail)***

# AJIBU AFUNGUKA YANGA INAVYOTAABIKA MIKOANI

**Na Mwandishi Wetu**

LICHA ya timu yake kupata ushindi wa mabao 2-1 dhidi ya wenyeji Mbao FC katika mechi ya Ligi Kuu Tanzania Bara iliyochezwa juzi, kwenye Uwanja wa CCM Kirumba jijini Mwanza, nahodha wa Yanga, Ibrahim Ajibu, amesema ushindi huo walioupata ulitokana na wachezaji kupambana kwa kiwango cha juu.

**Ajibu alisema kuwa mchezo huo na mingine ya mikoani ni migumu na timu yake inalazimika kutumia mbinu za ziada.**

Nahodha huyo alisema kuwa ushindi huo wa juzi umewaongezea morali kuelekea katika michezo mingine inayofuata ukiwamo wa Kombe la FA dhidi ya Namungo FC utakaochezwa Jumapili mkoani Lindi.

“Ushindi huu ulikuwa muhimu sana kwetu... tumetoka kupoteza mchezo uliopita, hivyo ilikuwa lazima kupata ushindi, tunashukuru tumefanikiwa lakini ligi ni ngumu, hasa kwenye michezo ya mikoani,” alisema Ajibu.

Aidha, alisema anashukuru mbinu za kocha wao, Mwinyi Zahera, katika kila mchezo ambazo zinawasaidia kuvuna pointi na kuendelea kujiimarisha katika msimamo wa ligi hiyo.

“Kama wachezaji tutaendelea kupambana na kuhamasishana katika kila mchezo, lengo letu ni kuhakikisha tunafanya vizuri kwenye ligi na hata kwenye Kombe la FA,” alisema Ajibu.

Aliongeza kuwa kwa sasa hakuna timu ambayo imejihakikishia kutwaa ubingwa na mechi zimebaki nyingi, hivyo lazima wapambane katika kila mchezo ili kupata ushindi.

“Kwenye ligi hakuna timu ambayo ina uhakika wa ushindi, kikubwa kwetu ni kupambana kuhakikisha tunashinda katika kila mchezo ulioko mbele yetu, tuna mchezo wa Kombe la FA dhidi ya Namungo... tunaelekeza nguvu huko kama wachezaji kuhakikisha tunafanya vizuri,” alisema Ajibu.

Kikosi cha Yanga kilirejea jijini Dar es Salaam kikitokea Mwanza na kuanza maandalizi ya kuwafuata Namungo, timu inayoshiriki Ligi Daraja la Kwanza.



Straika wa DTB FC, Focus Miengo (kushoto) akipambana kuwania mpira dhidi ya mchezaji wa Tuamoyo katika mechi ya Kundi C ya Ligi ya Soka Kanda ya Dar es Salaam iliyochezwa juzi jijini. DTB ilishinda mabao 3-2. **PICHA: HISANI YA DTB**

# *Makonda apongezwa kumgharamia Cassian*

**Na Mwandishi Wetu**

RAIS wa Mtandao wa Wasanii wa Injili na Maadili Tanzania, Dk. Godwin Maimu, amempongeza Mkuu wa Mkoa wa Dar es Salaam, Paul Makonda, kwa kujitolea kumsaidia gharama za matitabu mshindi wa shindano la ‘Bongo Star Search’ (BSS) mwaka 2009, Pascal Cassian.

Msanii huyo ambaye kwa sasa anaimba muziki wa injili alipata ajali hivi karibuni akiwa safarini kutoka Dodoma kurejea jijini Dar es Salaam na kuumia sehemu mbalimbali ikiwamo nyonga na kibofu cha mkojo.

Akizungumza na gazeti hili jana, Dk. Maimu alisema kitendo kilichofanywa na Makonda sio tu cha kiupendo, lakini ameonyesha uungwana wake kwa wananchi akiwa kama kiongozi mkubwa wa mkoa.

“Ameonyesha upendo, uungwana na utu licha ya kuwa yeye ni kiongozi mwenye majukumu mengi, ameonyesha kujali wasanii wa aina mbalimbali, kwa kweli tunampongeza na kumshukuru, na kwa jambo ili jema sio vibaya kwa viongozi wengine bila kujali nyadhifa zao wakijitolea kusaidia makundi mbalimbali ya watu, wasanii na wengineo,” alisema Dk. Maimu.

Pia Maimu alimpongeza Rais Dk. John Magufuli na serikali ya awamu ya tano kwa kujali wananchi wake bila kuangalia dini, kabila na tofauti nyingine zilizopo.

Naye Cassian amemshukuru sana Makonda na serikali pamoja na Watanzania wote waliojitoa kwa ajili yake na kuwataka waendelee kumsaidia hadi hali yake itakapoimarika.

## Michezo majeshi kuanza kesho Dar

**Na Mwandishi Wetu**

TIMU za majeshi zinatarajiwa kuchuana katika michezo ya majeshi itakayofanyika kuanzia kesho hadi Machi 9, mwaka huu, kwenye Uwanja wa Uhuru jijini Dar es Salaam, imeelezwa.

Akizungumza jana jijini, Mwenyekiti wa Baraza la Michezo ya Majeshi ya Tanzania (BAMMATA), Brigedia Jenerali, Suleiman Mzee, alisema kuwa majeshi yatakayoshiriki katika michezo hiyo ni Jeshi la Ulinzi la Wananchi Tanzania, Jeshi la Polisi, Jeshi la Kujenga Taifa, Vikosi vya Serikali ya Mapinduzi, Idara ya Uhamiaji, Jeshi la Magereza na Zimamoto.

Alisema kuwa timu hizo zitachuana katika soka (wanaume), ngumi (wanaume), netiboli (wanawake) wakati mpira wa mikono, wavu, kikapu na kulenga shabaha zitashiriki timu za wanawake na wanaume.

Alisema kuwa lengo la kuandaa michezo hii ni kuendeleza uhusiano, urafiki na udugu baina ya majeshi haya tofauti na vile vile kuibua na kuinua vipaji vya michezo kwa wanachama wake.

“Ninawaalika wananchi wote wa Dar es Salaam na mikoa ya jirani kuja kushuhudia michezo hii ili kujipatia burudani na ni fursa nyingine ya wananchi kuimarisha uhusiano, urafiki na ushirikiano na vyombo vinavyowalinda,” alisema.

Alimtaja Makamu wa Pili wa Rais wa Serikali ya Zanzibar, Balozi, Seif Ali Iddi, ndiye anatarajiwa kuwa mgeni rasmi katika ufunguzi wakati Waziri wa Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo, Dk. Harrison Mwakyembe ndiye atakayefunga michezo hiyo.

## DTB yang’ara na kutinga Sita Bora

**Na Mwandishi Wetu**

TIMU ya Diamond Trust Bank, imefanikiwa kutinga hatua ya Sita Bora ya Ligi ya Soka Kanda ya Dar es Salaam, baada ya kuifunga Tuamoyo ya Kigamboni mabao 3-2 katika mechi iliyochezwa juzi jioni kwenye Viwanja vya Islamic hapa jijini.

Bao la kwanza la Diamond Trust Bank lilifungwa na mshambuliaji wake tegemeo, Robert Kobelo, ambaye aliifanya timu yake iende mapumziko ikiwa mbele kwa bao 1-0.

Kipindi cha pili kiliendelea kwa kasi, lakini mshambuliaji mwingine wa timu hiyo, Juma Juma, alifanikiwa kufunga mabao mawili ambayo yaliwafanya waweze kusonga mbele katika mashindano hayo.

Timu hiyo iliyopo katika Kundi C linalojumuisha Magereza, Rungu FC, Faru Dume, Palyanda, Ungindoni, Boom FC, Abajalo na Tuamoyo, ilimaliza hatua hiyo ya makundi ikiwa katika nafasi ya pili kwa kujikusanyia pointi 18 nyuma ya vinara wa kundi hilo, Ungindoni ambao wana pointi 19.

Kila kundi hutoa timu mbili zinazosonga mbele katika ligi hiyo ambayo hutafuta bingwa wa mkoa na timu tatu bora zitafuzu kuingia moja kwa moja kwenye Ligi Daraja la Pili Taifa.

# Michezo

Ijumaa Februari 22, 2019

Nipashe




Rashford, United sasa kimeeleweka HABARI UK. 30



Mshambuliaji wa Yanga, Haritier Makambo (kulia), akijaribu kumpiga chenga beki wa Mbao FC, David Mwassa, katika mechi ya Ligi Kuu Bara iliyochezwa juzi, kwenye Uwanja wa CCM Kirumba jijini Mwanza. Yanga ilishinda mabao 2- 1. **PICHA: ANTHONY GERVAS**

## Zahera asimulia alivyoitesa Mbao

**Na Faustine Feliciane**

BAADA ya kupata ushindi wa mabao 2-1 dhidi ya Mbao FC katika mechi ya Ligi Kuu Tanzania Bara iliyochezwa juzi, Kocha Mkuu wa Yanga, Mwinyi Zahera, ametaja sababu ya kuondoka na pointi tatu ilitokana na wachezaji wake kujituma na kila mmoja kuweka dhamira ya kumaliza "uteja".

Zahera, aliendа mbali kwa kusema kuwa kipindi cha mapumziko wakati timu yao ikiwa nyuma kwa bao 1-0 katika chumba cha kubadilishia nguo, aliwaambia wachezaji wake kuwa wana nafasi ya kushinda mchezo huo.

Kocha huyo alisema kuwa hakuna mbinu za kiufundi alizowapa wachezaji wake zaidi ya kuwaaminisha kwamba wanaweza kushinda na wanachotakiwa ni kuendelea kupambana.

"Sikufanya chochote cha kiufundi, yaani sikutaka kubadilisha chochote, niliwaambia wana uwezo wa kushinda mchezo huo, wachezaji wenyewe kwa wenyewe walihamasishana, Ninja (Abdallah Shaibu) na Kelvin (Yondani) wenyewe waliwahamasisha wachezaji wenzao kuwa wanaweza kushinda wakipambana, na ndicho kilichotokea," alisema Zahera.

Kocha huyo alisema kuwa juhudi zilizoonyeshwa na wachezaji wake baada ya kuwa nyuma ndicho kitu kilichowapa nguvu ya kupata matokeo ya ushindi na "kuvunja mwiko" wa kufungwa na timu hiyo wakiwa ugenini.

"Kabla ya mchezo, nilisema historia haichezi mpira... nilikuja kwa lengo la ushindi, nashukuru tumetimiza jambo hilo, nawapongeza wachezaji wangu kwa kujituma na kupambana kupata ushindi huu," alisema Zahera.

Yanga imevunja mwiko wa kuwa 'teja' wa timu hiyo kwenye michezo inayofanyika kwenye Uwanja wa CCM Kirumba jijini Mwanza, kabla ya mchezo wa juzi Yanga haikuwahi kupata ushindi kwenye uwanja huo dhidi ya Mbao.

Zahera alisema baada ya kumalizika kwa mchezo huo sasa, wanaelekeza nguvu zao katika mechi ya Kombe la FA dhidi ya wenyeji, Namungo FC inayoshiriki Ligi Daraja la Kwanza itakayochezwa Jumapili kwenye Uwanja wa Kassim Majaliwa uliopo Ruangwa, Lindi.

# Simba, Azam kumaliza ubishi

**Na Somoe Ng'itu**

### ●●● Ni siku saba baada ya mabingwa hao watetezi kuwaliza Wana-Jangwani...

WASHAMBULIAJI wa kimataifa wa Simba Mganda, Emmanuel Okwi na Mnyarwanda, Meddie Kagere, wanatarajia kurejea dimbani wakati kikosi cha timu yao kitakachoivaa Azam FC katika mechi ya Ligi Kuu Tanzania Bara, itakayochezwa leo kwenye Uwanja wa Taifa jijini Dar es Salaam.

**Nyota hao wawili walikosekana katika mechi iliyopita dhidi ya African Lyon kutokana na kutumikia adhabu ya kadi tatu za njano, wakati timu yao ikiibuka na ushindi wa mabao 3-0.**

Akizungumza na gazeti hili jana, Kocha Mkuu wa Simba Mbelgiji, Patrick Aussems, alisema kuwa kikosi chake kiko tayari kwa mchezo huo muhimu licha ya kupata muda wa siku mbili za mazoezi baada ya kurejea kutoka ugenini jijini Arusha.

Aussems alisema kuwa licha ya rekodi ya timu yake "kumbeba", bado amewaandaa nyota wake kuingia uwanjani kwa lengo moja la kuondoka na pointi tatu na kuendelea kujiweka katika nafasi nzuri ya kutetea ubingwa wanaoushikilia.

"Tumekuwa na siku mbili za mapumziko, tumeanza mazoezi, kwa kifupi tuko tayari, tuko tayari kwa mchezo huo dhidi ya Azam," alisema Mbelgiji huyo.

Aliongeza kuwa Azam ni timu nzuri kutokana na kuundwa na wachezaji wengi wenye uzoefu na Ligi Kuu Bara na anatarajia kukutana na ushindani kutoka katika kikosi hicho ambacho nacho kitashuka uwanjani kikitokea ugenini jijini Tanga.

Naye Kocha Msaidizi wa Azam FC, Juma Mwambusi, amesema kuwa mechi hiyo inatarajiwa kuwa na ushindani kutoka kila upande na hakuna timu itakayoingia uwanjani ikiamini inakwenda kufungwa.

Mwambusi alisema kuwa wanaamini watapata matokeo mazuri katika mchezo huo ambao utatoa jibu la kikosi kipi kina timu na benchi bora zaidi kwenye ligi hiyo inayoshirikisha timu 20.

"Mchezo wa mpira ni maandalizi, ukiwa na maandalizi bora unaamini utapata matokeo mazuri, hii ni mara ya kwanza tutakutana nao huku tukijua tunakutana na timu ambayo msimu huu imekuwa na matokeo mazuri, tunaliamini benchi la ufundi," alisema Jaffer Idd, msemaji wa timu hiyo.

Alisema kuwa nahodha, Aggrey Moriss, ambaye timu yake itashuka uwanjani ikiwa na kumbukumbu ya kutoka sare ya bao 1-1 dhidi ya Coastal Union katika mechi ya mwisho, atarejea dimbani kwa ajili ya kuimarisha safu ya ulinzi baada ya naye kumaliza adhabu ya kadi tatu za njano.

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >